ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.

11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.

22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani

35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile

59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nne – Tarehe 27 Januari, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kaimu Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma): Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2012/2013.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani hati ya Hotuba ya Kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2012/2013.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ussi Jecha Simai (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala naomba kuwasilisha Muhtasari wa Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2013/2014.

Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 20

Kujaa kwa Eneo la Kuzikia la Mwanakwerekwe

Mhe. Nassor Salim Ali (Kny: Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa) – Aliuliza:-

Eneo la Mwanakwerekwe kwa sasa linaonekana limejaa na maiti au wachimbaji wa makaburi wanarudia humo kwa humo na maiti zinapandiana kwa sasa.

(a) Je, wizara yako ina mpango gani wa kutafuta eneo mbadala kwa wananchi wa Zanzibar hususan eneo la Waislamu.

(b) Je, eneo hilo lilipoasisiwa lilikuwa na ukubwa kiasi gani.

(c) Kwa wale watu ambao wamejenga ndani ya eneo la kuzikiana serikali ina mpango gani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mahmoud Muhammed swali lake nambari 20 lenye kifungu a, b na c naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:

Ni kweli kwa sasa eneo la makaburi la Mwanakwerekwe hasa kwa upande tunaozikiana Waislamu ni mdogo ukilinganisha na mahitaji. Hali hiyo imesababishwa na kupungua kwa eneo la awali na kuongezeka kwa idadi ya watu wanaoishi katika mji wa Zanzibar na viunga vyake ambao wanalitumia eneo hilo kwa kuzikiana.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a) Serikali imepanga kulitumia kwa kuzikiana eneo jengine la Kama walikozikwa baadhi ya wenzetu waliofariki katika ajali ya Meli ya M.V. *Spice Islanders*.

b) Eneo la makaburi la Mwanakwerekwe lilikuwa na ukubwa wa hekta 80 za mraba na kwa sasa baada ya kubadilika kwa matumizi ya

ardhi ya eneo hilo, zimebakia hekta 25 za mraba, na kwa wakati huo lilianzia eneo la Asha Fatuma katika Soko la Mwanakwerekwe.

c) Maeneo ya kuzikiana Mwanakwerekwe yamezungushiwa ukuta ili kuzuia uvamizi, lakini kwa wale ambao wataendelea na uvamizi taratibu na hatua za kisheria zitachukuliwa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwamba sasa hivi kumetokea watu wanakwenda katika maeneo ya makaburi na kuchimba mchanga katika maeneo yale, jambo ambalo linasababisha kuyafukua makaburi yale na kuziacha zile maiti nje.

a) Je, Mhe. Waziri anafahamu tatizo hilo.
b) Ikiwa anafahamu serikali inachukua hatua gani kuona kwamba jambo hili litadhibitiwa ili kuona maiti zile bado zinahifadhika kadiri ya vile zilivyokuwa zimekusudiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nitumie fursa hii kuwasihi sana wananchi wanaoendelea kuchimba mchanga katika maeneo ya makaburi tunayozikiana, binadamu baada ya kufika hatima yetu hapa duniani. Kwamba jambo hilo si zuri na si la kiungwana na jambo hilo pia linawapasa watafakari katika maisha yao ya leo na maisha yao ya baadae.

Kumfanyia marehemu tendo ovu lolote lile haistahiki, marehemu tunatakiwa tuwafanyie mambo mema kwa kuwaombea Mwenyezi Mungu baada ya kwishakuondoka hapa duniani ili watakapofika mbele ya haki Mwenyezi Mungu awape shufaa na awasamehe yale madhambi yao ambayo yamewakuta.

Sasa kwa kweli watu wa namna hii wanaofanya kitendo kama hiki wanafanya kitendo cha kinyama, bora niseme ni kitendo cha kikafiri kabisa si kitendo ambacho kinapaswa kufanywa na Waislamu au waungwana au waumini wowote wa dini ambazo zipo hapa duniani.

Lakini je, suala kuwa tunalifahamu? Serikali kwa ujumla inafahamu matatizo ambayo yanafanywa na watu wasio waaminifu katika kuchimba mchanga katika maeneo mengi ya mji wetu likiwemo eneo la Mwanakwerekwe.

Swali la pili ni kwamba hatua gani serikali itafanya. Hatua za kisheria kwa kweli serikali inajitahidi kuchukua kwa watu ambao wanabainika kufanya vitendo hivi. Nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba, sasa

tutajitahidi tuwe makini zaidi katika kuona watu wanaofanya vitendo hivi ambavyo si vizuri tunawachukulia hatua za kisheria kufuatana na sheria ambazo zipo katika taasisi zetu na ambazo tumezipitisha hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa amekiri kwamba eneo la makaburi la Mwanakwerekwe limekuwa dogo kwa mujibu wa kuongezeka idadi ya watu kila siku, lakini na kwa kuwa kumejitokeza baadhi ya watu baada ya kuzika wanazijengea kaburi ili kulizuia eneo lile kwa muda mrefu kuzikiwa tena.

Je, serikali inatoa wito gani kwa wale wanaojengea makaburi na kwa yale makaburi yaliyokwishajengewa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu mama sasa hivi kuwa eneo letu limekuwa dogo na ndio maana tunatarajia kuhamishia eneo la Kama. Ni busara tu kwa sisi wenye maiti kutumia busara katika kuona jambo ambalo tunalifanya linafaa au halifai. Sasa hili jambo linatokana na imani ya mtu mwenyewe, sasa ningemuomba Mhe. Mohammed Mbwana serikali kama serikali tusingeweza kutoa tamko juu ya jambo hili, ningeomba jambo hili tukalipeleka kwenye Ofisi ya Mufti tukapata fat-wa kuhusu imani ya jambo hili.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ningependa aliambie hili Baraza lako tukufu kwa wale maiti ambao wako pale katika maeneo ya Mwanakwerekwe na eneo ambalo kwa sasa limejaa, eneo ambalo liko wazi utaratibu wake wa watu kuingia na kutoka haujamilikiwa.

Je, serikali ina mpango gani wa kuweza kulihifadhi eneo lile ambalo watu wamezikwa ili watu wasiendelee kuliteka eneo lile na kufanya mambo mengine ambayo hayakukusudiwa kwa shughuli hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, sisi serikali tutaona uwezekano wa kuweza kutengeneza utaratibu wa kuhifadhi maeneo wanayostiriwa marehemu, lakini jambo hili ni jambo la kheri hasa kwa waislamu wote, ningetoa wito kwa waislamu kama walivyojitokeza waislamu wa mwanzo katika kulihifadhi eneo lile.

Lakini vile vile ningetoa wito kwa watu wa dini nyengine katika maeneo yao, kwa sababu maeneo yale ni maalum na ni nyeti kwa ajili ya kuwahifadhi wenzetu, basi sisi pia tukashajihisha hasa Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi. Ninachotaka kuwahakikishia kwamba Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa tutaanzisha utaratibu wa kuchangia fedha kwa ajili ya kulijenga eneo lile, lakini mchango huo utakapokuja hapa Baraza la Wawakilishi basi sisi Wajumbe wa Baraza na sisi tuombe kheri za Mwenyezi Mungu tutoe michango yetu ili tulihifadhi eneo lile.

Nam. 8

Vikundi vya Ushirika Kufanyiwa Ziara

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibiwa swali langu naomba kidogo nifanye marekebisho.

Swali linasema kwa kuwa serikali huwaomba, naomba itiwe huhimiza, wananchi kuunda vikundi vya ushirika ili kujikwamua na hali ngumu ya maisha vikiwemo vikundi vya ufugaji, kilimo na uvuvi; ambapo uendeshaji wa vikundi hivyo unahitaji taaluma na kuwezeshwa kifedha. Pamoja na azma hiyo nzuri ya kuwasaidia wananchi inaonekana bado serikali haijawa tayari kutekeleza hili.

Je, serikali ina mpango gani wa kuvifanyia ziara vikundi hivyo ili kuona uwezo wao na kuweza kuviwezesha.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 8 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Saba inayoongozwa na mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imejidhatiti kutekeleza kwa ufanisi azma ya kuwasaidia wananchi ili waweze kujikwamua na hali ngumu ya maisha na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi.

Serikali imekuwa na utaratibu maalumu wa kufanya ziara ya kuvitembelea vikundi vya ushirika. Katika kipindi cha Julai – Disemba 2013, vikundi mbali mbali vya ushirika vilitembelewa na kupatiwa misaada. Mhe. Mama

Mwanamwema Shein na Mhe. Mama Asha Seif Ali Idd wametembelea jumla ya vikundi 10 Kisiwani Pemba na kutoa misaada yenye thamani ya shilingi 4,909,300.

Aidha, mimi mwenyewe binafsi katika kipindi hicho nimetembelea jumla ya vikundi saba (7). Vikundi hivyo ni pamoja na Nia Safi *SACCOS* iliyopo Kinyikani, Pemba ambayo inajumuisha vikundi vitano vidogo vidogo. Kikundi hicho nilikichangia shilingi 1,500.000 baada ya wao wenyewe nao kuahidi kuchangia shilingi 1,500,000 kwa ajili ya kununulia vifaa vya kilimo.

Vikundi vyengine nilivyovitembelea *Mungu ni Mwema* kilichoko Kitambuu ambacho nilikipa msaada wa shilingi 500, 000 na Kikundi cha *Jogoo hafi kwa Utitiri* kilichoko Kidongochekundu Unguja nilichokisaidia shilingi 300,0000. Kikundi cha ushirika cha Kikwajuni nacho nilikichangia shilingi 200,000.

Katika kuimarisha uendeshaji wa vikundi vya ushirika Idara ya Ushirika chini ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto huwa inatoa mafunzo ya aina mbali mbali. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2013, idara imetoa taaluma juu ya uongozi, ujasiri amali na uendeshaji wa vikundi vya ushirika kwenye vikundi vya ushirika 230 katika wilaya zote za Unguja na Pemba.

Kwa ujumla vikundi vya ushirika ni vingi , lakini vitaendelea kutembelewa, kupatiwa taaluma na kila utakapopatikana uwezo vitasaidiwa. Ahsante.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri bado kuna vikundi vidogo vidogo katika shehia na mawilaya bado havijapata kutembelewa wala kufanyiwa taaluma ya vikundi vya ushirika. Na kwa kuwa serikali huyaona sana mashirika makubwa ambayo tayari yashaweza kujiwezesha kuliko vikundi vidogo vidogo ambavyo vikundi hivyo ndio vinavyozaa vikundi vikubwa.

Je, Mhe. Waziri, haoni kutowawezesha vikundi vidogo vidogo ni kuwavunja moyo wananchi hao.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, naomba nimueleze Mhe. Mwanajuma Faki kuwa vikundi hivi vyote tulivyovisaidia sio vikundi vikubwa ni vikundi vidogo vidogo. Lakini kwa sababu sijawahi kufika katika shehia yake kama tulivyokubaliana basi anaona kwamba vikundi vidogo vidogo havisaidiwi,

lakini *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia nitafika katika eneo lake na vikundi vyake vidogo vidogo tutavisaidia na tutavielimisha.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri atakubaliana nami kwamba Mama Shein anafanya kazi nzuri ya kupigiwa mfano.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba Mhe. Mama Mwanamwema Shein, Mama Asha Balozi wanafanya kazi ya kupigiwa mfano.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuniruhusu nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa vikundi vya ushirika vya akinamama vipo vyenye juhudi kubwa na kazi zao ni nzuri sana. Je, serikali ina mpango gani wa kuviwezesha vikundi hivyo pale yanapotokea maonesho ya nchi za jirani kama vile Uganda, Burundi ili na wao kuweza kushiriki katika maonesho hayo kwa ajili ya kujitangaza zaidi na kujitafutia masoko.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa sasa hatuna mpango wa kuvipeleka katika maeneo hayo aliyoyataja kutokana na kwamba fedha hatuna, fedha tulizonazo ni kidogo tunajitahidi kuwapeleka angalau kwenye maonesho ya Tanzania Bara pamoja na hapa hapa Unguja, lakini kwa nchi za nje inakuwa tabu kidogo, lakini kama wizara ikipata uwezo basi tutaweza kuwapeleka mpaka huko.

Nam. 30

Kufanya Vibaya kwa Zanzibar kwenye *'Kagame Cup'*

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:-

Timu ya Soka ya Taifa ya Zanzibar (*Zanzibar Heroes)* imewavunja moyo sana Wazanzibari wengi pale ilipofanya vibaya sana kwenye mashindano ya mwaka 2013 ya *Kagame Cup* yaliyofanyika nchini Kenya.

Kwa kuwa wachezaji nguli mwaka 2013 hawakuingizwa kwenye timu hiyo wakiwemo Nadir Haroub, Nassor Said 'Cholo' na Mlinda mlango Mwadini Ali, ambao huisaidia sana timu yetu kufanya vizuri.

Je, ni sababu gani ya msingi iliyopelekea wachezaji hao (*professionals*) kuachwa kwenye timu.

Mhe.Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na naomba nimjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake namba 30 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli timu yetu ya Taifa ya Zanzibar (*Zanzibar Heroes)* katika mashindano yaliyopita ya Kagame nchini Kenya haikufanya vizuri. Na ni kweli baadhi ya wachezaji wenye uzoefu akina Nadir Haroub na mlinda mlango Mwadini Ali hawakuteuliwa kujiunga na timu hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mchezaji Said Nassor (Cholo) aliteuliwa ingawa hakuweza kushiriki katika mashindano hayo baada ya kuumia. Sababu hasa za kutoteuliwa baadhi ya wachezaji zinatokana na mwalimu mwenyewe ambaye kimsingi ndiye mwenye jukumu la kuteua timu hiyo kutokana na sifa na vigezo anavyoviona vinafaa.

Hata hiyo, ziko taarifa zinazoeleza kwamba baadhi ya wachezaji walioachwa walikuwa viwango vyao vya uchezaji vimeshuka kulingana na uoni wa mwalimu, na wengine ni kutokana na ukosefu wa nidhamu.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, nataka nikushukuru kwa dhati kabisa kupata nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza, lakini kabla sijauliza swali hili ningeomba unipe sekunde kama kumi au kumi na tano nitoe neno la shukurani tu.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati jana ilifanyika fainali ya mashindano ya timu ya wanawake ya Mpira wa Miguu Amani, na kwa bahati nzuri timu kutoka Jimbo la Kwahani imechukua ubingwa kwa mashindano haya ya mpira wa miguu. Naomba niwapongeze vijana wa Jimbo la Kwahani kwa kuchukua ushindi huu na kuwatakia mafanikio mema katika safari yao ya mpira wa miguu kwa wanawake.

Mheshimiwa swali langu la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, mimi nataka Mhe. Waziri akiri kwamba kilichofanyika hapa sio kigezo cha uwezo wa wachezaji. Kwa sababu kabla timu hiyo haijateuliwa manung'uniko yalianza, labda atueleze na hii inaonekana kwamba labda hatuna *format* maalumu ya kuchagua makocha.

Nataka kujua Mhe. Waziri wana utaratibu gani wa kuchagua makocha ambao watakuwa na ubora kwa kufunga mikataba. Kwa sababu miaka michache

tulikuwa tuna Bushiri, hatukuchukua muda kaja Morocco na sasa hivi amekuja Salum Bausi. Sasa nataka kujua Mhe. Waziri, utaratibu wanaotumia kuwachagua makocha wenye uwezo na uzalendo kwa nchi yao.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kabla sijajibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi nami naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wizara kumpongeza yeye na timu ya jimbo lake kwa kuwa bingwa wa Timu hii ya Mpira wa Miguu ya Wanawake.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nijibu kwamba, masuala haya ya kuchagua wachezaji kwanza ni suala la kiufundi, katika mchezo wa mpira mafundi huwa ni makocha wenyewe. Kwa hiyo, inawezekana mtu kwa utashi wake au kwa muono wake akaona fulani labda ameachwa ni mzuri zaidi, lakini kwa maoni ya mwalimu ambaye ndiye kocha tuliyempa jukumu yeye ndiye aliyeona kuwa aliyemteua ndio anafaa zaidi. Kwa hivyo, manung'uniko na mambo mengine yanaweza yakasemwa sana lakini la msingi mtu ambaye yuko kwenye *field* ana uwezo na ujuzi, nadhani tumpe nafasi afanye kazi yake.

Kuhusu makocha ni jukumu la *ZFA* kumuona kocha yupi anafaa na kumteua. Ni kweli zamani kulikuwa na makocha Bushiri na watu wengine sawa, lakini kila zama na zama zake na kocha anakuja anapanda na anashuka kiwango chake, jambo la kawaida katika nchi zote duniani. Kwa hivyo, *ZFA* yenyewe ndio inaona vigezo gani imeweka kwa mwaka huu au kwa kipindi hiki kwa ajili ya kuteua kocha. Kwa hivyo, sisi ambao si wajuzi sana wa suala hili nadhani tuwaachie watu ambao wana ujuzi wao na wana maarifa yao katika suala hili Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri, wakati anajibu swali hili la pili amesema kwamba *ZFA* inategemea uwezo na mipago yake kuajiri kocha.

Je, kutokana na jibu hilo haoni kwamba ipo haja sasa serikali kupitia wizara husika kama vile mfano Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete alipomuajiri kocha kutoka Brazil na hivi sasa kutoka Denmark. Je, serikali kupitia Rais wetu Dr. Ali Mohamed Shein na serikali yake hii, haioni kwamba ipo haja kuajiri kocha kwa ajili ya kuendeleza mpira wetu wa miguu hapa Zanzibar ili kuweza kuwasaidia *ZFA*.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa sasa serikali haioni umuhimu wa kuajiri kocha wa kigeni, tunachofanya sasa hivi serikali ni kuhakikisha kwamba makocha wa

Kizanzibari wanapewa taaluma na ujuzi ili waweze kujengwa uwezo na ndio maana tukamtaka, kumuomba na kumualika Kocha wa Taifa wa Italy aje hapa awafundishe makocha wetu jambo ambalo amekubali.

Kwa hivyo, la msingi sio kuajiri kocha wa kigeni, la msingi ni kuwawezesha makocha wetu wa Kizanzibari kuwa na uwezo wa kufundisha. Kwa hivyo, hili ndio jambo ambalo kwa sasa tunaliona ni muhumu zaidi.

Nam. 33

Uwanja wa Gombani Kupewa *ZFA*

Mhe. Nassor Salim Ali: Aliuliza**:-**

Kwa kuwa masuala ya michezo wa mpira wa miguu yanaendeshwa na kusimamiwa na chama husika cha mpira wa miguu *ZFA* kwa hapa Zanzibar.

Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya viwanja vya mchezo huo wa mpira wa miguu kama vile kiwanja cha Amani na Gombani Pemba kupewa *ZFA* kusimamia viwanja hivyo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Nassor Salim Ali, swali lake namba 33 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi, kwamba masuala yote ya mchezo wa mpira wa miguu Zanzibar yanasimamiwa na Chama cha Soka cha Zanzibar (*ZFA*). Hata hivyo, Serikali haioni kwamba kuna haja viwanja vya michezo vya Amaan na Gombani kusimamiwa na Chama hicho.

Sababu kubwa ya kuona hivyo ni kuendeleza lengo maalumu la serikali la kujenga viwanja hivyo ambalo ni kukuza michezo mbali mbali nchini na sio mpira wa miguu peke yake. Kinachohitajika kionekane katika viwanja hivyo ni kufanyika mashindano ya aina zote ikiwemo mpira wa miguu, riadha, *hockey*, mpira wa vikapu, michezo ya ndani na shughuli nyingine zinazohusiana na mambo ya kitaifa.

Hivyo, viwanja hivyo kusimamiwa na chama kinachoshughulikia mchezo mmoja ni kupoteza lengo lililokusudiwa na serikali la kujenga na kuendeleza viwanja hivyo kwa maslahi ya michezo yote.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, mbali na majibu ya Mhe. Waziri, lakini katika ulimwengu wote masuala ya soka kama alivyojibu kuwa yanasimamiwa na Chama husika cha mchezo huo wa mpira, lakini Mhe. Naibu Spika, ukienda hata kwa wenzetu Tanzania Bara kwamba taratibu zote zinazohusiana na masuala haya ya mpira wa miguu na viwanja vya mpira wa miguu huwa vinasimamiwa na *TFF*. Hivyo, ndio nikauliza kwamba iko haja kwamba serikali kuwashirikisha kwa njia moja au nyengine kuweza kusimamia viwanja hivi vya michezo.

Mhe. Naibu Spika, katika masuala haya ya Mpira wa Miguu hasa hapa Zanzibar na Tanzania Bara, kule Tanzania Bara *TFF* mchezo wowote ambao unachezwa katika Uwanja wa Taifa au viwanja vyovyote viliopo ndani ya Tanzania, huwa kuna mgao maalumu wa chama husika cha Mkoa pamoja na chama cha Taifa yaani *TFF*.

Je, serikali haioni kwamba iko haja kuiangalia sheria yao kuhakikisha kwamba chama husika cha *ZFA* pamoja na Wilaya kwa sababu sisi hatuna Mkoa, tuna Wilaya hupewa mgao wa 10% kama vile wanavyofanya kule Tanzania.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba viwanja hivi viwili vinamilikiwa na serikali havimilikiwi na *ZFA* Taifa, wala Wilaya, wala havisimamiwi na *ZFA* Taifa, wala Wilaya.

Kwa hivyo, viwanja hivi ni kwa ajili ya michezo yote, ndio ukaona pale riadha wamewekewa *tartan* wakitaka kutumia wanatumia na taratibu zinafanyika tukijaaliwa wizara itahakikisha kwamba na kiwanja cha Gombani nacho kiekewe *tartan* kwa ajili ya shughuli za mchezo wa riadha. Kwa hivyo, tunachozungumza kwamba mapato yanayotokana na shughuli hizo hatuoni umuhimu kwamba kipewe *ZFA* wilaya ya Mjini au *ZFA* Wilaya ya Chake Chake hiyo haiwezekani, kwa sababu vile ni viwanja vya serikali ambavyo mapato yake yaende katika taasisi ambayo imekusudiwa.

UTARATIBU

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, niliposema kwamba Tanzania Bara viwanja vyote vinamilikiwa na serikali, lakini kuna mgao huwa wanapata chama husika. Ndio nikauliza kwamba serikali haioni haja kuvigaia mgao wa 10% chama husika ili kuweza kujiendesha. Kwa sababu Mhe Naibu Spika, wanategemea mapato ya mpirani ili kuweza kuendesha mpira huo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, Sera ya Michezo ya Tanzania Bara na ya Zanzibar ni nchi mbili tofauti. Kwa hivyo, hatuwezi kufanya kila ambacho wanafanya Tanzania Bara na sisi tukakiiga hapa. Hizi ni nchi mbili tofauti katika masuala ya michezo.

Kwa hivyo, hatuwezi kuiga tu kwa sababu wenzetu *TFF* wanafanya hivi na Zanzibar tufanye. Kuna sera mbili tofauti ambazo zinaongoza masuala ya michezo katika nchi zetu hizi.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika katika Baraza lako tukufu kwa hali ya afya njema.

Mhe. Naibu Spika, tumejionea wenyewe katika kutimiza miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba sasa hivi Uwanja wa Amani hautoshelezi na haukidhi haja ya kuchukua watu wengi, maana yake unafurika na watu wengine hawapati kuona sherehe ambazo zimekusudiwa.

Je, Mhe. Waziri, atakubaliana na mimi kwamba sasa hivi imefika wakati wa kutafuta sehemu ya kujenga kiwanja kikubwa zaidi kuliko cha Amani.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kiwanja cha Amani ni kiwanja ambacho kilijengwa kwa shughuli maalumu ya michezo na wenzetu hivi sasa hawatumii viwanja vya michezo kwa ajili ya sherehe za kitaifa. Nakumbuka Mhe. Naibu Spika, tulikwenda na Mhe. Spika, Ghana na wenzangu hapa tukaona mfano ambavyo wenzetu wanavitumia viwanja vyao vya sherehe mbali na viwanja vyao vya michezo.

Kwa hivyo, wazo la Mhe. Asha Bakari Makame, tunalichukua na serikali tutalifanyia kazi kuona namna gani tutatenganisha viwanja vya michezo na viwanja vya shughuli za sherehe za kitaifa, tutalifanyia kazi Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Waziri, kwanza nikupongeze kwa majibu yako mazuri sana na mimi nilikuwa nimeshaweka swali kuwa ikiwa *ZFA* italipwa, basi na mimi nilikuwa nataka niombe nilipwe chama changu cha riadha.

Mhe. Waziri, umesema kuwa wakati wote uwanja wa Gombani utaweka *tartan* na kwa kuwa sisi sasa hivi tumeandaa Chama cha Riadha kuleta mashindano ya kitaifa. Mhe. Waziri, ni lini hiyo *tartan* itakamilika?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Makamo wa Rais Taifa wa Chama cha Riadha Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, suala hilo ni la kibajeti na lipo katika maandalizi ya Bajeti ya mwaka 2014/15, naomba kwamba tukija na bajeti inayohusiana na uwekaji wa *tartan* katika uwanja ya Gombani Pemba naomba tuunge mkono kwa sababu tunamtayarishia yeye mazingira.

Nam. 16

Matengenezo ya Meli ya L.C.T JITIHADA

(Mheshimiwa Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 23

Huduma Tembezo kwa Magonjwa Yasiyoambukizwa

Mhe. Hija Hassan Hija: (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma): Aliuliza**:-**

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwanza nimpe pole kwa kulazwa Hospitalini kuanzia jana usiku.

Sasa Mhe. Naibu Spika, swali lake namba 23, naomba lijibiwe.

Kwa kuwa katika maeneo mengi ya nchi yetu yamekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wa maradhi yasiyoambukizwa na kwa kuwa tiba pamoja na madaktari wa wagonjwa bado ni tatizo.

Je, ni lini serikali itaanzisha utaratibu wa kutoa huduma sehemu tofauti kwa ajili ya kutoa ushauri, kuelimisha pamoja na kutibu magonjwa hayo yasiyoambukiza kama inavyofanyika kwa baadhi ya huduma nyengine za afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu**:-**

Kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 23 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na hoja na Mhe. Mwakilishi kwamba kumekuwa na ongezeko la magonjwa yasioambukiza sio tu hapa nchini kwetu bali kote duniani. Baada ya wizara kulifahamu hili ndipo uamuzi wa

kuanzisha kitengo maalumu ambacho kitakuwa na jukumu la kuratibu magonjwa yasiyoambukiza na kutoa miongozo ya kujikinga pamoja na matibabu.

Katika jitihada za kuhakikisha huduma hizo zinaimarika, Wizara ya Afya kwa kupitia kitengo chake cha Maradhi yasiyoambukiza kimefanya tathmini ili kuweza kubaini mahitaji halisi kwa vituo vyote vinavyotarajiwa kutoa huduma hizo. Kufuatia tathmini hiyo, muongozo wa matibabu umetengenezwa na orodha ya vifaa muhimu kwa ajili ya kutoa huduma hizo umetayarishwa. Kwa sasa muongozo wa matibabu tayari umeshachapishwa na vifaa vyote vilivyoagizwa tayari vimefika nchini.

Wizara ya Afya imeteua vituo 34 vya huduma ya Afya ya msingi ambavyo vinatarajiwa kutoa huduma za magonjwa hayo. Uteuzi huo umelenga kuwasogezea wananchi huduma hizo kwa vile zimekuwa zikipatikana katika ngazi za Mahospitali tu. Kinachofuatia sasa hivi ni kuwapatia mafunzo ya kisasa wafanyakazi wa vituo hivyo na huduma kuanzishwa rasmi.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hayo wananchi waliweza kupata huduma hizi kupitia siku za afya ya vijiji ambazo zimekuwa zikisimamiwa na timu za afya za Wilaya. Pia, kupitia matukio mbalimbali ambayo kwa njia moja au nyengine yalihusisha kazi zinazoendana na huduma za magonjwa yasiyoambukiza kama vile katika maadhimisho ya siku ya kisukari duniani, maombi kutoka ofisi mbalimbali za serikali, maadhimisho ya miaka 50 ya sherehe za Mapinduzi, n.k.

Aidha, elimu imekuwa ikitolewa kupitia njia mbali mbali ikiwemo vyombo vya habari, magazeti na mikutano ndani ya jamii. Mikutano mingi iliyofanywa ilienda sambamba na kuanzishwa vikundi vya mazoezi ambavyo vimepewa jina la *"Obama fitness Club"* na Mawe Matatu cha kule Micheweni. Vikundi vya Obama vipo katika maeneo ya Mahonda, Mkwajuni, Bambi ya bondeni, Mtende, Gymkhana, Fuoni, Jamhuri *hall* (Wete), Madungu na Skuli ya Ng'ombeni (Mkoani). Lengo la kuanzishwa vikundi hivi ni kuhamasisha wananchi kuimarisha siha zao, kwani moja kati ya matatizo makubwa yanayotuathiri wananchi wa Zanzibar ni kutofanya mazoezi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba idara imeanza kuandaa muongozo unaosambazwa katika vituo husika na wataalamu wahusika. Zoezi hili Mhe. Naibu Spika, limeenda sambamba na ongezeko la nguvu kazi. Kwa maana hiyo wataalamu na vitendea kazi.

(a) Je, naomba kujua mbali ya muongozo ambao wizara imetoa wamejipanga vipi kuwapata wataalamu ili waende kufanya kazi katika vituo hivyo husika.

(b) Ametaja maeneo ambayo vikundi vya mazoezi vimeanza kazi, wizara sasa ina mpango wa kuhamasisha shehia zote za Zanzibar kuunda vikundi kazi kwa ajili ya mazoezi ili kupunguza maradhi haya ambayo yameenea Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya:

(a) Mhe. Naibu Spika, suala la nguvu kazi kama nilivyolieza kwamba wale walioko tayari ni wafanyakazi ambao wameshapata taaluma. Kilichopo ni hiyo *course* iliyotayarishwa maalumu ambayo ni ya kuwaongezea uwezo. Kwa hivyo, wafanyakazi wetu waliomo katika vituo jumla ya kazi yao ni hiyo. Kilichokuwa kinahitajika ni kuwaelimisha zaidi na hiyo kazi itafanywa halafu huduma zitaendelea.

(b) Mhe. Naibu Spika, suala la kuunda vikundi Wizara ya Afya inachokifanya ni kuhakikisha kwamba watu wawe na afya na tunatoa maelekezo kwamba watu wafanye mazoezi. Wafanye mazoezi kwa vikundi au mtu mmoja mmoja. Tunapolijibu suala hili si mara moja si mara tatu leo nalijibu kuelekeza watu kwamba jamani kwa njia yoyote mazoezi tufanye. Mfano sisi Wawakilishi hapa tunakaa tangu asubuhi mpaka usiku tumekaa kitako na tukiamka asubuhi tumekaa kwenye magari, na tukitoka hapa tumetoka kwenye magari hiyo si afya njema kwetu. Tuna Timu hapa za Baraza la Wawakilishi, tuna timu hapa za Wanawake na Wanaume Wawakilishi wangapi wanajihusisha na hilo au wangapi kati yetu asubuhi angalau anakwenda hata kilomita moja.

Kwa hiyo, hilo sio suala la kuhamasishwa tu, unatakiwa wewe binafsi uwe na dhamira ya kutaka kulinda afya yako na katika kulinda afya yako unaweza ukajiunga kwenye kikundi unaweza ukafanya peke yako mradi lile lengo lifikiwe. Sasa kama ni hivyo hao Masheha, vijana, Baraza la Michezo wananisikia na wengine sote tulioko hapa, kwa hiari zetu tufanye mazoezi. Katika umri huu tuliokuwa nao kuugua maradhi hayo kama hatufanyi mazoezi hatuwezi tukayaepuka.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa hivi sasa kumezuka ugonjwa wa *typhoid* na zaidi kisiwani Pemba ambao unaathiri watu kwa kiasi kikubwa.

Je, ugonjwa huu Mhe. Naibu Waziri, chanzo chake ni nini na hatua zipi zitachukuliwa za kudhibiti ugonjwa huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, *typhoid* si moja kati ya maradhi tunayoyazungumza hapa. Kwa sababu haya ni maradhi ya kuambukiza na sisi tunazungumza maradhi yasiyoambukiza, lakini kwa faida ya Mwakilishi naomba nimjibu kwamba maradhi hayo yanasababishwa na uchafu, vyakula tunavyokula kama hatuvipiki uzuri au hatuvioshi vizuri.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kabla sijauliza kwanza naomba kumpa pole Mhe. Jaku Hashim Ayoub, jana kwa kupata mkong'oto, nampa pole sana na nafikiri leo hajaja nadhani ameumia.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu mazuri. Katika uchunguzi wao wizara yao imeona kuwa kuwepo na vikundi vya mazoezi ni moja katika tiba nzuri ambayo inaweza kumuondolea mtu maradhi.

Je, Mhe. Naibu Waziri, huoni kwamba ipo haja sasa ukaweka bajeti maalumu ya kuvisaidia vikundi hivyo ili kuokoa gharama nyengine ambayo itakuhusu huko mbele ya safari.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri aliyoeleza Mhe. Naibu Waziri wa Afya, nilitaka kuongezea kuhusu haya maradhi ya kuambukiza.

Mhe. Naibu Spika, suala hili la maradhi ya kuambukiza nimeshapeleka maelezo au taarifa serikalini kama ni suala linalokuwa kubwa. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu wangu kasema kwamba maisha tunayoishi sasa ni tofauti mfano mzuri daladala. Hata mtu akitoka pale Mlandege kuja Darajani anapanda daladala.

Kwa hivyo, tumebadili tabia za maisha tukirudi nyumbani sisi na ki-*remote* hakuna mtu anayeshughulika na mazoezi.

Mhe. Naibu Spika, nilialikwa China na moja lilogundulikana na wachina kwamba gharama kubwa ya matibabu ya afya inatokana na watu kwamba hawafanyi mazoezi. Kila raia anangoja augue halafu aende hospitali na akifika hospitali akiwa hakupata matibabu anaanza kulaumu, lakini yeye mwenyewe kuchukua dhamana akajilinda na afya yake kabla hajaumwa limekuwa ni tatizo sugu na gharama za afya zinapanda, moja ya sababu ni hiyo.

Kwa hivyo, serikali imetuagiza kwamba tutayarishe mpango kwa kushirikiana na wizara mbili, Wizara ya Michezo na Wizara ya Mazingira. Kwamba tuhakikishe kwamba kila mtu ujumbe anaupata, afya kwanza kuliko tiba yaani kinga ni bora kuliko tiba. Kinga hiyo ina namna mbili; moja ya kuweka mazingira safi. Mhe. Mwajuma Mdachi, kauliza hizo.

Lakini la pili, na sisi wenyewe kuhakikisha kwamba tunafanya mazoezi na tunajilinda. Tunashirikiana na Wizara ya Habari katika kuandaa hili na hivyo vikundi vinavyoambiwa kwamba viende mpaka kwa Masheha hivyo vilioko mpaka Kizimkazi na Uzini ni kwa sababu ya shughuli zetu Wizara ya Afya, kutokana na hichi kitengo tulichokisema. Kwa hivyo, tunashikirikiana kulifanya hilo.

Suala alilolisema Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, linafanana na hili kwamba tunahitaji kujilinda tusingoje kutibiwa. Sasa unaposema tuweke pesa kifungu maalumu kwa tiba maana yake tunaepuka wajibu wetu na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, uzito wako nimeshakwambia mara tatu au nne kwamba si uzito mzuri kwa afya yako. Naomba ushirikiane na mimi tufanye mazoezi pamoja tujilinde kwanza.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya au kwa bahati nzuri nalazimika kuliweka sawa kuhusu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, lililotokea jana.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu unipe dakika mbili nilieleze.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, jana kaenda kufanya usanii akitaka sifa na kazipata. Kwa sababu keshaandika kwenye vyombo vya habari. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, hakufanyiwa lolote isipokuwa kawachokoza askari, akawatukana mpaka matusi ya nguoni na mnawajua askari. Waheshimiwa nawaambia nyote tuheshimu utaratibu. Nilifikisha agizo hili serikalini kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja imegeuka kama soko. Serikali ikanambia hata kama unaweza kuweka jeshi kulinda nidhamu za serikali Mhe. Waziri weka.

Tumetafuta kikundi cha jamii kusaidia kuweka utaratibu huo umeanza kufanikiwa, hospitali imeanza kuwa na heshima, baadhi ya Waheshimiwa mkifika mnasema sisi Waheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kaenda Hospitali saa 4. Askari wakamwambia Mheshimiwa utaratibu wa kutizama wagonjwa ni saa 12 mpaka 1:30 na 7 mpaka 8:00 na 10 mpaka 11, hivi sasa si wakati. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, akalazimisha wakamwambia Mheshimiwa unataka tukuvunjie heshima. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, akamtafuta Munir Zakaria.

Mimi akanipigia simu niko nyumbani sijisikii vizuri akanambia kuwa nina matatizo njoo unisaidie. Nikamwambia kwamba nisubiri dakika kama 15 nijitie maji halafu nije. Nikafanya hivyo kwa kuona kwamba Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ana matatizo. Kumbe alikwishamtayarisha Munir Zakaria ili apate vyombo vya habari, nafika pale namkuta Munir Zakaria ananikimbilia mimi kutaka kuni-*interview*, namuuliza Munir Zakaria wewe umekuja kutizama mgonjwa gani? Aaah maana yake hili suala la kijamii, namwambia nakuuliza saa hizi umekuja kutizama mgonjwa gani?

Nikamwambia sikiliza, nisingependa suala hili ulifanye la habari, hili suala linahusu Utawala nimetoka kama Waziri na kuja kumsikiliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ana tatizo hili, nisingependa ukaliingiza kwenye vyombo vya habari. Akanijibu lazima tuliingilize, nikamwambia sasa nakwambia Munir Zakaria mimi Waziri wa Afya au wewe?

Nikawambia sikiliza, madhali wewe ni Waziri wa Afya msaidie Mhe. Jaku Hashim Ayoub, na mnakumbuka ile *caption* mkiitizama nilikuwa nafanya hivi. Mimi nilikuwa sijui kama ameshaweka ile *camera*. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, anakuja ananambia Mhe. Waziri vipi? Nikamjibu Waziri wa Afya yule pale atakusaidia nikazungusha uso nikatoka. Sikurudi tena na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, akapiga simu sikujibu tena. Kwa sababu alitaka kufanya usanii!

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kafanya usanii wa kutaka sifa kazipata, Waheshimiwa tukifika pale twende na heshima zetu tufuate utaratibu wa Hospitali.

Mhe. Naibu Spika, samahani kidogo juzi nilikuwa Nairobi kumtizama Dr Malik, tumefika pale na gari ya Ubalozi. Nimeshuka pale, askari ana kidudu kile anakufunua mpaka chupi! Hatizami wewe ni nani wala nani. Huko unakokwenda kuna wagonjwa hatujui unakwenda na nini. Tukishaachiwa sote na kila mtu anasachiwa, na ukishafika mle Hospital amri ni ya *nurse*. Tumetaka kwenda wakati sio *nurse* akasema "*no*", kitu ninachoweza kuomba mpaka nimpigie daktari wangu. Huo ndio utaratibu wa heshima ya hospitali.

Tunakwenda China kila Hospitali kuna walinzi, wanalinda utaratibu wa Hospitali. Tulindeni utaratibu wa Hospitali ionekanae ni Hospitali, ile ni Hospitali sio soko. Kwa hivyo, tukienda tujitambulishe, na Mhe. Naibu Waziri wa Afya, amesema Mheshimiwa yeyote anakwenda akikionesha kitambulisho chake cha Baraza la Wawakilishi anasaidiwa, lakini huwezi ukaenda saa 4 ukasema unataka kumuona mgonjwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, huyu huyu wiki moja iliyopita kaenda na watu 7 akawaomba askari hawa hawa wakamruhusu. Tangu lini mgonjwa mmoja anatizamwa na watu 7. Kumaliza watu 7 wengine wanakuja, askari akamwambia unakwenda wapi? Aaah namfuata Mhe. Jaku Hashim Ayoub juu. Akaambiwa huko tayari kuna Mhe. Jaku Hashim Ayoub na watu 7, askari akamzuia yule, akapiga simu yule, kupiga simu akamwambia Mhe. Jaku Hashim Ayoub, itabidi ushuke wewe na watu wako huyu hapa haji uko.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, huyu huyu wiki iliyopita kasaidiwa, jana amezuiwa imekuwa kasheshe ili apate sifa. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kafanya usanii! Ahsante sana.

Nam. 37

Zanzibar kuwa na Vyanzo vyake vya Nishati ya Umeme

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza **:-**

Kumekuwa na ongezeko la ghafla la bei za umeme nchini kiasi ambacho watu wengi wameamua kurudi kwenye vibatari, mishumaa, kuni na mkaa. Kwa kuwa *ZECO* (Zanzibar) inaongoza kwa kuuza umeme ghali kwa wananchi wake ukilinganisha na nchi nyengine za Kiafrika,

Je, ni lini Zanzibar itaanzisha vyanzo vyake vya umeme badala ya kutegemea umeme kutoka Bara ambao ni ghali mno.

Mhe. NaibuWaziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu **:-**

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimwia Mwakilishi swali lake nambari 37 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Kabla ya kumjibu swali lake la msingi napenda kumfahamisha Mheshimiwa kwamba sio kweli kuwa Zanzibar inaongoza kwa kuuza umeme ghali kwa wananchi wake, ukilinganisha na nchi nyengine. Kwa mfano huu wananchi wa Zanzibar wananunua umeme kutoka Tanzania Bara. Lakini bado wananchi wa Zanzibar wanalipa umeme kwa bei rahisi ukilinganisha na wenzetu wa Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:

Katika kujibu swali la msingi ni kwamba serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa kutafuta vyanzo tofauti vya kuzalisha umeme hapa Zanzibar na sasa

hivi yupo mtaalamu kutoka Jumuiya ya Ulaya ambaye anaendelea kufanya utafiti wa upatikanaji wa umeme mbadala.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Waziri, serikali ilitoa fursa ya kuwa wawekezaji wa umeme waje hapa ili kuweza kusaidia kuondoa msongamano aidha wa kupanda bei au kuweza kupata wananchi unafuu wa bei.

Je, Mhe. Waziri, wizara yako imefikia wapi wawekezaji kama hawa ili kuweza kutoa nafuu kwa hawa wawekezaji wa hapa.

Mhe. NaibuWaziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ni kweli na mpaka sasa ndivyo ilivyo tunawakaribisha wawekezaji wanaotaka kusaidia katika kuzalisha umeme na kuuza katika *grid* ya taifa bila ya matatizo yoyote. Tatizo linalojichomoza linakuja kwenye suala la bei. Mhe. Naibu Spika, unajua kwamba sisi tunauza umeme kwa *unit* moja shilingi 222 kwa mwananchi ni *average price* hiyo kwa ajili ya umeme. Lakini karibu wote waliokuja sasa hivi umeme wao kwa kuununua sisi, hii 222/= tunauza sisi kwa wananchi, lakini umeme wao kwa kuununua sisi katika *ZECO* unaanza kwa *unit* moja shilingi 800 mpaka 1,000.

Kwa hivyo, katika hali hiyo bado tunaendelea kuzungumza nao kwamba lazima wafikie katika bei ambayo tutaweza kuwauzia wananchi wetu. Bei hizi kubwa wanazotuletea karibu wawekezaji wote, si mmoja, si wawili, si watatu. Mnazungumza vizuri juu ya suala la ujenzi, mitambo na kila kitu, lakini mkija suala la sasa mnunue umeme unaanza kwenye shilingi 800 kwa *unit* moja mpaka shilingi 1,000, hilo ndio tatizo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, swali alivyojibu mwanzo Mhe. Waziri kama alivyoulizwa kwamba Zanzibar ni miongoni mwa nchi ambazo zenye kuuza umeme au wenye kutoza ada ya umeme kwa bei kubwa. Na kimsingi Mhe. Naibu Spika, suala la umeme linaanza na uwekezaji wenyewe wa umeme. Kwa hiyo, mtu baada ya kuwekeza na kurejesha gharama zake hapo ndio ataweza kuuza bei ya umeme.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ili Zanzibar tuweze kuwa na umeme wa bei nafuu inabidi tuwe na vianzio tofauti tofauti vya umeme. Sasa hivi tunacho kianzio kimoja kutoka kwa wenzetu Tanzania Bara. Lakini kwa kuwa hivi karibuni imegundulika Zanzibar kwamba tuna rasilimali kubwa sana ya gesi ambayo baada ya kuvunwa gesi hiyo inategemewa utapatikana umeme mwingi sana

hapa Zanzibar. Na jambo pekee ambalo tunahisi kwa sababu hatuna makaa ya mawe, hatuna maporomoko ya maji makubwa ambayo ni sehemu ya vianzio vya maji.

Je, Mhe. Waziri, kuna kikwazo gani mpaka sasa hivi kinachosababisha hii rasilimali yetu ambayo tumefanyiwa utafiti tukaambiwa tunayo ya gesi ikaanza kuvunwa angalau wananchi wakaanza afueni ya kupata umeme ambao umekuwa kwa bei kubwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa mimi mwenyewe nimefanya utafiti, tulikwenda Songosongo wananchi kule wanapewa umeme bure kwa sababu ya ile gesi inayotoka pale kutokana na faida inayopatikana. Sisi Zanzibar hatutaki tupewe umeme bure? Je, ni lini Mhe. Waziri hiyo rasilimali ataanza kuifukua huko ardhini ili tuweze kufaidika nayo? Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ni kweli zipo nadharia zinazoeleza kwamba Unguja kuna gesi na mafuta. Nadharia hizi zinahitaji kufanyiwa utafiti ili zithibitishwe kwamba kweli Unguja tuna gesi na mafuta. Mhe. Hamza Hassan Juma, amehudhuria maelezo mafupi yaliyofanywa na kampuni zinazofanya kazi za uchimbaji mafuta si mara moja, si mara mbili, lakini nadhani ameelezwa mpango au muda watakaochukua mpaka kuweza kuhakikisha kwamba mafuta yapo.

Na kwa mara ya mwisho semina ilipokuwepo hapo juu katika Ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi na Wajumbe, walikuwepo wataalam walitwambia kwamba suala la kufanyia utafiti mpaka kufika kuthibitisha suala hilo halitapungua miaka mitano, lakini hasa linakwenda mpaka miaka kumi ikibidi.

Sasa hili Mhe. Hamza Hassan Juma, analijua, kwa hivyo nadhani tusiwatie tamaa wananchi sasa hivi kabla hii nadharia kuthibitishwa. Ikishakuthibitishwa hii nadharia hapo tena litakuja suala la kuhakikisha kwamba kweli gesi na mafuta yapo katika ardhi yetu.

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2012/13 – Wizara ya Nchi (AR) Ikulu na Utawala Bora

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe juzi Ijumaa iliwasilishwa ripoti moja tu kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Leo tutaendelea na Wizara mbili zilizobakia na baadae tumwite Mwenyekiti

asome taarifa mpya ya Kamati. Kwa hivyo sasa hivi tunamwita Waziri wa Nchi (AR) Ikulu na Utawala Bora kuwasilisha ripoti yake ya utekelezaji.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji kwa maagizo yaliyotolewa na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, nazo Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, pamoja na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa na afya njema tukiendelea vizuri na shughuli zetu za hapa Barazani.

Sina budi pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kupata bahati kwa mara nyingine tena kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha utekelezaji wa maagizo mbali mbali yaliyotolewa na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zinazoigusa Wizara yangu.

Mhe. Naibu Spika, natoa shukrani za pekee kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na Kamati ya Kusimamia Hesabu za Serikali. Kamati hizi chini ya uongozi wa Wenyeviti wao, Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura, pamoja na Mhe. Omar Ali Shehe, Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake.

Mhe. Naibu Spika, Kamati zimekuwa zikitusaidia sana katika kutuongoza na kutushauri ili kufanikisha utendaji wa shughuli zetu kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kuweza kuchangia hotuba zetu na hoja ambazo tunaziwasilisha hapa Barazani na kutoa miongozo iliyo sahihi.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/14 jumla ya maagizo 14 yalitolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati au Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza. Maagizo yote yameweza kufanyiwa kazi na ofisi yangu. Aidha, michango na ushauri iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe imekuwa chachu kwa ofisi yangu katika kutekekeza mipango ya Serikali kwa wakati na ufanisi ulio bora.

Mhe. Naibu Spika, mnamo mwezi wa Agosti mwaka jana muundo wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ulibadilika ambapo Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Usajili na Kadi

za Utambulisho na Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ iliondolewa na kuhamishiwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Aidha, katika mabadiliko hayo, Idara ya Utawala Bora, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali na Tume ya Mipango zilihamishiwa katika ofisi hii. Kwa sasa muundo mpya wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi unajumuisha ofisi na idara zifuatazo:

1. Ofisi ya Faragha.
2. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.
3. Tume ya Mipango.
4. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
5. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
6. Idara ya Mawasiliano Ikulu.
7. Idara ya Utumishi na Uendeshaji.
8. Ofisi ya Usalama wa Serikali *(GSO).*
9. Ofisi ya Mdhamini Pemba.
10. Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi Nchi za Nje.
11. Idara ya Utawala Bora.
12. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi.

Utekelezaji wa Maagizo

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kwa ruhusa yako niwasilishe kwa ufupi utekelezaji wa maagizo yote 14 yaliyotolewa na Baraza lako tukufu kama ifuatavyo:-

Agizo la kwanza, tuwatumie Wazanzibari walioko nchi za nje ili kutusaidia kutuunganisha na wawekezaji, wahisani na mashirika mbali mbali ya kusogeza maendeleo ya nchi yetu.

Utekelezaji, Idara inaendelea na mchakato huo kwa kufanya mazungumzo na jumuiya za Wazanzibari walioko Canada, Marekani na Uingereza. Maelezo zaidi Wazanzibari waliopo katika maeneo hayo wanaendelea na juhudi za kutafuta wawekezaji na misaada kwa ajili ya Wazanzibari kwa kutumia Ofisi za Kibalozi na Wazanzibari wenzetu ambao tayari wapo katika hizo nchi nilizozitaja yaani *DIASPORA.*

Agizo la pili, kutafuta jengo au ofisi ambayo itakuwa nje ya jengo la Ikulu ili kurahisisha *DIASPORA* kupata fursa ya kuitembelea ofisi yao kiurahisi zaidi. Ushauri huu utekelezaji wake, kazi imeanza na tunaendelea kuufanyia kazi

kwa sababu si rahisi kupata jengo kwa haraka. Lakini ushauri tumeupokea na kwa hatua ya awali Idara inayowaratibu Wazanzibari wanaoishi nje imehamishiwa katika jengo lililokuwa la Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi *(ZIPA)* yaani pale nje Ikulu.

Agizo la tatu Mhe. Naibu Spika, kuratibu kikamilifu shughuli za Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi. Utekelezaji, uratibu unafanywa kwa mujibu wa Mpango Kazi wa Idara na ni endelevu.

Agizo la nne, ni uingizwaji wa sera za Ofisi ya Usalama wa Serikali *(GSO)* kwamba hauridhishi. Utekelezaji, juhudi za makusudi zimeanza kufanyika ambapo kwa mwaka wa fedha 2013/14 ofisi hii imepangiwa bajeti ya shilingi milioni 61.6 kutoka shilingi milioni 54.9 za mwaka 2012/13, sawa na ongezeko la wastani kwa asilimia 12.2.

Maelezo zaidi, juhudi zinapelekea ofisi hii kuingiziwa wastani wa shilingi milioni 4.5 kwa mwezi katika mwaka huu wa fedha 2013/14 kutoka wastani wa shilingi milioni mbili kwa mwaka wa fedha uliopita 2012/13.

Agizo la tano, kuharakishwa upatikanaji wa hatimiliki ya majengo ya Ikulu pamoja na yale ya Serikali. Utekelezaji wake Mhe. Naibu Spika, jengo la Ikulu ya Mnazi Mmoja tayari limeshapatiwa hatimiliki. Kwa maelezo zaidi hatimiliki za majengo mengine zipo katika hatua za ukingoni kukamilika. Majengo hayo ni *Bwefum State Lodge, Kibweni Palace, Maisara State Lodge* (Bosnia), *Migombani State Lodge, Mazizini I State Lodge* na *Mazizini II State Lodge.*

Agizo la sita Mhe. Naibu Spika, matengenezo madogo na makubwa ya Idara ya Utumishi na Uendeshaji yawekwe pamoja na yasitenganishwe. Utekelezaji, matengenezo hufanywa kwa mujibu wa mahitaji na vifungu husika kufuatana na mwongozo wa utayarishaji wa bajeti. Hili nalo tunashirikiana na Wizara ya Fedha kuona ya kwamba yale matumizi makubwa na matumizi tuweze kuyachanganua ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, agizo la saba, ni kumualika Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando kuja kuliona jengo la *ZIPA.* Utekelezaji, ofisi imefanya mawasiliano na Mhe. Mtando kwa njia ya simu na barua yenye kumbukumbu namba AR/IKLB/90/5Vol.IV/78 ili aweze kuja kuliona jengo hilo. Mhe. Mtando ameahidi tuwasiliane nae wakati huu wa vikao vya kawaida vya Baraza la Wawakilishi ambavyo vinaendelea ili aweze kuja kuona hali halisi ya ukarabati unavyoendelea katika jengo lile.

Agizo la nane, ukarabati wa jengo la Ikulu ya Kibweni. Utekelezaji, ofisi tayari imewasilisha waraka Serikalini yaani Baraza la Mapinduzi ili kuomba kuwa na mradi maalum wa matengenezo ya majengo yote ya urithi ambayo ni *gazzetted.*

Agizo la tisa, kufanyiwa ukarabati wa hali ya juu Ikulu ya Mkoani. Utekelezaji, Ikulu ya Mkoani tayari imeshafanyiwa matengenezo makubwa yaliyojumuisha jengo litakalotumiwa na walinzi ambapo kwa sasa Ikulu hiyo ipo katika hali ya kuridhisha kabisa. Matengenezo naweza kusema yapo kwa asilimia 95. Hivi sasa matengenezo yanayoendelea ni ya ukamilishaji wa nyumba ndogo ya askari polisi pamoja na ukuta unaoizunguka Ikulu hiyo.

Agizo la kumi Mhe. Naibu Spika, ni kuandaa vipindi maalum *(documentary)* ambazo zitaonesha kazi za Mhe. Rais alizozifanya katika sekta mbali mbali na baadae zioneshwe katika Shirika la Utangazaji Zanzibar. Utekelezaji Mhe. Naibu Spika, vipindi 7 vya TV na 12 vya redio vimeandaliwa na kurushwa hewani na *ZBC.* Vipindi vya TV pia vimeoneshwa kwa njia ya sinema katika vijiji 15 vya Unguja. Mpango kama huu wa kuonesha kwa njia ya sinema upo njiani nao kuupeleka katika Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kupitia vipindi hivyo wananchi wamekuwa wakipata taarifa ya shughuli ambazo Mhe. Rais amekuwa akizitekeleza siku hadi siku.

Agizo la kumi na moja, ni kuezekwa kwa paa na kuchimbwa kwa kisima katika jengo la Ikulu ya Wete. Utekelezaji wake Mhe. Naibu Spika, utafiti uliofanywa na *ZAWA* umebaini kwamba maji ya chumvi yapo karibu katika eneo la Ikulu ya Wete. Kwa hivyo kumepelekea kushindikana kuchimba kisima. Aidha, mawasiliano yamefanywa na Ofisi ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu matengenezo ya Ikulu ya Wete kama walivyofanya hapo awali. Maelezo zaidi Mhe. Naibu Spika, uunganishwaji wa maji unasubiri mradi wa maji ambao unatekelezwa kwa maeneo ya Wete. Ni imani yetu kwamba baada ya kukamilika mradi ule mkubwa wa usambazaji maji vijijini na mijini unaoendelezwa na *ZAWA,* basi shida ya maji katika Ikulu ya Wete itatoweka kabisa.

Agizo la kumi na mbili Mhe. Naibu Spika, ni kutengenezwa kwa barabara iendayo katika jengo la Ikulu ya Chake Chake. Mhe. Naibu Spika, nathubutu kusema kwamba utekelezaji wa agizo hili umekamilika kwa asilimia mia moja, yaani barabara imeshatengenezwa na imekamilika. Tunawashukuru sana ndugu zetu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na hasa idara ile ya UUB.

Agizo la kumi na tatu, ni kuitishwa kwa tenda ya matengenezo ya majengo ya Ikulu Pemba. Utekelezaji, tenda imeitishwa na ujenzi unaendelea.

Agizo la mwisho Mhe. Naibu Spika, ni kuzilipia bima gari za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Utekelezaji, utaratibu wa kuzilipia bima gari za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambapo magari yote ya Pemba yameshalipiwa bima, na ya Unguja nayo pia yamo njiani kuona kwamba magari yote yanalipiwa bima kama agizo la Serikali lilivyoelekeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa muhtasari huo ndio ulikuwa utekelezaji wa maagizo tuliopewa. Kwa kuhitimisha Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itaendelea kupokea ushauri na maelekezo kutoka katika Kamati zako za Kudumu na Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa jumla. Hatua hii itaiwezesha ofisi yangu kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kutusaidia kutatua changamoto zinazotukabili. Ni matarajio yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wataendelea kushirikiana na ofisi yangu katika jukumu letu la kuwahudumia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma kwa kutuwezesha kuwa wazima na kutupa nguvu za kuweza kushiriki kikao hiki muhimu kwa manufaa ya Zanzibar na wananchi wake. Naomba pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maelezo ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuhusu utekelezaji wa maagizo na ushauri tulioupokea kutoka kwa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa kwa mwaka 2012/13.

Mhe. Naibu Spika, vile vile napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani maalum na za kipekee kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii waliopita na wa sasa kwa michango, ushauri, maelekezo na miongozo waliyoitoa na wanayoendelea kuitoa kwa Ofisi ya Makamo wa Kwanza na Rais. Hakika ushauri na miongozo yao imekuwa ni chachu ya mafanikio yaliyopatikana juu ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kuwashukuru Wajumbe wenzangu wote wa Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano wao wa dhati kwangu mimi binafsi pamoja na watendaji wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, baada ya shukrani hizo kwa heshima naomba nitoe maelezo ya utekelezaji wa maagizo na ushauri uliotolewa na Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2012/13 kama ifuatavyo:-

Kuhusu utekelezaji wa maagizo. Agizo namba moja lilikuwa ni juu ya Idara ya Mazingira kulifukia shimo la Bumbwini kwa kufuata taratibu za kimazingira. Kwa kutambua kuwa mikataba ya ujenzi wa barabara husainiwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na kampuni ya ujenzi na kuhusisha suala la uchimbaji wa kifusi kwa ajili ya ujenzi huo. Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ilifuatia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ili kuona kuwa shimo la Bumbwini linafukiwa kupitia kampuni ya *MECCO* iliyoruhusiwa kuchimba.

Kazi ya kufukia ilifanywa na kampuni hiyo ingawa sio kwa kiwango cha kuridhisha. Matatizo ya kimkataba baina ya kampuni ya *MECCO* na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambayo yameitaka Serikali kutoa eneo la uchimbaji ndio yaliyochangia kutokuendelezwa ipasavyo kwa eneo hilo.

Agizo la pili, Wajumbe wa Kamati kupatiwa kanuni za kudhibiti matumizi ya msumeno wa moto. Mhe. Naibu Spika, kila Mjumbe wa Kamati amepatiwa nakala moja ya kanuni ya kudhibiti matumizi ya msumeno wa moto na nakala moja ya kanuni ya kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki kwa mujibu wa barua yenye namba OMKR Nam. 10/2 Vol. II ya tarehe 10/12/2012.

Agizo la tatu, kutokufunguliwa kwa njia ya kuelekea pwani iliyofungwa na Ndugu Khatib Jecha. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa suala hili halisimamiwi moja kwa moja na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Idara ya Mazingira imelipeleka suala hili kwa taasisi husika ambazo ni Idara ya Mipango Miji na Vijiji, Idara ya Ardhi na Usajili, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini, pamoja na Sheha wa Nzwardini kwa hatua za kufanikisha suala hilo.

Agizo la nne, kunahitajika kuwekwa mashine katika bandari ya Malindi na viwanja vya ndege Unguja na Pemba kwa ajili ya ukaguzi wa mizigo ya kila aina na kiwango. Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais iliandaa *enrollment* ya utekelezaji wa Sheria ya Dawa za Kulevya ambayo imewashirikisha wadau wote wa mapambano dhidi ya dawa ya kulevya. Katika utekelezaji wake gharama za vitendea kazi mbali mbali zimeainishwa. Taasisi zinazohusika kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na Serikali kwa ujumla inaendelea kuwasiliana na taasisi mbali mbali za kimataifa kwa kutafuta msaada wa utekelezaji wake, kwa vile ununuzi wa vifaa hivyo kwa kupitia bajeti zetu za Serikali peke yake ni ngumu sana.

Utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Kwanza, wananchi wanahitajika kupatiwa elimu ya kutosha ili waweze kufuata sheria na utaratibu wa kuvuna maliasili zisizorejesheka. Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira imetoa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine ambayo pamoja na mambo mengine imegusa sera, sheria na kanuni za kimazingira. Jumla ya wanachama kutoka vikundi 21, vikundi 13 kutoka Unguja na 8 kutoka Pemba vya ulinzi shirikishi ni miongoni tu mwa wadau waliopatiwa elimu hiyo ikiwa ni pamoja na kanuni ya usimamizi wa maliasili zisizorejesheka.

Vikundi vya ulinzi shirikishi vilivyobahatika kupatiwa elimu hiyo ni Shehia ya Jang'ombe, Mwera, Mtofaani, Bumbwini Mafufuni, Fukuchani, Chwaka, Ukongoroni, Kilimani, Mkokotoni, Jambiani, Kama, Uroa na Matetema kwa upande wa Unguja.

Sambamba na hayo, mashindano ya mpira wa miguu na insha kwa wanafunzi yalifanyika kwenye maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ili kuwa ni sehemu ya kuelimisha jamii juu ya uhifadhi wa mazingira.

Ushauri wa pili, Taasisi ya Viwango Zanzibar *(ZBS)* kwa kushirikiana na taasisi nyengine za Serikali kuhakikisha kuwa bidhaa chakavu zinazoingizwa nchini ni zile zenye viwango. Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imewasiliana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko juu ya suala la kuweka viwango kwa bidhaa chakavu za umeme na *electronic* ambazo zinaingizwa nchini. Baada ya mawasiliano Wizara ya Biashara iliomba maafisa wawili kutoka Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa ajili ya kuunda kamati ya kulishughulikia suala hili. Majina hayo yamepelekwa na mkutano mmoja wa wadau umefanyika wa kuangalia mambo muhimu yanayofaa kuzingatia.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira imewasilisha taarifa zote zinazohusiana na bidhaa chakavu za umeme na *electronic* ili *ZBS* iweze kuchukua hatua zinazohusika.

Ushauri wa tatu, kuweka utaratibu wa kufuatilia athari za kimazingira kabla ya utekelezaji wa miradi. Mhe. Naibu Spika, mahusiano na mashirikiano baina *ZIPA*, Kamisheni ya Utalii, Idara ya Misitu, Idara ya Mawasiliano, Idara ya Mipango Miji na Vijiji, na Idara ya Ardhi na Wilaya juu ya tathmini ya athari za kimazingira yameimarishwa. Aidha, mapitio ya Sheria ya Mazingira yamezingatia mapungufu ya sheria yaliyokuwepo juu ya tathmini za athari za kimazingira.

Ushauri wa nne, ufinyu wa bajeti na uhaba wa usafiri kwa Ofisi Kuu Pemba. Mhe. Naibu Spika, bajeti za Idara zote za Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ni ndogo. Kila mwaka tunapopata nyongeza ya bajeti huzingatia maagizo mbali mbali ya Kamati za Baraza la Wawakilishi. Aidha, juhudi mbali mbali zimefanyika kutafuta usafiri kwa ajili ya Idara ya Mazingira Pemba na Ofisi Kuu.

Kwa upande wa Idara ya Mazingira ya Pemba gari iliyokuwa ya mradi wa *SMOLE* tuliiomba na sasa ipo Idarani hapo kwa shughuli mbali mbali za ufuatiliaji wa shughuli za kimazingira. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2013/14 Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imeweka fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari la Ofisi Kuu Pemba.

Ushauri wa tano, marekebisho ya Sheria ya Mazingira. Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imefikia katika hatua nzuri kuandaa Rasimu ya Sheria ya Mazingira kulingana na changamoto inayokabiliana nazo sasa hivi. Ofisi itawasiliana na Kamati yetu kuweza kukaa na Kamati hiyo inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa ajili ya kupata ushauri wao katika rasimu hiyo kabla ya mchakato wa kuipeleka Serikalini. Nia yetu kazi hii ifanyike punde tu baada ya kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi.

Na ushauri wa sita, kuna haja kwa Viongozi wa Jimbo na Naibu Sheha kulitembelea eneo la Rumbwende Kangani kwa lengo la kulifanyia tathmini. Aidha, ni vyema kwa viongozi hao kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira na ya Misitu kufikiria kutafuta eneo mbadala kwa ajili ya kuvuna rasilimali hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Idara yake ya Mazingira kwa kushirikiana na Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka ilifika katika eneo la Rumbwende Kangani ambalo lilikuwa linachimbwa mchanga na wananchi bila ya kufuata taratibu. Kufuatia hali hiyo taasisi hizo zilizuiliwa uchimbaji huo ili kutokana na kuwa eneo hilo halijaruhusiwa kutumika kwa ajili ya shughuli hiyo. Baada ya wananchi hao kuzuiliwa walitakiwa watume maombi ya kutaka kufungua shimo la mchanga katika eneo lao, lakini hadi hivi sasa bado hawajawasilishwa maombi yao ili taasisi husika ziweze kuyafanyia kazi maombi hayo.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais naomba kuwasilisha utekelezaji wa maagizo hayo ya kamati kwa 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika: Sasa kwa makubaliano yetu kwamba zikishawasilishwa utekelezaji wa ripoti hizi na mwenyekiti anasoma taarifa yake ya ripoti mpya, halafu tunachangia kwa pamoja. Kwa hivyo sasa hivi ninamwita mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Hamza Hassan Juma.

Na wale wenye nia ya kuchangia, hapa nina jina la mjumbe mmoja tu, kwa hivyo mwenye nia anaweza kuleta tukaweza kujipanga vizuri katika mchango.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ninapenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza kutoa michango katika ripoti hizi za Kamati, lakini kabla sijaanza hivyo Mhe. Naibu Spika, ni vizuri kidogo nikajaribu kuweka sawa baadhi ya mambo kabla sijaanza kusoma ripoti mpya.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa utaratibu huu tumeuanzisha hivi karibuni inawezekana ukawa na changamoto za hapa na pale, lakini ninaamini kila siku zikienda changamoto tutaweza kuziweka sawa.

Mhe. Naibu Spika, katika ripoti hii ya mwaka huu inawezekana kuna baadhi ya mambo ambayo tuliagiza katika ripoti iliyopita. Kwa kuwa utaratibu wetu Mawaziri wanakuwa ripoti hizi hawatuletei moja kwa moja kwenye kamati isipokuwa zinawasilishwa moja kwa moja hapa Barazani wakati wa vikao. Kwa hivyo inawezekana kuna baadhi ya mambo ambayo yanaweza yakajitokeza yakawa kama ni maagizo na mapendekezo katika ripoti ya mwaka huu ikawa katika ripoti ambayo Waheshimiwa Mawaziri walipokuja kutoa maelezo inawezekana kwamba wameshayatolea ufafanuzi.

Kwa hivyo naomba kama kuna mambo yatakuwa yanajirejea, naomba kwa kweli muweze kuvumilia, lakini kutokana na huu mfumo wetu ambao tuliokuwa nayo kwa sababu kama ingelikuwa ripoti hizi Mhe. Waziri wanatuletea moja kwa moja kwenye kamati, basi ninaamini kuna mambo mengine yasingeweza kujirejea.

Lakini kimsingi kwa kweli kwa niaba ya kamati ninawashukuru sana Mawaziri wote watatu; Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais, lakini vile vile, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwa kweli maagizo na maelekezo mengi ya kamati kama walivyosema tulikuwa na mashirikiano nao makubwa, mengi kwa kweli walikuwa wameyatekeleza.

Hata hivyo, jambo moja katika ripoti yangu litaweza kujitokeza tena hasa katika hizi ripoti za Kamati Teule. Mhe. Naibu Spika, ripoti hizi za kamati tunashukuru sana kwamba serikali kwa kweli wanazifanyia kazi na wanazitekeleza kwa vizuri. Lakini bado katika masuala ya ripoti za Kamati Teule bado kuna mambo mengi ambayo sasa hivi yamekuwa kiporo na inawezekana kila tutakapokuwa tunazungumza katika ripoti hizi yakawa yanajirejea.

Moja kati ya mambo ambayo nitajaribu kulitolea mfano na ambalo ni kadhia kwa wananchi wetu ni suala la mwekezaji wa Hoteli hii ya Cristal's Inn pale Paje, ambapo Kamati yangu ilikwenda na pamoja na kwamba agizo Nam.32 ambalo lilieleza kwamba kuhusu lile jiwe lililoekwa pale kwa ufadhili wa mwekezaji huyu wa Hoteli ya Cristal na unyanyasaji ambao anaoufanya kwa wananchi wa pale Paje kwa kuwazuia njia ya kupita.

Mhe. Naibu Spika, ukiacha suala hili la jiwe la nyumba za Polisi ambalo lililoandikwa pale limeekwa na mwekezaji wa Hoteli ya Cristal, lakini bado ule unyanyasaji wenyewe wa kuweka mageti ya kuwazuia wananchi kuweza kwenda baharini, hili tatizo bado limekuwa sugu. Na tatizo hili kwa kweli si suala la kuekwa mwaka mzima mpaka tunapata ripoti tukaambiwa bado linashughulikiwa.

Mhe. Naibu Spika, tulipokwenda na kamati tulikuta barua ya Tawala za Mikoa, Halmashauri, ambayo inayomtaka mwekezaji yule kuondoa lile geti ili wananchi waweze kupita kwenda baharini. Agizo lile mpaka leo kwa kweli halikutekelezwa pamoja na jeuri anayoitoa mwekezaji yule na kusema kwamba serikali yote ipo mikononi mwake. Mhe. Naibu Spika, hii mpaka leo yule mwekezaji ameshindwa kuondoa lile geti lake na kuweza kuwaruhusu wananchi kupita kwenda kutumia fukwe za bahari na shughuli zao nyengine, ni kweli yale maneno yake yanathibitika kwamba ametuweka mikononi.

Kwa hivyo mimi bado naomba sana na kwa bahati kwa kuwa kuna mabadiliko ya wizara, nitamuomba Mhe. Waziri wa Nchi, ambae sasa hivi amekabidhiwa masuala ya Serikali za Mitaa basi tuandae siku ambapo kamati au kwa utaratibu wowote mwengine, tuende nae akashuhudie yeye mwenyewe na atagundua kwamba kuna maandiko ambayo yametoka katika wizara yake, kwenye Halmashauri yake lakini yameshindwa kutekelezwa.

Sasa sijui mwekezaji huyu ni mwekezaji wa aina gani. Lakini vile vile, mwekezaji kutokana na kuzuia na kuweka vizuizi vya kuelekea baharini, ameweza vile vile kumzuia mwekezaji mzalendo kuweza kulitumia eneo lake. Na matokeo yake eneo lile sasa hivi analitumia yeye, amejenga pale vibanda vya kuekea wageni na analaza wageni ndani ya eneo la mzalendo.

Mhe. Naibu Spika, huyu si mwekezaji. Lakini vile vile kuna ukiukwaji mwengine wa sheria za ardhi ambao tutakapokuja kuzungumzia suala la ripoti ya ardhi, tutakuja kulizungumza. Sasa mimi nilikuwa naomba Mhe. Naibu Spika, sisi tunapokwenda kwa wananchi tukachukua matatizo lakini vile vile tukaishauri wizara, mimi naomba Mawaziri pamoja na shughuli nyingi ambazo walizokuwa nazo lakini na haya vile vile yanakuwa ni ya msingi.

Lakini pamoja na hayo mengine mengi Mhe. Naibu Spika, serikali imeweza kuyatekeleza, lakini kubwa zaidi ninataka niseme agizo la kamati yetu kuhusu Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuhakikisha kwamba sherehe za miaka 50 zinakuwa kubwa za aina yake. Kwa kweli hapa kamati yangu inapongeza sana pamoja kwamba kuna baadhi ya wananchi ambao hawajui umuhimu wa Mapinduzi ya Zanzibar wanabeza, wanasema tumetumia fedha nyingi. Lakini Mhe. Naibu Spika, hata sisi Waswahili tunapokuwa na sherehe za watoto wetu, hasa wale tunaowazaa mwanzo Mhe. Mhe. Naibu Spika, unajikamua lakini kuhakikisha kwamba sherehe ile inakuwa kubwa.

Sasa hili ninadhani Mhe. Naibu Spika, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kuweza kutumia gharama kubwa kwa ajili ya maadhimisho ya miaka ya 50 ya mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, hii ilikuwa ni haki yetu kwa serikali na kwa kweli hili lilikuwa ni wajibu wetu.

Hili Mhe. Naibu Spika, leo vizazi vingi nikiwemo mimi mwenyewe hata hayo mapinduzi yenyewe sikuyaona. Sasa kama leo mimi mwenyewe mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, nina umri wa miaka 50 kasoro mmoja, mapinduzi sikuyaona na wakati mimi sasa hivi ninakaribia kujukuu na wengine wenye umri wangu mimi wameshajukuu, je kama hatukuweza kufanya jambo likawakumbusha mpaka wale vijukuu vyetu kwamba hii nchi yetu ilipata uhuru wake kutokana na mapinduzi na mapinduzi haya ndio yaliyotukomboa sisi. Mhe. Naibu Spika, kuna ubaya gani serikali kufanya jambo kubwa ambalo wananchi wote wakaweza kutambua mapinduzi yao.

Mhe. Naibu Spika, ili niweze kumalizia suala hili la mapinduzi. Tunaona nchi nyingi, wenzetu nchi mbali mbali ambao waliopata uhuru wao kutokana na mapinduzi hata China wanasherehekea uhuru wao. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naipongeza sana serikali kwa kuweza kufanya sherehe kubwa ambazo kwa kweli sasa hivi mpaka vijukuu vyetu vinajua hasa nini maana mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache sasa hivi naomba moja kwa moja niende katika ripoti hii au muhtasari wa ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya maeneo kwenye ripoti hii ninaweza nikayaruka kwa sababu tayari tuna kitabu cha ripoti hii, ambacho ninaomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie kuanzia ukurasa namba moja mpaka ukurasa namba ishirini na tatu. Humu yamo maelezo ya kutosha katika ripoti yetu hii, na ninaamini Waheshimiwa Wajumbe watapata nafasi kubwa ya kuweza kuchangia ripoti hii.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema nitajaribu kuruka baadhi ya maeneo lakini vile vile nitaanza katika utangulizi wa kuwataja Wajumbe wa Kamati ili iendelee kuwepo katika kumbukumbu. Wajumbe wa Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ni:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2.Mhe. Saleh Nassor Juma	-	Makamo Mwenyekiti
3.Mhe. Ali Mzee Ali	-	Mjumbe
4.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	-	Mjumbe
5.Mhe. Subeit Khamis Faki	-	Mjumbe
6.Mhe. Ashura Sharif Ali	-	Mjumbe
7.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Mjumbe
8.Ndg. Rahma Kombo Mgeni	-	Katibu
9.Ndg. Makame Salim Ali	-	Katibu

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 106 (h) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo 2012. Majukumu yake yametajwa katika kifungu cha 114 za Kanuni hizo za Baraza la Wawakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;

b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa Barazani;

c) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika;

d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;

e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka;

f) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika;

g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo; na

h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Mhe. Naibu Spika**,** Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki nane katika mizunguko minne kama ifuatavyo:-

i) Unguja wiki mbili tarehe 13 hadi tarehe 24 Mei 2013.

ii) Dar-es-Salaam wiki mbili kuanzia tarehe 09 hadi tarehe 20 Septemba 2013.

iii) Pemba wiki moja kuanzia tarehe 18 hadi 22 Novemba 2013 na Unguja wiki moja kuanzia tarehe 25 hadi tarehe 29 Novemba 2013.

iv) Unguja kwa muda wa wiki mbili kuanzia tarehe 30 Disemba 2013 hadi tarehe 10 Januari 2014.

Mhe. Naibu Spika**,** katika kipindi cha Mei, 2013 hadi Januari, 2014, Kamati ilitekeleza Majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Baraza, 2012. Majukumu hayo yalitekelezwa kupitia ziara mbalimbali katika Wizara na Taasisi tunazozisimamia, uchambuzi wa Miswada, uchambuzi wa Bajeti, pamoja na Kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara na taasisi husika.

Mhe. Naibu Spika, aidha kamati ilitumia Hadidu rejea zifuatazo katika kufanikisha majukumu yake nazo ni Hansards, ripoti za utekelezaji pamoja na vitabu vya bajeti vya Wizara husika.

Baada ya utangulizi huo, naomba nianze na Wizara ya Nchi (OR), Ikulu na Utawala Bora.

WIZARA YA NCHI (OR), IKULU NA UTAWALA BORA

Mhe. Naibu Spika, kiujumla Kamati yangu inaipongeza Wizara kwa kuweza kutekeleza malengo yake iliyojipangia katika utekelezaji wa Bajeti hasa kwa robo mbili Julai/Disemba 2013 licha ya kuwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti.

Kamati aidha inapongeza kwa dhati kabisa mashirikiano mazuri yanayooneshwa na Wizra hii kwa kipindi chote ambacho Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni za Baraza toleo la 2012.

Kiujumla Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa Wizara wa maagizo ya Kamati ya mwaka wa fedha uliopita.

Suala la Makaazi na Usafiri wa Viongozi hasa kwa Pemba

Kamati inapenda kutoa wito maalum wa kuharakishwa na kushughulikiwa suala la makaazi na usafiri wa Viongozi Wakuu hasa kipindi wanapokuwa Pemba aidha wawili au wote watatu kwa pamoja.

Uzoefu kwa sasa unaonesha kwamba ukimtoa Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, basi viongozi wakuu wa kitaifa wanaobakia inakuwa ni tatizo si kwa makaazi tu bali kwa usafiri pia suala hili kama nilivyosema mwanzo linajirejea tena katika ripoti hii.

Mhe. Naibu Spika**,** Kamati inaendelea kusisitiza kwa mara nyengine tena kuharakishwa kwa ujenzi wa Ofisi ya Rais huko Pemba kutokana na ukosefu wa Ofisi uliopo kwa muda mrefu ambao umekuwa ukisumbua utendaji kazi za Ofisi hiyo.

Suala la Diaspora

Licha ya uhaba wa fedha unaotokana na bajeti finyu wanayopatiwa Idara hii, imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kiwango cha kuridhisha kiasi. Lakini hapa vile vile kuna kitu ninataka niongezee, lakini kamati inashauri kitengo hiki kuekewa bajeti maalum ya kuweza kuwafanya kuweza kuwatembelea hao *Diaspora* katika nchi mbali mbali ili kuweza kuwasaidia taarifa mbali mbali lakini vile vile, kuweza kusaidia nchi yetu.

Kuhusu Utawala Bora

Mhe. Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba dhana nzina ya Utawala Bora inahitaji kutolewa elimu ya kutosha ili iweze kufahamika. Utawala Bora unajumuisha ndani yake Utawala wa sheria, Upigaji vita Rushwa, Uhujumu Uchumi n.k.

Mwisho kwa Wizara hii Mhe. Naibu Spika, tungependa kugusia suala zima la Takwimu. Takwimu sahihi na matumizi ya takwimu hizo ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi yoyote duniani kwani takwimu hizo ndizo zinazoongoza mipango ya kila sekta katika kufikia malengo waliyojipangia.

Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Wizara ya Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora:-

1. Kamati imeridhishwa na hatua zilizofikiwa katika ukarabati wa Ikulu ya Mkoani, lakini pia kamati inataka Ofisi ya Rais kushughulikia kwa haraka suala la ujenzi wa uzio kwa lengo la kuimarisha usalama wa Ikulu hiyo ya Mkoani.

2. Kamati inaridhishwa na inapongeza hatua iliyofikiwa kwa upande wa Unguja kwamba Ikulu zote pamoja na majengo yake yameshapatiwa hatimiliki. Hata hivyo kwa upande wa Pemba bado suala hili halijashughulikiwa ipasavyo, hivyo Kamati inaiagiza Ofisi hii kuwasiliana na Wizara ya Ardhi kuharakisha utoaji wa hatimiliki za majengo hayo.

3. Aidha Kamati imeridhishwa na maendeleo ya matengenezo ya jengo la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Wete Pemba na kuona hatua iliyofikiwa. Hivyo Kamati inatoa wito ya kuongezwa kwa bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili iweze kukamilisha hatua zilizobakia za ujenzi.

4. Kamati pia inaendelea kusisitiza kwa mara nyengine tena kuharakishwa kwa ujenzi wa Ofisi ya Rais huko Pemba kutokana na ukosefu wa Ofisi uliopo kwa muda mrefu ambao umekuwa ukisumbua utendaji kazi wa Ofisi hiyo.

5. Kamati inatoa agizo kwa Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora kumalizana na suala la mjenzi wa *Rest House* ya Micheweni iweze kukamilishwa ambayo imeshadumu kwa muda mrefu.

6. Kamati aidha inaishauri Ofisi ya *CAG* kuanza kufanya *Technical Auditing* hasa kwenye miradi ya barabara, madaraja na majengo ya serikali ili kujiridhisha kutokana na ubora wake. Pia Kamati inashauri Ofisi hii *CAG* ianze kufanya tathmini ya kitaalamu kuweza kujua hasara inayopata Serikali kutokana na tabia ya kucheleweshwa miradi mbali mbali nchini ikiwemo ya barabara na majengo mengine. Mhe. Naibu Spika, hili tumeliona kwa sababu kuna miradi mingi ya serikali ambayo inachukua muda mrefu kukamilika lakini inashindwa kuletewa thamani yake halisi ikiwa aidha tunapata hasara au tunapata faida.

7. Kamati pia inaishauri Serikali kuishirikisha kikamilifu Ofisi ya *CAG* katika mradi wa *e-government* katika ngazi ya kitaalamu ili waweze kujua kinachofanyika na kuweza kufanya kazi kwa urahisi pindi watakapohitaji taarifa zinazowahusu katika mkongo huo.

8. Kuna haja na ulazima wa kushughulikia kesi za udhalilishaji wa watoto ili ile dhana ya Utawala Bora iweze kufanikiwa, na hii zaidi ni katika utolewaji wa haki katika sehemu za Mahakama kwa kesi hizi za udhalilishaji.

9. Kamati inaitaka Idara hii kuwajibika ipasavyo ili uhuru wa kusema katika masuala ya dini na siasa usitumiwe vibaya na kuwadhuru wengine.

Mhe. Naibu Spika, Maagizo ya Kamati kwa Wizara ya Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora.

1. Kamati inatoa agizo la kumalizwa kwa utata juu ya suala la Ikulu ya Micheweni ni la muda, hili ninafikiri itakuwa ninalirejea, kwani ni muda mrefu sasa kumekuwa na kauli ya mazungumza na muhusika. Kamati imeona ni vyema kuchukuliwa hatua za haraka kulimaliza suala hili.

2. Kamati inatoa agizo kwa Wizara husika kushirikiana na wahusika wote ikiwemo watu wa ardhi kuharakisha utoaji wa hatimiliki za majengo haya kwa upande wa Pemba.

3. Pia kamati inaiagiza Ofisi ya Rais kushughulikia suala la kuzuia mmongo'nyoko wa ardhi uliopo katika Ikulu ya Mkoani hasa upande wa nyuma ya jengo ambayo ninafikiri haya yote nimeshayaelezea.

4. Kamati inaiagiza Ofisi ya Rais Ikulu kulisimamia suala la Ikulu ya Mkokotoni na kujengwa fensi.

5. Kamati inaitaka Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora kuandaa mradi ambao utaweza kushughulikia ukarabati pamoja na mmog'onyoko wa ardhi unaosababishwa na maji chumvi uliopo katika eneo la Ikulu ya Bwefumu.

6. Kamati inaagiza kukamilishwa kwa *scheme of service* ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupitia Ofisi ya Rais.

7. Kamati pia inataka kuangaliwa upya sheria iliyompa mamlaka *CAG* ili taarifa zake ziweze kuwa ni sehemu ya ushahidi. Mhe. Naibu Spika, hili tumelieleza kwa sababu CAG anatumia gharama nyingi na nyenzo nyingi kuweza kukusanya taarifa mbali mbali ambazo taarifa zile Mahakamani haziwezi zikatumika kama ushahidi. Kwa hivyo mimi ninafikiri Mhe. Naibu Spika, kamati yangu ndio maana ikajaribu kushauri kuangalia upya sheria zetu.

8. Kamati imeiagiza Ofisi ya Ikulu na Utawala Bora ya Rais kusimamia na kutekeleza suala la ulinzi katika eneo la ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa sababu eneo lile bado lipo wazi sana kuhusu kiulinzi.

9. Kamati inaiomba Serikali kumpatia haki zake Mkurugenzi wa Mamlaka ya Rushwa Zanzibar hii kama sheria inavyoelekeza. Aidha, Kamati inaomba Serikali kumpatia usafiri Mkurugenzi huyu

ili aweze kufanya kazi zake kwa ufanisi hasa kutokana na unyeti wa kazi zake.

10. Kamati imeitaka Ofisi ya Mdhibiti kuwashauri *ZRB* kuachana na tabia ya kukusanya mapato ya serikali kwa njia ya kwenda, kulipa fedha dirishani lakini vile vile watumie njia ya benki ili waweke *slip*.

WIZARA YA NCHI OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu inaipongeza sana Wizara kwa utekelezaji mzuri wa majukumu ya kazi zake pamoja na utekelezaji wa Bajeti katika kipindi hiki licha ya kuwa na changamoto ya ukosefu wa fedha hasa katika Bajeti yake.

Aidha, Kamati inaipongeza Wizara kwa utendaji wake na ushirikiano mzuri iliotoa kwa Kamati katika kipindi chote ambacho Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ilitekeleza majukumu ya kazi zake ilizoagizwa na Baraza.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeridhika na utekelezaji wa Wizara kwa maagizo yaliyotolewa lakini vile vile sambamba na hayo Kamati ilibaini kuna baadhi ya changamoto zinazokabili wizara hiyo na kuitaka Serikali kuzichukulia za haraka hatua, miongoni mwa Changamoto hizo Kamati ilitoa maoni na ushauri ufuatao:-

Suala la ujenzi wa nyumba za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Pemba

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu imeona kuwa kuna tatizo la ukosefu wa nyumba za kufikia Viongozi Wakuu wa Kitaifa wanapofika Pemba wakiwa katika ziara zao hasa Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais. Kamati inaikumbusha serikali kuu kuliangalia suala la ujenzi wa nyumba za Viongozi hao hasa kule Pemba, kwani Kamati hairidhiki kabisa na jinsi wanavyoshughulikiwa hasa kimakaazi wanapokuwa kisiwani Pemba.

Kuongezeka kwa malalamiko na migogoro mingi ya ardhi

Mhe. Naibu Spika, Kamati imeona kuwa kuna tatizo la kuwepo kwa malalamiko na migogoro mingi ya ardhi, jambo ambalo limepelekea kuongezeka kwa malalamiko mengi sana na migogoro ya ardhi katika Idara husika ya Ardhi pamoja na Mahkama ya Ardhi. Kamati imeona kuwa sasa

kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali kuliangalia vizuri sana suala hili na kulichukulia hatua ipasavyo kwa wale wanaolalamikiwa katika migogoro hiyo. Tunafahamu kwamba Ripoti ya Kamati Teule kuhusiana na Migogoro ya ardhi bado inafanyiwa kazi. Ripoti hii tulipoandika bado repoti ya serikali ilikuwa haijawasilishwa, kwa hivyo hii tunayoisema tunaunganisha vile vile kwamba tunaiomba sana serikali waiangalie sana ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi ya migogoro ya ardhi na kuweza kuifanyia kazi kama ilivyoeleza kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Lakini vile vile, kama tulivyoeleza katika ripoti ile Mhe. Naibu Spika, kwamba hata yale ambayo hayakuwemo katika ripoti kwa sababu migogoro ya ardhi ipo mingi, tunaomba sana serikali kuweza kuyafanyia kwa haraka ili kurejesha imani au kuwapa imani wananchi wetu kuona serikali yao inawatumikia.

Mhe. Naibu Spika, kamati aidha inapenda kujua suala la Mahakama ya Ardhi kuhamishwa kutoka Wizara ya Ardhi imefikia wapi. Hii ni kwa sababu suala hili tuliwahi kulishauri hicho kipindi cha nyuma kwamba migogoro ya ardhi mingi inatokana na watendaji wa ardhi kuwa Mahakama ya Ardhi kuendelea kuwepo katika Wizara ya Ardhi, kwa sababu Waziri muhusika anakuwa huyo huyo mmoja. Tulishauri Mahakama ya Ardhi iwe chini ya Mahakama Kuu.

Suala la maafa

Mhe. Naibu Spika**,** Kamati ikiwa pamoja na Wizara husika tulilizungumzia sana suala la maafa ambalo kwa sasa limekuwa na malalamiko mengi sana kwa wananchi. Serikali imekuwa ikionekana kuchelewa sana katika kukabiliana na maafa pindi pale yanapotokea. Sasa umefika muda kwa Serikali kuiwezesha Idara hii ya Maafa kwa kuipatia vifaa vya kisasa ili kuweza kukubiliana na majanga hasa pale yanapotekezea iweze kuwajibika kwa haraka na kwa muda muafaka.

Ingawa Mhe. Naibu Spika, inavyoonekana Idara ya Maafa kazi yao kubwa ni kuratibu pale yanapotokezea maafa, lakini Kamati inashauri kuwa idara hii iwe ni Idara kamili inayojitegemea wenyewe bila ya kutegemea vifaa kutoka kwa taasisi nyengine.

Lakini vile vile kuna baadhi ya vifaa wanavyo wao wenyewe lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna suala la *typing errors*, bado kamati yangu inaishauri serikali kuanzisha ule mfuko wa maafa ambao utaweza kuijenga Idara ya Maafa kuliko ilivyo sasa hivi kutegemea *OC* kupitia katika wizara.

Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali

Kamati inaridhishwa kwa kiasi juu ya Uratibu wa Shughuli za serikali unavyofanywa hivi sasa lakini inaishauri serikali hasa katika suala zima la taarifa au ripoti za Kamati Teule. Kwa kweli ripoti hizi Mhe. Naibu Spika, za Kamati Teule bado serikali kuna maeneo mengi ambayo imeshindwa kuyafanyia kazi na miongoni mwa maeneo hayo, bado serikali inakosa mapato mengi kutokana na baadhi ya maeneo serikali kutokuyafanyia kazi. Kwa hivyo bado nilikuwa ninaomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Naibu Spika, tumeanzisha utaratibu mzuri wa Waziri kukaa na zile kamati ambazo zilizotoa ripoti kuangalia maeneo gani ambayo yana mapungufu. Naomba utaratibu ule uendelee ili kumaliza hizi kero nyengine ambazo zilizozungumzwa katika ripoti za kamati.

Uhifadhi wa Nyaraka za Serikali na Nchi kwa Ujumla

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaridhishwa kwa kiasi jinsi serikali yetu inavyozipa umuhimu nyaraka za nchi yetu. Licha ya hatua hizo lakini bado Kamati inaona hatua muhimu zaidi na za haraka zichukuliwe ili kuhakikisha uhifadhi wa urithi wetu wa nyaraka kwa faida ya sasa na baadae.

Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

1. Kamati inaendelea kushauri juu ya suala la usafiri wa Viongozi Wakuu lazima liekewe bajeti yake maalum na litekelezwe kwa umakini na uangalifu mkubwa kwani makaazi ni stara na si busara kuendelea na utaratibu unaotumika hivi sasa. Hapa imechanganyika Mhe. Naibu Spika, lakini tumekusudia suala la usafiri na makaazi kwa ajili ya vyombo vyetu vya wakuu wa kitaifa kule Pemba.

2. Kamati inashauri Jengo la Baraza la Wawakilishi Pemba lifanyiwe marekebisho makubwa ili vikao vya Baraza vile vile viweze kufanyika kwa upande wa Pemba.

3. Kamati inaishauri serikali kuipatia Idara ya Maafa vifaa vya kutosha idara hii na vya kisasa pindi litakapotokezea tatizo waweze kukabiliana nalo kwa haraka. Kamati pia katika hili inaishauri Serikali kusaidiana na kushirikiana na wawekezaji binafsi mfano katika uwekezaji kwenye

sekta ya anga ambayo kama tulivyosema katika ripoti za nyuyma, kama kuna mwekezaji ambaye yeye ameweza kuleta uwekezaji mpaka ndege ambazo zinazoweza kutua baharini lakini bado serikali wameshindwa kuwapa vibali vya kuweza kufanya shughuli zao.

Maagizo ya Kamati

a. Kamati imelitaka Jeshi la Polisi kutoa agizo kwamba vituo vya Polisi isiwe sehemu ya mahakama bali iwe ni njia tu ya kuelekea mahakamani hasa katika hizi kesi zinazohusu udhalilishaji wanawake na watoto.

b. Kuhusiana na ajali ya boti ya Kilimanjaro II iliyotokea hivi karibuni, kamati inaiomba Serikali kutoa taarifa maalum, sahihi na kamili juu ya ajali hiyo ili kuondoa dhana ambazo zimezagaa mitaani hasa kuhusu utoaji wa taarifa wa ajali ile.

c. Kamati inaitaka Wizara ya Kilimo kufuatilia deni linalodaiwa Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa matrekta ambayo yalikopwa kutoka katika JKT. Suala hili Mhe. Naibu Spika, tulilipata tulipokuwa katika ziara yetu ya kule Tanzania Bara.

Mhe Naibu Spika, Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Mhe. Naibu Spika, kamati kijumla inaridhishwa na utendaji wa wizara hii hasa katika kusimamia masuala ya mazingira katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kamati imesisitiza kuangaliwa suala la upatikanaji wa ofisi ya mazingira, kwani jengo analolitumia hivi sasa, haliridhishi kabisa kutokana na udogo wa jengo hilo pamoja na uhaba wa nafasi ambao ni tatizo kubwa katika utekelezaji wa majukumu yao ya kazi ya kila siku. Kamati aidha, inashauri kufanyiwa marekebisho ya haraka sheria ya mazingira kama alivyoeleza Mhe. Waziri, alipokuwa akijibu taarifa zetu, nafikiri kuna maelezo mazuri tu aliyoyatoa na kamati yangu inayasubiri kwa hamu kubwa.

Mhe. Naibu Spika, kamati pia imebaini udhaifu mkubwa kwa upande wa *ZIPA* katika utekelezaji wa kusimamia sheria ipasavyo, hii ni kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wawekezaji hupewa vibali hata kabla ya kufanyiwa tathmini ya kimazingira, jambo ambalo ni kinyume cha sheria na hivyo kamati inatoa wito tabia hii iwache mara moja kwa maslahi ya nchi na kuwataka waweke mbele

maslahi ya nchi kuliko maslahi ya watu binafsi, kwani janga lolote litakalotokezea katika suala zima la maafa, watakaopata hasara na maafa ni wananchi wa Zanzibar na sio wawekezaji.

Mhe. Naibu Spika, suala hili zaidi tulilizungumzia zaidi kwenye miradi ya wawekezaji, kwenye mahoteli na miradi mingine mikubwa ya wawekezaji ambayo haifanyiwi tathmini ya mazingira. Mhe. Naibu Spika, uharibifu wa mazingira bado unaendelea na ni jambo ambalo linasikitisha, kuona mpaka leo kuna taasisi za serikali zinashiriki moja kwa moja katika uharibifu huo wa mazingira. Miongoni mwa taasisi hizo ikiwemo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, ikisaidiwa kwa karibu zaidi na Halmashauri ambazo zinaonekana ziko mbele zaidi katika kukusanya mapato, lakini sio suala la kufanya juhudi katika uhifadhi wa mazingira.

Kuratibu katika shughuli za madawa ya kulevya. Mhe. Naibu Spika, jitihada za pamoja na za dhati kabisa zinahitajika ili kutokomeza tatizo la madawa ya kulevya hasa katika nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, kamati imebaini ugumu na ukubwa wa kukabiliana na tatizo hili linalotokana zaidi na ukubwa wa mtandao wenyewe. Hivyo, kamati yangu inawashauri kuwe na ushirikiano wa pamoja na kuundwe kikosi maalum kuanzia ngazi ya sheria, ili kuwabaini wale wote wanaohusika na biashara ya matumizi ya madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika, aidha, kamati inaitaka serikali kuchukua juhudi za makusudi na za wazi kama inavyofanya kwa zao la karafuu, ili kuweza kunusuru jamii yetu katika maharibiko haya, hasa katika eneo la madawa ya kulevya. Kamati pia inaitaka jamii kusaidia katika mapambano dhidi ya madawa ya kulevya kwa kuwafichua wahusika wanaoendelea kuharibu vijana ambao ni nguvu kazi ya taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa ingawa hatukuwahi kuiandika katika ripoti hii, lakini ni vizuri kueleza katika ripoti hii kadhia iliyotokea hivi karibuni katika uwanja wa ndege wa Zanzibar, kukamatwa madawa ya kulevya kwa zaidi ya kilo 30, kwa kweli tunaitaka serikali kuhakikisha kwamba wale wahusika wote waweze kukamatwa na wafikishwe katika vyombo vya sheria.

Mhe. Naibu Spika, masuala ya watu wenye ulemavu. Kamati inaipongeza sana Idara ya Watu wenye Ulemavu, hasa kwa kupitia kwa mkurugenzi wake kwa kazi kubwa anayoifanya, hasa katika kuwatambua na kutetea haki za watu wenye ulemavu. Pia, kusaidiana na asasi za kiraia katika kuwapatia huduma pamoja na mafunzo mbali mbali, ili kujiunga pamoja katika kutetea haki zao.

Kamati inashauri kuangaliwa kwa kina suala la ajira hasa kwa watu wenye ulemavu, kwani wapo baadhi yao ambao wana uwezo wa kufanya kazi, lakini bado hawajapewa nafasi zinazostahiki katika suala la kupatiwa ajira. Aidha, kamati inashauri pia kuchukuliwa hatua suala la udhalilishaji la watu wenye ulemavu ambalo bado linazidi kuongezeka siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, suala hili la ajira naomba sana niendelee kulisisitiza hasa kwa watu wenye ulemavu. Kwa sababu tulizungumza katika sera, lakini mpaka sasa hivi bado inabakia katika maandiko, lakini katika utekeleza na kwenye suala zima la serikali inapotoa ajira, bado kipaumbele kwa ajili ya watu wenye ulemavu hakija chukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, suala la maradhi ya Ukimwi na *VVU*. Mhe. Naibu Spika, kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Tume ya Ukimwi, pamoja na *NGOs* zinazoshughulikia masuala ya Ukimwi, kutokana na kazi kubwa wanazofanya za kupambana na kudhibiti maambukizi mapya ya maradhi ya Ukimwi. Pia, elimu wanayoitoa kwa jamii inasaidia sana kujikinga na maambukizi mapya ya maradhi ya Ukimwi.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaishauri serikali kuendelea kutenga fungu kubwa zaidi katika bajeti kwa kila mwaka, ili kuweza kusaidia mapambano ya maambukizi mapya ya Ukimwi dhidi ya magonjwa hatari ya Ukimwi. Hili litafanikiwa tu pale litakapoweza kuendelea na kutolewa elimu kwa wananchi kila itakapobidi. Aidha, kamati pia inaishauri Tume ya Ukimwi kutumia vyema fedha zote zinazotolewa, ikiwa za serikali ama za wahisani kwa madhumuni ya kufikia lengo lililokusudiwa la kuwasaidia watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi, pamoja na kutoa elimu ya umma na sio vyenginevyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa wananchi kamati inapenda kuwatanabahisha na kuwatahadharisha juu ya kuchukua hatua sahihi kila mmoja wetu, kwa kujilinda na kuwalinda wengine ili wasiweze kupata maambukizi mapya. Sote tunafahamu adhari ya maradhi haya ya Ukimwi pamoja na wajibu wa kujilinda na kuwalinda wengine wasiambukizwe. Ni imani ya kamati yangu kwamba yale malengo yaliyokusudiwa kufikiwa 0.3 yataweza kufikiwa kama yalivyokusudiwa ikiwa sote tutashirikiana kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, maoni na ushauri wa kamati katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kamati inaishauri serikali kuendelea kutenga fungu kubwa zaidi katika bajeti ya kila mwaka, ili kuweza kuziba pengo la fedha zinazopungua kila siku za wafadhili na kusaidia mapambano ya maambukizi

mapya ya ugonjwa wa Ukimwi. Suala hili litafanikiwa tu pale itakapoweza kuendelea kutolewa elimu kwa wananchi kila pale inapobidi.

Vile vile, kamati inashauri kuangaliwa kwa kina suala la ajira kwa watu wenye ulemavu, kwani wapo baadhi yao wana uwezo wa kufanya kazi, lakini bado serikali kila inapotoa ajira wanashindwa kuweka kipaumbele kwa watu maalum ambao wanaishi na watu wenye ulemavu.

Tatu, kutokana na umuhimu wa utekeleza wa kazi ya Idara ya Mazingira, ikiwemo suala la ufuatiliaji na uharibifu wa mazingira. Serikali inahitajika kuchukua jitihada za makusudi ili kuipatia Idara ya Mazingira Pemba usafiri wa kutosha na wa uhakika, vyenginevyo uhaba wa usafiri na mafuta unapelekea ongezeko la uharibifu mkubwa wa mazingira katika maeneo yetu.

Maagizo ya kamati katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kamati inamtaka waziri anayeshughulikia masuala ya ardhi, kutoa maelezo ya kina na ufafanuzi ndani ya Baraza juu ya umiliki halali wa eneo linalojengwa, kituo cha kubadilisha tabia huko Tunguu ambalo limekuwa ni kadhia kubwa.

Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia Idara ya Mazingira itahakikisha kwamba miradi yote ya serikali na ya watu binafsi kufanyiwa tathmini ya kimazingira kabla ya kuanza kwake, ikiwemo miradi ya ujenzi wa barabara, hoteli na miradi mingine mikubwa ya ujenzi kwa hapa Zanzibar.

Vile vile, kamati inaitaka Idara ya Mazingira ishirikiane na Bodi ya Viwango ya Zanzibar (*ZBS*), ili bidhaa zinazoingizwa kwenye viwango vya chini, kimatumizi kiafya kwa wananchi. Hasa katika hizi biashara za vifaa chakavu ambavyo vinavyoingia hapa nchini, kwa sababu vingi vinaonekana vikizagaa mitaani ambavyo haviwezi kutumika, lakini vile vile kuangalia na afya zetu.

Mhe. Naibu Spika, nne, sheria ya mazingira iharakishwe na kuletwa Barazani ili mianya yote ya uharibifu wa mazingira iweze kuzibwa. Lakini la tano, ni suala la usafiri kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kule Pemba, kamati inatoa agizo la kutatuliwa suala hilo kwa haraka iwezekanavyo, ili kuwafanya watendaji wetu waweze kufanyakazi kwa ufanisi mkubwa.

Sita, kamati imeagiza kuwepo kwa utaratibu maalum wa kushughulikia bidhaa chakavu na zinazoingizwa hapa nchini, ikiwa ni pamoja na kuzingatiwa ubora na ikitokea kuviangamiza, basi wataalamu husika washirikishwe ipasavyo. Vile vile, kamati inatoa agizo kwa *ZIPA* kuacha tabia ya kuweka mbele maslahi binafsi, bali waweke maslahi ya nchi

kwanza. Kuwajibika katika kutekeleza na kusimamia sheria ipasavyo, hii inatokana na ukweli kwamba baadhi ya wawekezaji hupewa vibali kabla ya kufanyiwa tathmini ya mazingira, jambo ambalo ni kinyume cha sheria hiyo ya uwekezaji.

Mhe. Naibu Spika, nane, kamati yangu inaagiza kufanya utafiti utakaojumuisha wataalamu wa serikali, kukaa na kuangalia kitaalamu zaidi juu ya matumizi sahihi ya eneo la Kisauni ambalo lilikuwa likichimbwa kifusi kwa faida ya nchi na watu wake. Aidha, kamati inaagiza Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, ishirikiane kikamilifu na Idara ya Mazingira katika shughuli zao kwa maslahi ya umma.

Hitimisho

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla kamati imeweza kufanikisha majukumu yake kwa kufuatilia utekelezaji wa kati katika taasisi kama ilivyoainishwa katika ripoti hii kwa ufanisi mkubwa. Kamati pia, inashukuru jitihada zilizochukuliwa na taasisi hizo katika utekelezaji wa kazi zao, ambapo kamati imeweza kutoa maelekezo, ushauri na maagizo ambayo inaamini yataweza kusaidia kutekeleza majukumu yao ya serikali kwa ufanisi kwa kupitia Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Pia, kamati inatoa shukrani za dhati kwa wale wote waliofanikisha kazi za kamati kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Vile vile, kuwezesha taarifa ya kamati kutayarishwa na kuasilishwa kunakohusika. Kamati inamshukuru kwa dhati Mhe. Spika, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wote, pamoja na makatibu wetu wa kamati na watendaji wote wa Baraza waliofanikisha kazi yetu hii ya kamati.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumalizia, nataka niongezee maneno kidogo ili niwaachie wajumbe waweze kuchangia ripoti hii. Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka niwaombe sana watendaji wetu wote wa serikali. Kamati zetu safari hii zimebadilika sana na tumebadilisha sana ratiba kutokana na ratiba tuliyokuwanayo mbele katika Bunge la Katiba. Kwa hivyo, hata ripoti hii Mhe. Naibu Spika, tulipokuwa tunaiandaa, bado kuna fedha nyingi ambazo tulitegemea zilikuwa ziingizwe katika wizara zilikuwa bado, kutokana na muda tumekwenda haraka kuliko vile ilivyotarajiwa.

Kwa hivyo, nawaomba sana watendaji wa serikali, kwa sababu tutakujakuwa na kikao cha bajeti baada ya kurudi katika Bunge la Katiba. Kwa hivyo, yale mengi ambayo tuliokwenda katika wizara na tukaambiwa fedha zilikuwa hazijaingizwa, basi tunaomba pale tu fedha zitakapoingizwa waweze

kuyatekeleza kwa ufanisi mkubwa ili tuje kuona utekelezaji wake pale tutakapokuja kwenye kuandaa hotuba yetu ya bajeti.

Mhe. Naibu Spika, nazungumza hili ili isije ikawa mwanya, kwamba tayari kamati imeshapita tena kwa kuwa hawatokuja tena wakajakuona kwamba hili suala litakuwa limemaliza. Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba sana wajumbe wa kamati, hizi ndio ripoti za kamati na ripoti hizi za kamati tukiweza kuzichangia vizuri na kuishauri vizuri serikali, basi itaweza kupunguza makali mengi hasa wakati wa bajeti. Kwa sababu hapa ndipo tunapoishauri wizara, kwa sababu kamati zetu ndio ambazo zilikwenda katika idara mbali mbali za serikali kwenda kuangalia utendaji wa shughuli za serikali.

Kwa hivyo, naomba sana. Waheshimiwa Wajumbe tunajua tuna shughuli nyingi, shughuli zetu hizo zote tukishakuwa hatukurudi majimboni, basi watu wataanza kupapatua warudi tena majimboni. Kwa hivyo, kwa vile sisi tumepata bahati ya wananchi kututuma hapa Barazani, basi hizo shughuli nyingi naomba tuzipunguze ili tuweze kuchangia kikamilifu, kwa sababu humu muna kero mbali mbali za wananchi pamoja na bajeti yetu na muna mambo mbali mbali ya kuweza kuwahudumia wananchi. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana waheshimiwa tuchangie ripoti hizi, tuwashauri vizuri mawaziri wetu, ili kuweza kuwasaidia kwenda kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache napenda kuwashukuru sana kwa kuweza kunisikiliza, ahsanteni sana. Naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza hapa nimeona maajabu sana, ulipotaja jina langu, bila mimi kuwasha *switch* ya taa, basi yenyewe imewaka, hilo jambo nimeona faraja sana Mhe. Naibu Spika. Ni maajabu makubwa sijapata kuona. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa leo hapa tunaanza kujadili hii, kamati yako ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, wakiwemo Rais mwenyewe, Makamu wa Pili, Makamu wa Kwanza. Lakini namuona waziri mmoja tu, kumbe yuko na mwengine huko nyuma nilikuwa sijamuona. Mhe. Naibu Spika, basi sitaki kupiga dongo, kwa sababu kumbe na waziri mwengine ameji-*act* huko nyuma *backbenchers*. Lakini moja ya ishara, labda anataka kunirithisha mimi kiti chake Dk. Mwinyihaji.

Mhe. Naibu Spika, kuna jambo ambalo nimeliona na hapa ndipo pahala pake niweze kulisema, kwa sababu hapa ndipo panapotoka uteuzi wa mawaziri au uundwaji wa wizara. Suala hili Mhe. Naibu Spika, nimeona nitowe kilio changu hapa kwa kumsaidia Mhe. Rais wangu mpenzi.

Mhe. Naibu Spika, wajibu wetu sisi viongozi wa Baraza hili ni kutoa ushauri kwa viongozi wetu. *Inshaallah* naomba sana Mhe. Naibu Spika, nitautoa ushauri huu kama nilivyoutoa ushauri uliopita hata vikosi vikapata waziri wake na hili naomba nilitowe kwa manufaa ya umma na yeye utekelezaji uzidi kuwa mzuri na kero hili litaondoka Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii ya ardhi ni kubwa sana ni mzigo mkubwa sana, tusipoigawa katikati Mhe. Rais akaliona hilo, basi suala hili litakuwa ni mzigo mzito tutagombana kila siku. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Rais, unisikilize kijana wako, ni mtu mmoja ambaye *Alhamdulillah Rabilaalamina*, watu wengine tukisema basi midomo yetu Mwenyezi Mungu anaitakabalia katika mambo ya kheir na sisi, sisi ni Masharifu wa Mchangani.

Mhe. Naibu Spika, sio vijana wala sio dhambi kusema wizara hii ikawa na mgawanyiko ikawa Wizara ya Nishati na iwe pamoja na masuala ya *ZECO*, maji na mambo mengine. Lakini wizara hii kwa upande mwengine tukisema wizara ya makaazi na shirika la majumba, basi haitokuwa dhambi. Mimi naomba sana kwamba ardhi makaazi inaingia hata shirika la nyumba litaingia hapa.

Namuomba sana Mheshimiwa hili anisikilize tena. Naomba nirudie tena kuwa wizara hii tukizigawa mbili kama wenzetu Tanzania Bara wanavyofanya, sio dhambi na sisi tukaiga kule ili tuweze na sisi kuipunguzia mzigo. Maana yake leo tukikusanya utakuta wizara hiyo makaazi, ardhi, nyumba, maji *ZECO* na mengineyo. Kwa kweli tutamchanganya sana Mhe. Waziri.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Naibu Spika, sio vibaya Mhe. Rais wa Zanzibar, akaona hebu nimwite Makame Mshimba awe waziri, labda zaidi naweza kumpa mawazo mazuri huko tukikutana Ikulu wakati anakwenda kunywa chai nikaweza kumfahamisha suala hili. Naomba sana alifikirie suala hili ili kuweza kulitekeleza.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye sheria. Mhe. Haji Omar Kheir, jana alivyosoma ripoti yake hii, aligusia masuala ya utekelezaji wa ardhi ambayo ni migogoro. Mhe. Makamu wa Pili, ningeomba sana kuna sheria ambazo anazikosa na ndio maana ikawa kauli yake haitekelezwi vizuri. Tutamtilia misongamano kila siku ya ardhi, nafikiri hatimaye haitokuwa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, migogoro ya ardhi hapa, juzi tu katuletea Mhe. Mwenyekiti wa Kamati Teule, ripoti safi tena mwanana kabisa. Kwa sababu huwezi kusema kitu kama hujawa na historia ya kitu. Hata kama ukitaka

kunukuu kesi, basi weka kumbukumbu ya kesi za Uingereza. Unanukuu kifungu cha kule, unasema kwamba kifungu namba fulani kesi ile mtu fulani aliingia hatiani kwa misingi moja, mbili na tatu, si ndio Uingereza ndio mama wa sheria. Sasa na yeye Mwenyekiti wetu wa Kamati Teule alinukuu mambo ya historia ya nyumba tulikotoka, ni jinsi gani ardhi ilipokuwa mali, jinsi gani viongozi wetu waliopita walitoa maagizo kwa kupitia kwa viongozi wao.

Mhe. Naibu Spika, sijui leo huko juu makatibu wapo na mara nyingi sana inakuwa makatibu hatuwaoni ambapo wao ndio watekelezaji wakubwa. Ingekuwa leo ni siku ya kupitisha vifungu, basi mimi ningezuwia fungu, ningesema sipitishi fungu kama sijawaona makatibu huko juu. Kama wapo hebu naomba niwaone siwaoni. Kama wapo wanyooshe mikono, sogeeni mbele sasa tuwaone vizuri, ili tuweze kutoa malalamiko yetu yaliyokuwa mazuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, ameingia ambaye tayari ni mtaalamu wa sheria, lakini kutokana na hali halisi ilivyo bado hatujamtendea haki Mhe. Waziri wetu Makamu wa Pili, anapotoa taratibu za kusema kuwa jamani hee! tatizo hili lifuatiliwe na liishe. Ni sawa sawa na kamati kutoa agizo hatimaye lile suala linakuwa mpaka leo halifanyiwi kazi mpaka tunarudia kamati kila siku. Mhe. Naibu Spika, suala hili kwa kweli haliridhishi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwanasheria ,kama yupo tumpe meno Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, akitoa agizo kama siku ya kwanza, ya pili na ya tatu halikutekelezwa, basi amsimamishe mtu mara moja. Lakini leo sheria inampinga, sisi tunampa tu sheria ya migogoro ya ardhi, lakini hana uwezo wa kutoa kitu fulani futa kwa mujibu wa sheria, hana uwezo huo, tunamtwika mzigo tu kwa kumpa lawama.

Sasa tutengeneze sheria yetu, tusiogope kutengeneza sheria Mhe. Naibu Spika. Kuna mawaziri wanaogopa sheria sijui kwa sababu gani, hii ni moja ya sifa ya waziri akileta sheria hapa ikapitishwa ambayo inamlinda au inamtetea mwananchi au inasaidia serikali sheria zile, basi wewe utapata sifa nzuri. Ukiondoka katika wizara ukiwa umeweka sifa za sheria ambazo zinaleta maslahi. Lakini tunaogopa, Mhe. Naibu Spika, suala hili la migogoro halishi na halitokwisha kuntu, kwa sababu hatufatilii. Hapa tunasema kwamba pahala fulani kuna matatizo, basi imeishia kwenye *briefcase*. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Naibu Spika, nimeona suala hili nilisema ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nilisema kwamba tumeunga kitengo cha Mdhibiti ambaye anafanyakazi yake vizuri sana, niseme ukweli ulivyo vya kuonesha ni jinsi gani ubadhirifu unafanyika. Lakini mwisho wake zinaishia katika *briefcase*, kwa sababu hana meno ya kuendeleza tena huko mbele, jamani sheria tumtengenezee sheria ambazo vielelezo vyake vitakubalika ndani ya Mahakama yetu sisi, ambavyo viko *cream* kabisa havitaki hivi wala vile.

Naomba hili suala tusilirudie tena. Mhe. Mwenyekiti, amesema sasa hivi hapa tuwaambieni vizuri tu na tuwasisitizeni ili hili suala lifuatiliwe. Mhe. Mwenyekiti wa kamati ni bure tu, tunasema sana tena kwa utulivu kabisa na mbwembwe tunatia, lakini hatimaye hakuna utekelezaji, ukweli tuuseme, twende na ukweli na uwazi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, katika ukurasa wa 8, hili neno *CCTV*. Hivi sasa tuna hali mbaya katika nchi yetu, tuna mambo ambayo yako chini kwa chini kama ugaidi, mtu anaweza kuingia tu. Nina rafiki yangu mmoja ana ofisi yake nzuri na hivi vitu vimo Mhe.Naibu Spika, ukiingia wewe, basi keshakujua una nini ndani ya mwili wako, seuze serikali. Tutafute vitu kama hivi vya usalama, hali ni ngumu sana. Mtu anakwenda Ikulu pengine akishakubaliwa pale tu, anaonekana ndio basi.

Lakini unatakiwa wewe kabla hujatia nia kwenda Ikulu,basi iwe Ikulu iwe imeshakuona, hivi vitu vinakubalika sasa hivi twende na wenzetu wanavyokwenda na wakati Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, ni sawa tumeshatoa agizo, lakini naomba hili suala lifuatiliwe kwa umakini kabisa na maeneo haya ya viongozi wetu yako karibu na wananchi wa kawaida na watu wenyewe hawaishi kugeuka. Naomba suala hili liweze kufuatiliwa kwa makini kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kuchangia. Tumesema tuna kitengo cha rushwa, lakini nilipokwenda pale nilijaribu kuzungumzia sana suala la sheria na yeye ndio vile vile ana tatizo la sheria kuwa yeye akishamaliza kumtia hatiani fulani *bin* Fulani, amehusika na ulaji wa rushwa, basi kazi yake imekwisha. Jamani wana sheria. Mhe. Mwanasheria mwenyewe kanisikia akiwa huko nje na sasa anaingia ndani na kajua kuwa mwanafunzi wake anatafuta sheria za kuweka katika utendaji mzuri. Namshukuru sana Mhe. Mwanasheria sio mtu tabu kumbe.

Mhe. Mwanasheria, ukikaa kitako na sheria pia inataka tuifanyie marekebisho, ambapo sheria hizo zitatusaidia kuwapa haki au uwezo kwa hawa watu wetu, Mdhibiti wa Mahesabu au hawa watu wa kitengo cha rushwa. Kwa sababu mara nyingi hawa wakiishia tu wanakwenda kuipeleka

kunakohusika, wao tena wanakuwa wamemaliza *documents* zao, yaani ameiwasilisha kwa Mhe. Naibu Spika, yeye kazi hamna.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba tuwatafutie njia kwa mujibu wa sheria ili na wao *document* yao ikubalike kuwa hii ni sheria, isimamie ushahidi, vyenginevyo vyovyote watakuwa na njia ya kuweza kuifanya au yeye mwenyewe muhusika aende kule kama *DPP* anavyosimamia masuala mengine, ili tuone hiyo njia ya kuweza kufanya hivyo. Wanasheria naomba hili munikubalie, tukichelewa tunapata matatizo.

Mhe. Naibu Spika, tunachelewa sana. Juzi nilisema na hata hapa nitasema tena na sitoona tabu kusema Mhe. Naibu Spika, kwa nia nzuri tu. Hivi sasa tuna wimbi kubwa sana la ujambazi, watu hufanya Zanzibar ni shamba la bibi la kuja kuchukua pesa na wakaondoka, lakini ukiona ni sababu gani zilizofanya ikawa hivi, sheria zetu zimepitwa na wakati. Jamani nisikieni na mimi kilio changu hii ni hatari.

Watu wanakamatwa na silaha, sisi Zanzibar hatuna sheria ya kumfanya mtu amiliki silaha, lakini ni nyepesi sheria hiyo, basi tuliangalie suala hili Mhe. Mwanasheria, wafanyabiashara wetu wanateketea na raia pia wanaogopa sasa hivi Zanzibar. Zanzibar tulikuwa hatuijui bastola, bastola yetu tulikuwa tunaijua ile ya mnazi mmoja ya kwenda kununua, ndio tulikuwa tunaijua ile basi. Lakini leo Mhe. Naibu Spika, vijana wa Kwahani wameokota silaha tena watoto wadogo. Ukimpeleka Mahakamani baada ya muda fulani yule mtu anatoka nje, kwa maana hiyo katafute nyengine uje nayo. Mwenyezi Mungu atusaidie.

Mhe. Mwanasheria na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, Mwenyezi Mungu atusaidie. Jamani mtuokowe kwa mujibu wa sheria ili haki itendeke, naomba sana tena naomba kwa unyenyekevu mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala hili la Micheweni, tumelisema sana na ninaamini na Mhe. Rais, pengine keshachangia kusema. Lakini la kushangaza ikiwa kama kweli na Rais kachangia kulisema suala la Micheweni kuwa limalizike, halafu mpaka leo halijamalizika.

Mhe. Naibu Spika, mambo kama haya iko siku Mwenyezi Mungu akinijaalia nikiwa Rais, nitafanyakazi nzuri, nitawatoa tu watu kazini. Maana yake Mhe. Rais hamtaki kumsikiliza. Sema Rais wetu maskini ya Mungu Mwenyezi, Mungu kamjaalia toka asubuhi ni mpole tu. Lakini iko siku tutapata Rais mjanja kama sisi wakali hapa sio mchezo, siku ya tatu tu namuambia waziri kaa pembeni, weka mwengine twende kazini. Sasa hapa tunashangaa sana.

Mhe. Naibu Spika, kila siku suala hili linasemwa Micheweni kuhusu ile Ikulu. Jamani katika sisi nani ataijua Ikulu ile kama hatotoka humu ndani. Tusifanye masihara, kwa Mwenyezi Mungu hakuna dogo, pengine humu humu ndani miongoni mwetu atakuwa Rais na atakwenda Ikulu kwenda kukaa kule Micheweni, eee! wamo humu wenye ishara hizo za kuwa Rais unawanukia, wamo humu na inawezekana. Kwa Mwenyezi Mungu hakuna dogo, maana yake ndio hilo kubwa lenyewe.

Hakuna kubwa kwa Mwenyezi Mungu, namshukuru sana Mheshimiwa. Sasa mimi kila siku suala hili, mpaka alifika kumfanyia *flustration* ya akili, anaamua jambo lililokuwa halistahiki kwa binaadamu kuliamua. Anagombana na Makatibu Wakuu, tatizo liko wapi, kwa nini tulifanye hili suala. Limekwama wapi?

Mhe. Naibu Spika, sipendi kuomba omba nikaonekana na mimi ni mdhaifu wa kuomba, lakini mtu unakuja unaomba kiuchungu kutaka kuonesha mfano kwa sababu hili suala linawezekana. Mimi ingelikuwa inawezekana ningesema hebu nipewe uwaziri kwa siku moja tu, halafu muone. *I am serious,* si kitu cha mchezo Mheshimiwa kwa nini isiwezekane. Rais keshasema litatueni, limalizeni mimi nangoja nini waziri.

Nenda Wizara ya Fedha kawambie Wizara ya Fedha, kwani mambo mangapi tunafanya ya fedha na fedha zinapatikana. Tukisema jambo hili mwaka huu tulikamie na fedha zinachangwa humu. Tulichanga fedha za meli humu ni fedha nyingi sana, nani asiyejua hapa kwa kuwa tunaitaka.

Mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, kwa kweli suala hili linatia huruma, mnamfanya mkandarasi awe *flustreted,* anakwenda akirudi masikini ya Mungu, hebu limalizeni. Hakai yeye ile Ikulu, imalizeni mpeni haki yaki ili atoke aende zake masikini ya Mungu ili Micheweni na wao iwe imepata Ikulu. Ikulu si mchezo kuipata, watu wengi wanaihangaikia hiyo na hawaipati, lakini wengine wanaipata kwa sababu ina jina kubwa. Si masihara kuingia Ikulu.

Mhe. Spika, naomba sana. Mwenyezi Mungu kalileta jambo kubwa sana la neno kuita Ikulu sio kitu cha masihara. Sijui watu wengine hawa wahusika sijui hawajui nini maana ya Ikulu. Inawezeka pengine hawajui dhana yake na maana yake. Lakini kama mimi ninayejua nini mantiki ya Ikulu, siku moja ukinikaribisha nasema *Alhamdulillahi* kama kuna picha naomba nipigwe mara tatu. Nimeingia Ikulu, nimeingia Ikulu, dogo hilo? Lakini leo tunaizembea hatuitengenezi. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, hili suala lazima liangaliwe kwa mujibu wa taratibu.

Mhe. Naibu Spika, Mwenyekiti wangu wa kamati kila siku analisema hilo. Kuna wawekezaji wengine jamani sheria, sheria, sheria. Lakini kumbe nimemgundua anapiga kelele bure, sheria nyinyi hamtaki kuzifuata. Mtu gani asiyesikia huyo, binaadamu gani. Leo mpaka kituo cha Polisi mtu anamiliki. Agizo hilo tumeshatoa mara ngapi.

Kwanza nimshukuru sana Katibu wa Makamu wa Kwanza, niseme ukweli sitaki kuficha. Mimi sikuzote nakwambieni sitokuwa muongo, sitompenda mtu kwa kuwa ni mtu, nitampenda mtu kwa vituko vyeke na utendaji wake wa kazi. Kuna vituko vya aina nyingi, vituko vya utendaji wa kazi si vituko vyengine, kuwa mtundu, ndio maana ya vituko.

Tumemuelezea sheria zitakazompa Idara ya Mazingira, ameona hilo na yuko mbioni pamoja na Waziri wake kutuletea, wakati wowote tutaletewa kitu hicho. Wakati wowote tutaletewa kitu hicho, wapo mlango wazi. Waziri tunacheza naye na Makatibu wake na Manaibu Katibu wake. Hicho kitu wamekiona na hivi karibuni Mhe. Naibu Spika, imenifurahisha ripoti yao sijapata kuona. Niliwambia kwamba hii ni nzuri sana nilichelewa kuingia, lakini nilipoiona tu ripoti nikasema *yes good*, nilianzia juu nikaishia chini nikasema nzuri, kwa sababu vile vitu vimepangika vile tunavyovitaka siku zote.

Haki yao watu wape, na sasa hivi utekelezaji wake tumemwambia masuala ya dawa za kulevya. Mimi nilimtania kwa suala la vespa moja tu. Kanitajia zaidi ya mambo ambayo yanaofanyika katika vespa zinazobeba unga. Amenambia namba ya asubuhi na jioni inakuwa tofauti. Kama si utekelezaji huo ni kitu gani. Lakini hana sheria zaidi ya hapo. Jamani tufanye *revolution change* ya sheria.

Naomba sana hili suala, tulifanye Mhe. Naibu Spika, ili kuweza kufikisha pahali, tuone sheria zetu zinaweza kutusaidia. Lakini vyengine vyovyote Mheshimiwa tutafika pahali wizara zitakuwa kazi yao bure tu, tumepiga kelele sana kuhudu madawa ya kulevya. Juzi kuna mambo yametendeka hapa na yeye nimpe haki yake Mhe. Haji Omar Kheir (Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ), haki yake nimpe amejitahidi.

Mhe. Spika, lakini waliokuwa ndio hatuwakamati. Nani ana ahadi na Mwenyezi Mungu kwamba katia saini kwamba yeye maisha yote hafi. Sasa unaogopa nini kumtaja mtu, eti utauliwa. Mimi na aniuwe, hakuna tatizo. Eeh! kufa nitakufa tu, hakuna ahadi niliyoweka kwa Mwenyezi Mungu kwamba sifi. Kafa kaka angu juzi maneno unayosema sawa sawa na tumeshamfukia zamani.

Mheshimiwa, inasikitisha watoto sasa hivi wanakwenda na maji, sisi tuwasaidie nini? ajira hakuna kabisa, ajira sinachukuliwa nafasi na watu wa nje. Mahotelini humo mote, hakuna ajira sasa hivi. Hebu tufanye *special* kwa vijana sasa hivi, tuondoe unga, tuwape kazi vijana za kufanya. Kama tutakuwa tunawapa kazi vijana sidhani kama mtu atakumbuka kula unga. Kama tutakamata nyanja vizuri, sidhani kama unga utaingia nchini. Lakini hatuko *serious*, tunazungumza tu hapa, ikisha hapa biashara imekwisha.

Serikali kweli ishindwe kufanya *special day* tukasema sasa leo tufanya operation. Kwa nini mambo mengine tunaweza Mhe. Naibu Spika, litushine hili? Yapo mengi tunaweza na tunadhibiti, *Alhamdulillah.* Mfano mdogo mimi napeleka kwenye karafuu. karafuu ivushe uone, masihara nini, huwahi kuvuka nayo wanaume hao wapo, wameshakufata. Lakini hii inashindikana. Tujicheki na sisi viongozi, mimi nina wasi wasi na sisi viongozi, miongoni mwetu tunashiriki hili suala. Sioni tabu kusema hilo. Mbona hampigi makofi kwa kuwa kweli hili suala linafanyika. (*Makofi*)

Mnapiga makofi mpaka nikushtuweni. Inawezekana yes kwa nini tuogope kusema kweli. Nilivyosema mwanzo kuwa miongoni mwetu, viongozi tunashiriki suala hili, watu jii mmenyamaza. Nilivyokwambieni mbona hampigi makofi, mnapiga makofi. Ndio maana likawa gumu Mhe. Naibu Spika, kama si mimi huyu, kama si huyu, huyu. Tunampa kazi bure Mhe. Makamu wa Kwanza, atafanya nini. Viongozi ni lazima tunashiriki, lazima, nitieni ndani miye sasa. Lazima tuseme. Tunawaua watoto wetu kwa makusudi.

Mhe. Naibu Spika, yale pale mabegi juzi yamekamatwa eti hajulikani mwenyewe nani. Wamekwenda kukamatwa masikini za Mungu waliokaa pale mjengoni wamekwenda kuchukuliwa. Mheshimiwa nataka kulia, machozi yananitoka kidogo kidogo, lakini wewe huyaoni. Uchungu, anakamatwa mzalendo ambaye siye, anakwenda kutiwa ndani Waliyokuwa ndio wanakwenda kuachwa. Basi jamani na hawa waachieni msiwatie ndani, kama hawa mnataka kuwanusuru, waachieni na wao. Ndio siku zote nikakwambieni kuwa msiwaonee wanyonge.

Ndio maana mimi sheria nyengine zinazombana mnyonge mimi nakataa kuziunga mkono na nyie wenyewe mnaona ushahidi hapa. Masikini za Mungu hawajui, yeye anaona mzigo umetiwa *tag*, mzigo umekwenda kwa mujibu wa utaratibu, eti leo mwenyewe hajulikani. Ah! kigogo lazimo kimo hapo. Eh! Mwenyezi Mungu, Uraisi, hetu nipe kazi hii uwone jua kama litatuwa. (*Makofi*).

Si masihara jamani viongozi wenzangu. Mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, hili suala tutaweka *Sober house* zaidi ya mia na sasa hivi zinajaa tena zinajaa, wanatusaidia sana hawa walioweka *Sober house*. Jamani wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza sasa hivi tuiongezee sheria, tuipe meno, wana jukumu kubwa la kuokoa taifa letu la kesho.

Mhe. Naibu Spika, au tuna wivu, maana yake watu wengine wanaogopa, maana mtu ukimwambia mimi mara hii nataka kwenda jimbo fulani. Unaanza kumtisha kwa kumwambia ukenda fulani atakuuwa, mwanga, kwa kuwa asiingie. Labda na hii tunaogopa. Kwa huyu aliyekula unga tukim-*train* vizuri baadaye atakuwa kiongozi, unaona tabu atachukua madaraka yako. Tusione tabu ndio ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba leo uniachie kama ikiwezekana na wajumbe wote wameridhika, mimi niendelee kuchangia. Ni suala ambalo zito na wanafurahika nao mchango wangu na wanaridhika nao.

Mhe. Naibu Spika, tuingie katika bajeti finyu. Mimi mara hii nataka kwenda na *model* nyengine. Kwa sababu kila siku zikicha napea, kila siku zikicha nina watu ambao ni wazee wananielimisha na mimi nakubali. Mwanzo nilikuwa napata shida sana nikiikamata Wizara ya Afya, mwenyewe Naibu ananitizama. Lakini kumbe namuonea sana huyu Mhe. Naibu wa Wizara ya Afya, kumbe kunakohusika sasa nipambane na Wizara ya Fedha. Nikapambana nao, nikawaombea kwa nia nzuri tu, kwa sababu tayari wanapanga bajeti nzuri Wizarani.

Ndio maana nikasema siku moja, wanapanga vizuri mawizara yote na kusema kwamba mimi mwaka huu nitatumia kiasi kadhaa. Sasa mwambie mapema huyu kama mimi fedha hizi sina, kuliko kumshughulisha na kumuhangaisha. Sasa mpe kile unachoweza kuhakikisha kwamba atakipata 100%, lakini hatimaye haiwezikani, haipatikani humu Mheshimiwa. Mimi nikiambiwa uchumi unakuwa, najiuliza unakuwa vipi, mimi huwa najiuliza. Hapa napata mashaka. Tutawasema bure hawa, makatibu na mawaziri, kumbe tatizo lipo kunakofedha. Tuwe wawazi katika fedha zile.

Ndio maana mimi nikasema kwamba mwaka huu ikiwezekana Mhe. Rais, atukubalie Bajeti Kuu isomwe mwisho sisi tuanza na hizi wizara, tuzianzie. Ingekuwa raha sana, wengine wanaweza wakapewa fedha, lakini wasizikamilishe vile inavyotakiwa. Au mtu anaomba fedha hii nifanyie jambo fulani anakuja kugeuka anafanya kwa jambo jengine, tutajua hapo.

Mhe. Spika, niwashukuru sana Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa kweli wamesimamia vizuri sana sherehe zetu na mambo mengine walijaribu

kutafuta wao wenyewe ubunifu wa kutuletea hizi ndubwana kama Mhe. Wanu Hafidh Ameir, alivyokivaa hichi kibeji, lakini kwa bahati mbaya nimekikosa cha miaka 50 kutimia, wametuletea kanga, kwa kweli wamesimamia vizuri sana. Nimpe ushujaa huo Katibu wangu na Waziri wake kwa usiku na mchana kutokulala. Maana katibu wangu nilikuwa nampigia simu sana alikuwa haiyoni kwa sababu ya uchovu wa kazi, si mchezo.

Kwa sababu kahangaika sana, kama kungekuwa kuna uwezekano Mhe. Rais, ningemuomba sana awapatie Shahada maalum ya utambulisho kutokana na kazi zao walivyofanya vizuri kwa kuweza kukamilisha suala hili. Hili nawapongeza sana. Kama si hivyo, basi angalau wapewe mapumziko waende japo nchi moja nje wakapumzike na mjumbe wao wa kamati, japo mmoja anichukue twende tukaangalie hali halisi iliyokuwepo huko.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika masuala ya uzamaji boti. Nilisema kwamba tuwe na vitendea kazi zinavyokwenda na wakati. Hili nalo linasikitisha sana. Kwa kuwa sasa hivi tayari Tume imeundwa ya kutueleza ukweli wa ajali iliyopita ya meli ya mfanyabiashara Bakharesa, tunaingojea. Lakini haya majanga, Mheshimiwa Idara hii tulisema iwe *stand by* kwa vitu ambavyo vinavyokwenda na wakati.

Lakini Mheshimiwa, tutasema mpaka lini, hali halisi zinazotokezea na kila leo tunasafiri Mhe. Naibu Spika. Mwenyezi Mungu atunusuru lisitokezee tena suala hili. Hata uje na meli gani mpya wakati Mwenyezi Mungu akiandika itakwenda tu. Lakini ukiwa na vitu vitakavyookoa utawahi kuokoa katika watu 10 utapata angalau watu saba au sita, lakini umefika *in time* katika tukio.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba wafanyabiashara wa nje na wa ndani wasione tabu kuisaidi serikali katika vifaa kama hivyo. Madhali wana uwezo wa kuleta boti, basi watusaidie na viokoleo ili ikabidhi serikali. Jamani hii ni moja katika raha, wewe ni nchi yako hii, waambie Bakharesa wasaidieni serikali, si vibaya kuisaidia serikali, ndivyo tuvyotaka, serikali ipo wazi kuweza kupokea vitu kama hivyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia. Naomba sana wafanyabiashara wa Zanzibar wa nje na wa ndani kama ilivyoelezwa humu maelezo ya Mheshimiwa Dokta Mwinyi Makame, kawaona na kawathamini sana. Kwa hivyo, naomba sana Mheshimiwa kuwa hili suala wafanyabiashara wa nje na wa ndani wawe karibu na serikali kwa kumsaidia yale mambo yaliyokuwa ni muhimu. Kwa sababu wao ndio wenye vyombo. Isiwe kila siku tunaunda

Tume tu, kuwapeleka Mahakamani, wao wenyewe wanaona tabu mambo hayo, haidhuru ni mambo ya Mwenyezi Mungu, lakini tahadhari lazima nivyema iwepo.

Mhe. Naibu Spika, najali wakati wako, nasema kuwa kama ikiwa niiunge mkono naiyunga mkono ripoti yangu. Naunga mkono na Wizara ambazo zinahusika tulizozitolea maagizo, naomba utekelezaji kama alivyosema Mwenyekiti wangu. Tuwashajihishe Mawaziri, tuwambie kuwa utekelezaji jamani uwe wa aina hii.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jinsi ambavyo ametujaalia uhai, uzima na kuweza kufika hapa tukiwa na furaha kwa ajili ya kujenga nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi wa Wakuu, Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa jinsi alivyofanya kazi kwa muda wote na Kamati yake na leo hii amewasilisha ripoti ambayo kimsingi ni ripoti nzuri na mimi naiyunga mkono kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kiwani.

Mhe. Naibu Spika, yote haya ambayo yameelezwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, kupitia ripoti yao inategemea utendaji wa serikali. Mhe. Hamza Hassan Juma, ametoa ripoti kwa wizara tatu kubwa na ndizo ofisi ambazo zinajenga taaswira ya nchi. Kwa hivyo, ofisi hizi zikienda kombo maana yake hakuna wizara ambayo itafanya vizuri.

Kwa hivyo, nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa kamati hii na wajumbe wake kwa jinsi walivyopekuwa na kuona changamoto ambazo zinaathiri utendaji wa kazi katika ofisi hizi. Changamoto ambazo wamezieleza zikiwemo za fedha na za nguvu kazi. Mimi kwa ujumla Mhe. Naibu Spika, nigusie maeneo machache na baadaye nizungumzie suala zima la nidhamu ya wafanyakazi, ambapo naamini Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kama ni mtendaji Mkuu wa serikali ndiye ambaye anapaswa kusimamia serikali na watendaji wake pamoja na wafanyakazi wote wa serikali hii.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 14, Kamati imeeleza changamoto na maoni yake juu ya ofisi au nyumba ya Mhe. Spika, ambayo hadi hii leo haijahamiwa. Si matumizi mazuri ya fedha za serikali. Nyumba ile imejengwa kwa ajili ya matumizi ya Mhe. Spika. Tunaomba serikali itwambie kikwazo ambacho kimeikumba serikali kwa nini hadi hii leo

nyumba ile haijahamiwa kwa lengo la kumtunza Mhe. Spika, na kutunza usalama wa viongozi wetu.

Sababu ambazo zimeelezwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwamba hakuna maji, hakuna nini, ni sababu ndogo mno. Ukiangalia thamani ya jengo na umuhimu wa ofisi hii, sababu za kukosa kwa maji si sababu za msingi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Naibu Spika, serikali itwambie ni lini serikali itakwenda kukamilisha huduma zile ili nyumba ile Mhe. Spika, aweze kuhamia. Kwanza kufaidisha matumizi mazuri ya fedha za umma, kumuwekea makaazi mazuri Mhe. Spika, na kuweka ustawi wa jamii kwenye familia ya Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyengine ambayo Kamati imeeleza ukurasa wa 14, ni hoja ya tatizo la sauti kwenye ofisi yetu ya Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi. Jambo hili sio la leo, limezungumzwa takriban miaka miwili au mitatu. Naomba sana Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais waanze kujipanga na kulitatua tatizo hili. Juzi hapa meza sita za mbele kulikuwa hakuna mtu anaeweza kuzungumza, kunapokuwa na suala la kuchangia, basi utoke kwenye sehemu yako uende nyuma kwa ajili ya kutoa mchango wako. Jambo ambalo Mhe. Naibu Spika, ni jambo la kutisha.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaendelea mbele hetu tuambie mnapozungumza nidhamu ya serikali tuanze leo hapa, atwambie nani anachukua maagizo ya Makamu wa Pili wa Rais, hivi sasa ndani. Nani amekaimu nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Haya yanayozungumzwa humu nani tunamwambia. Anaambiwa Mwanasheria Mkuu, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Waziri wa Sheria, Mhe. Waziri wa Ofisi ya Rais Ikulu, Mhe. Waziri, asiyekuwa na Kazi Maalumu au Waziri wa Ustawi wa Jamii.

Mhe. Naibu Spika, nchi hujenga kwa nidhamu. Bila ya nidhamu hakuna maendeleo Mhe. Naibu Spika. Mimi ninachoomba kwamba Ofisi hizi tatu ni Ofisi ambazo ni muhimu sana, wakifanya jambo ambalo haliendi sambamba, basi ofisi nyengine za chini zitaiga kichogo cha mlezi wao. Nimuombe Mhe. Naibu Spika, kwamba serikali hasa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iendelee kusimamia serikali kwa umakini sana.

Na ndivyo ambavyo nidhamu ya nchi itajengeka ikiwa viongozi wetu watasimamia nidhamu ya wafanyakazi. Hoja ya udhaifu ya kujenga uchumi wa nchi, si fedha tu, ni fedha na uwajibikaji. Unaweza ukawa na fedha nyingi, lakini ikiwa uwajibikaji mbovu, usidhani kama fedha itasaidia sana katika kuleta maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba ripoti hii imezungumza madawa ya kulevya na vile vile, Waziri anayeshughulikia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais afanye jitihada atwambie mabegi yale matatu au manne yaliyokamatwa ni ya nani? Mimi siamini kabisa kabisa kwamba yale yameteremka kama uzi wa hariri. Kama yale yameteremka kama nzige, maana linaweza likatanda wingu baada ya mvua ikanyesha ikatoa nzige. Lakini mabegi yale yamekuja mpaka yakafika Zanzibar hakuna anaeyajua kwamba mabegi yale ni ya nani.

Mhe. Naibu Spika, mapambano dhidi ya madawa ya kulevya yatakuwa ni magumu sana, ikiwa hatuko makini katika Viwanja vya Ndege na Idara mbali mbali. Leo ikiwa magegi yale yaliyokuwa yamekuja Zanzibar hatuyajui, sidhani kama serikali itajua meli inayosafirisha madawa ya kulevya baharini.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza ya Rais ifanye jitihada itwambie kwamba mabegi yale ni ya nani? na kama kuna watu waliohusika, basi waweze kutiwa nguvuni ili wananchi wapate taarifa sahihi, nani aliyekusudia kuingiza madawa yale au kutoa madawa yale katika nchi yetu bila ya utaratibu.

Mhe. Naibu Spika, kwa jumla ripoti hii imezungumza mambo mengi ambayo kama yangefanyiwa kazi kwa umakini kwenye Ofisi hizi tatu, nadhani serikali ingekuwa na uwezo mkubwa wa kufanya kazi za uwajibikaji. Nimesema kwamba nizungumzie nidhamu ya serikali na nianze Mhe. Spika, kwenye tabia iliyojengeka.

Mhe. Naibu Spika, mara kadhaa Baraza la Wawakilishi limekuwa likipata malalamiko kwamba Wawakilishi wako wamekuwa wakivunjiwa nidhamu sana. Mwaka jana tumesikia Mhe. Subeit Khamis Faki, amezungumza hadharani kwamba aliwahi kupigwa na kutukanwa bandarini. Mimi nilidhani kwamba serikali ingechukua hatua. Lakini hadi hii leo sina hakika kwamba serikali imechukua hatua.

Tuliwahi kusikia Mhe. Asha Bakari Makame, hapa amesema hadharani kwamba aliwahi kuteremshwa mtandio, sina hakika kama serikali imechukua hatua. Tuliwahi kusikia Mhe. Hamad Masoud Hamad, yeye mwenzetu alikuwa Waziri wa Miundombinu aliwahi kusema, sijui kama serikali ilichukua hatua.

Lakini mwezi Novemba humu ndani mimi binafsi nilitumia haki yangu ya kuuliza swali la msingi Wizara ya Afya, lakini majibu niliyopewa hadharani Mhe. Naibu Spika, wewe siku hiyo ndiye uliyekuwa kunaongoza kiti, sijui

kama serikali ilichukua hatua. Serikali hujengwa kwa nidhamu, ikiwa wawakilishi wanavunjiwa nidhamu hakuna hatua, sidhani kama kuna maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, leo asubuhi nimemsikia sana Mhe. Waziri wa Afya, na sitaki nijibu hoja yoyote. Lakini naomba nitumie kanuni 119 ya kuitaka Kamati ya Maadili ichunguze kadhia iliyomfika Mhe. Jaku Hashim Ayoub jana. Kama kuna udhaifu wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, atiwe hatiani. Na kama kuna watu waliofanya udhaifu wao kwa sababu ya Mheshimiwa, basi wachukuliwe hatuwa. Moja kati ya hatua za msingi ni kufukuzwa kazi, hatuwezi kuona wawakilishi wanatolewa muhanga. Leo Waziri anatwambia Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kafanya usanii. Tuchunguze ni usanii au ni udhalilishaji aliofanyiwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, alikwenda kumkagua Mzee Mussa ni Mwenyekiti wa CCM tawi la Kitogani. Alipata ajali ya gari na Wawakilishi humu ndani mwakilishi ndio *ATM*, mwakilishi ndio Mnazi Mmoja, Mwakilishi ndio daktari, bila ya fedha hakuna huduma. Je, ingelikuwa Mhe. Hija Hassan Hija, kenda kumuangalia mwakilishi au mwenyekiti wa CUF kule Kiwani, yangemfika yepi.

Mhe. Naibu Waziri, aliyozungumza asubuhi lazima yachunguzwe kama Mhe. Haku Hashim Ayoub, basi atiwe hatiani kwa makosa yake. Na kama wafanyakazi waliompiga Mhe. Jaku Hashim Ayoub, wana makosa wafukuzwe kazi haraka iwezekanavyo. Na mimi kwa msaada wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, sikubaliani kabisa kwamba mwandishi wa habari aliyechukua habari zile aliandaliwa.

Muandishi wa habari yule mini nilimuhoji, anasema asubuhi alikwenda hospitali na mke wake ndani ya gari yake kuna chombo cha habari kama *camera*, ndio kazi yake, muandishi wa habari yeye huchukua, ukisinzia humu ndani, watu husinzia wanachukuliwa. Alipoona vumbi akachukua picha, hajapangwa na mtu ....

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, nadhani twende kwenye taarifa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mheshimiwa, nazungumza utendaji wa serikali.

Mhe. Naibu Spika: Hiyo unayoizungumza haikusemwa ndani ya taarifa zote hizi, tumeshaisikia, serikali imesikia. Kwa hivyo, twende kwenye utaratibu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Naendelea Mhe. Naibu Spika, na nakubaliana na uwamuzi wako, lakini nasema natoa msaada kwamba tuangaliwe

Wawakilishi wako wana hali ngumu sana katika kufanya kazi. Mimi naomba nikukabidhi *CD* ya kadhia ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naomba nikukabidhi *CD* hii. Vyenginevyo ikiwa serikali haikuchukua hatua maana yake mnatuponza kwa wananchi, mnatuponza kwa watendaji wa serikali.

Mhe. Subeit Khamis Faki, amenambia pale amemsikia mfanyakazi wa serikali anazungumza hadharani kwamba yeye haja yake Wawakilishi kuwatia adabu. Kwa hivyo, *CD* hiyo ifanyiwe kazi. Vyenginevyo Bajeti ya Wizara ya Afya haina maana kuja Barazani hapa.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba sisi kazi yetu ni kuisaidia serikali,lakini ikiwa Wawakilishi hawa wanasaidia serikali ndio wanakuwa wabaya hatuoni faida yoyote. Ni mimi na wenzangu Kamati ya Ustawi watakuwa mashahidi Wizara ya Afya hii hii ilikuwa na bajeti ya milioni 300 Mnazi Mmoja, kamati yangu ikapandisha bajeti ile mpaka milioni 800. Ni sie sie ambao ni wabaya. Mhe. Naibu Spika, niiombe serikali sana kabisa ichukue hatua za nidhamu na kuwalinda Wawakilishi chini ya kanuni zetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo niliotoa sasa niende kwenye Kamati kwa ufupi niseme kwamba Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina jukumu la kulinda mazingira na hali nzuri na ustawi wa nchi yetu, na kamati imeeleza sehemu mbali mbali kwamba kuendelea kutilia msimamo juu ya uhifadhi wa mazingira, na kwamba jukumu la mazingira liko chini ya ofisi yake na ni lazima Mhe. Naibu Spika, Ofisi hii ijipange kulinda mazingira ya nchi yetu.

Tumekuwa tukishuhudia mara kadhaa kwamba bahari inapanda juu, wakulima wanaathirika. Sasa Ofisi hii licha ya ufinyu wa bajeti walionao lakini nadhani wajipange vizuri ili kukuza uelewa wa wananchi wetu juu ya athari ya mazingira na vile vile kusimamia wale wote wanaoathiri mazingira kwa njia moja ama nyengine. Tumekuwa tukisema mara kadhaa kwamba ujenzi wa hoteli zetu kwa kweli hauzingatii vigezo, na hoteli nyingi zimekuwa zikijengwa mageti ambayo ni kinyume na utaratibu. Kwa hivyo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Naibu Spika, naomba kwa kweli isimamie jambo hili kwa karibu mno sambamba na kuwaweka wananchi kuelewa suala zima la uharibifu wa mazingira.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais Ikulu Ofisi ya Mtakwimu Mkuu na Ofisi ya *CAG* Mhe. Naibu Spika, mimi niwapongeze kwamba wanaendelea kujenga ofisi zao kwa umakini, kuendelea kuongeza nguvu kazi na kuwasaidia wafanyakazi kitaaluma na hata maslahi ya wafanyakazi wao.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya *CAG* kwa kweli imekuwa mstari wa mbele katika kujenga uwezo wafanyakazi wake na kuwajengea hoja juu ya maendeleo ya wafanyakazi wenyewe. Kwa hivyo kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani Mhe. Spika, niwapongeze sana Ofisi ya *CAG* na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu na nimuombe Mhe. Waziri Ofisi ya Rais Ikulu, kwa kweli awe karibu nao sana, aelewe kwamba bila ya Ofisi ya *CAG*, bila ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu basi hakuna maendeleo.

Ninamuomba Mhe. Waziri kwamba asione tabu kuwaangalia kwa karibu na pale panapokuwa na changamoto za kimapato za kifedha basi ni vyema akakaa na Kamati ya Mhe. Hamza wakashauriana kwa ajili ya kuleta ufanisi mzuri kwenye Ofisi hizi. Tukubali kwamba bila ya Ofisi ya *CAG* kujenga uwezo Mhe. Spika, mapato ya nchi hii yataenda ambavyo havielekezi.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nimalizie kwa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwamba Kamati iliagiza Wawakilishi wapewe mafunzo ya Katiba mpya. Wameendelea kutoa mafunzo ya Katiba mpya lakini kwa mtizamo wangu Mhe. Naibu Spika, mafunzo bado hayajatosheleza kwa tunakoelekea. Ningemuomba sana Mhe. Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi ikatafuta wataalamu na nyenzo muhimu kwa kutoa mafunzo ya wazi na ya kina kwa ajili ya Wawakilishi wake ili kuelekea vyema kwenye Bunge la Katiba Dodoma mwezi ujao.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo nikuombe tena kwamba usimamie *CD* yangu niliyokupa ili kupata ukweli wa kadhia ya Mhe. Jaku. Naomba kuunga mkono hoja yangu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru sana kunipa fursa hii kuchangia hotuba hii ya Kazi za Kamati iliyosomwa na Mwenyekiti wetu asubuhi, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, lakini Mhe. Naibu Spika, nakuomba uturuhusu japo machache pamoja na kuwa hayakuzungumzwa ndani ya kamati lakini jicho likiumia basi mwili mzima unaumia, kwa hivyo Mheshimiwa niruhusu kidogo.

Mhe. Naibu Spika, na mimi napenda nianzie alipoanza Mhe. Hija Hassan Hija, kama watendaji wa serikali dhamira yao na makusudio yao ni kwamba wakiwapata Wawakilishi kwa kitu chochote kile kama ni kuwakomoa. Mhe. kipindi kilichopita mimi nilizungumza hapa mkanambia kama nahitaji suluti kumbe nilikuwa sihitaji suluti nilikuwa naeleza vile kama nidhamu na heshima, tukienda kwa wenzetu tunapata heshima ya hali ya juu, lakini tukiwa hapa petu tunakuwa na matatizo, Waheshimiwa tunaonekana kama sisi tukija hapa Baraza la Wawakilishi kuchangia hoja zetu tunaonekana kama tunawakomoa watendaji wa serikali.

Mhe. mimi nilizungumza hapa na nikasema nimefika mahala nikakamatwa tai pamoja na wenzangu watatu 3 na siku nyengine tena nikakamatwa tai Mkoani na hatuwakosi watendaji kwa kusema ukweli, na leo pamesemwa kama ukionesha kitambulisho inakuwa ni msaada wako, si kweli, vitambulisho vyetu havifanya kazi hii ni picha tu. Mhe. Naibu Spika, vitambulisho havijulikani na wala havifanyi kazi. Na ni kweli pahala popote pana nidhamu lakini na pahali popote pale lazima viongozi wanapewa heshima yao ya uongozi. Leo ikiwa Mheshimiwa Mwakilishi tunaona uchoyo kwa wenzetu wa Bunge wanavyofanyiwa, lakini sisi Waheshimiwa tunadhalilishwa Wawakilishi.

Na nilisema hapa nikaonekana nina ubishi, nilikamatwa tai mwenzangu keshapigwa. Na leo baada ya kwishapigwa Jaku ajitayarishe mwengine ajue anataka kupigwa mwengine, msifikiri kwa sababu kapigwa Jaku mkafikiri ndio imeshafika mwisho, kesho atapigwa mwengine. Wazee wa kale wasema "*wa fungo ukiliwa na wa kati kati unakuwa wa fungo"*. Kwa maana hiyo keshapigwa Mhe. Jaku kesho ajitayarishe mwengine anataka kupigwa, kwa sababu sasa hatutukanwi tena sasa tunapigwa.

Kipindi kilichopita tulikaa kitako tukazungumza kama uwanja wa ndege, bandarini na sehemu nyengine tunadhalilishwa zaidi. Leo keshakwenda pigwa mtu hospitali, kesho atakuja kupigwa mtu pengine na watakaopigwa hawa hawa Wawakilishi, kwa sababu hii ni *agenda* ya kuwa Wawakilishi wanakomolewa.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, pahali popote pakiwa hapana nidhamu mambo hayaendi vizuri. Waheshimiwa na sisi tunaomba na sisi tuekewe nidhamu, wenzetu wanaekewa nidhamu na sisi tuekewe nidhamu. Na mimi nasema yote haya ni serikali yenyewe ndio inayotukosesha nidhamu. Kwa sababu serikali ingekuwa inawachukulia hatua watendaji kwa kutudhalilisha basi isingefika kudhalilishwa, lakini pamoja na serikali na sisi wenyewe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunakubali tudhalilishwe.

Kwa sababu hatuna umoja na ushauri. Wenzetu kule Bungeni akiuzuliwa mmoja tu wanakuwa na msimamo mmoja tu, leo hapa sie kapigwa tunaona kapigwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, hapa *wallahi* kesho atapigwa mwengine fimbo, asipokuja na kiraka hapa mtu serikali haishughuliki.

Leo Wawakilishi anapigwa Mwakilishi anafika kwenda kuomba kuingia kumuona mgonjwa, Mwenyekiti wake ni mgonjwa kaenda kuomba kwa ridhaa, kweli kama aliondoa heshima kama alikosea Jaku, kwani vyombo vya sheria havipo? Kwa nini wachukue hatua ya kumpiga. Hivi hakuna sheria inayowekwa ya kuchukuliwa hatua kama kakosa nidhamu? Lakini mtu

anakwenda kupigwa kisha mnamuona Jaku, mnamuona Jaku mnasema ati kapigwa kwa sababu kakosa nidhamu, jamaa zangu tunavyokwenda serikali tunaikosesha nidhamu na tunakwenda sivyo.

Ikiwa Mwakilishi kaenda hospitali kuomba kumuona mgonjwa anapigwa, je mtu binafsi atafanywa nini? Mwakilishi kapigwa je mtu binafsi atafanywa nini? Tunavyokwenda sivyo, mimi nasema tena tunavyokwenda sivyo, na nilizungumza hapa kwa kelele mkasema nataka suluti. Je, suluti mmeziona Waheshimiwa keshagaragarishwa mwenzetu chini, leo askari mlinzi wa pale ndiye ana heshima zaidi kuliko Mwakilishi, na Waziri anakuja kutwambia ati kakosa nidhamu mtu.

Leo ndio mwatuchongea tupigwe hivyo mawaziri na watendaji wenu. Waheshimiwa basi tukishapigwa sisi Wawakilishi na nyinyi Mawaziri mtapigwa. Nimeshamwambia pale Mhe. Said Ali Mbarouk jitayarishe kutaka kupigwa na wewe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Kwa sababu jambo hili alilitolea taarifa Mhe. Waziri anayehusika na masuala ya afya na kuelezea namna ya tukio lilivyotokea, lakini bahati nzuri vile vile Mhe. Mjumbe alipokuwa anachangia ripoti ya Kamati ya kusimamia Ofisi za viongozi Wakuu wa Kitaifa, ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija, amelieleza na ametoa wazo zuri, kwamba jambo hili ni vizuri likapelekwa kwenye Kamati ya Maadili ya Baraza ikachunguza kadhia yenyewe ilivyo, ningeliomba sana Baraza lako tukufu Mhe.

Naibu Spika, kwamba jambo hili sisi serikali hatuna tatizo nalo, kwa sababu zimetoka shutma na Wajumbe wameeleza na bahati nzuri limejitokeza kwenye *channel 10* kwenye vyombo vya habari.

Mimi nadhani tukakiachia Kiti baadae kikasikiliza maoni, lakini kuendeleza kwa sababu hoja iliyopo mbele sio hii inayohusu Kamati ya Ustawi wa Jamii. Hili jambo lishasikika mimi nadhani baadae ukaja ukatoa maelezo kuhusiana na ombi ambalo la msingi lililotolewa na Mhe. Hija. Vyenginevyo tukiendelea hivi Wajumbe kuchangia na kuinyooshea vidole serikali haitakuwa jambo sahihi. Kiutaratibu hili jambo Kiti kimelisikia na sisi kama serikali tumelisikia, tutasikiliza maamuzi ya Kiti yatakavyotuelekeza, sisi kwetu hatuna tatizo. Ningeomba huu mjadala ukafikia hapa.

Mhe. Naibu Spika: Na *CD* tayari tumepewa, kwa hivyo twende kwenye *agenda* yetu baadae tutatoa uamuzi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana, lakini sisi tunajadili Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, hii ni Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa na haya mambo yanayofanyika yamo ndani ya viongozi wakuu kwa maana hiyo ndio tukayazungumza, na Mheshimiwa hata ukiona jambo linazungumzwa sana ujue limewagusa watu na hapa mahala pake sisi pa kulizungumza hili suala.

Katika *agenda* moja ni hiyo kwa sababu hili suala limo hii Ofisi hii muna Baraza la Wawakilishi, kuna na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na kuna Ofisi ya Rais mwenyewe. Kwa hivyo hapa tunapolizungumza ni mahala pale hasa, kwa sababu sisi limegusa Baraza la Wawakilishi, wanaofanyiwa vile ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, na Ofisi hii moja tunayoijadili Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndio yenye Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, tukazungumze wapi baada ya hapa.

Kwa hivyo, Mhe. hapa ni mahala pake hasa na Wajumbe kulizungumza ndipo watakapojua kama watu hili suala limewagusa Wajumbe. Kwa hivyo Mheshimiwa tupe uhuru kwa sababu kanuni zinaturuhusu kuzungumza suala hili. Ni mahala pake hasa hapa kuliko huko kwa Ustawi wa jamii, ustawi wa jamii si mahala pake, mahala pake ni hapa.

Mheshimiwa ninakushukuru sana. Kwa hivyo, ujumbe wangu umefika na hoja imetugusa sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine mimi nataka nilizungumze ambalo tumezungumza katika ripoti zetu za Kamati kuhusu utendaji wa viongozi wakuu kule Pemba. Mhe. Naibu Spika, tumezungumza kama serikali ya kuona kama Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili Pemba hawana gari viongozi, viongozi wetu wanaazimana gari, kwa maana hiyo naomba sana Mheshimiwa hili suala ninanalizungumza hapa, pamoja na kuwa tumeshalizungumza na watendaji, lakini ninalizungumza hapa ili kulipa uzito zaidi kuona kama serikali ifanye jitihada kuondoa tatizo la usafiri kule Pemba kwa viongozi wetu wakuu.

Na pia limezungumzwa suala la nyumba, kwa hivyo naomba hili Mheshimiwa hili suala lichukuliwe uzito.

Suala jenginge ambalo nataka niligusie kidogo ni suala la Ikulu ya kule Micheweni. Mheshimiwa ninafikiri vipindi viwili vya bajeti nilizungumza sana kuhusu suala la Ikulu ya Micheweni, lakini sasa naomba Mhe. Waziri, atakapokuja labda atupe ufafanuzi kuhusu suala la Ikulu ya Micheweni imefikia hatua gani ili twaomba isiwe kama gofu imalizwe. Kwa sababu Rais anapokwenda Micheweni ana sehemu yake ya kujidai kama sehemu

nyengine ambazokuwa akienda anakuwa na Ikulu yake basi na kule Micheweni imalizwe ile Ikulu ya Micheweni isiwe kama gofu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni suala la mazingira. Wenzangu wengi wamelizungumza na nataka nilizungumze. Mheshimiwa ninalolizungumza tunaomba Mheshimiwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, tumembebesha suala hili la mazingira lakini tumsaidie na yeye mzigo. Kwa sababu huu tunaombebesha ni mzigo mkubwa sana hasa ukizingatia wakati huu wa mabadiliko ya tabia nchi. Kama kuna mabadiliko ya tabia nchi na suala la mazingira linakuwa linachangia kama kuna uharibifu wa mazingira.

Kwa hivyo, Mheshimiwa anavyosema tumsaidie mzigo ninazungumzia kama Wizara ya Mawasiliano ni moja inayochafua mazingira kwa nguvu sana.

Kwa hivyo, naomba tumsaidie Mhe. Waziri kutokana na makampuni haya yanayokuja yakijenga barabara, lazima serikali iweke mikakati maalumu ya wale wajenzi wa barabara, pamoja tukiwa na maendeleo lazima tupate na hasara, lakini zile hasara zikishapatikana angalau kidogo turudishe ile hasara yake. Mheshimiwa mule munamochimbwa kifusi tuwabane makampuni yanayokuja kuchimba barabara wakimaliza angalau warudishe kidogo, japo kama hayatakuwa kama yalivyokuwa mwanzo, lakini warudishe kidogo.

Lakini Mheshimiwa ukienda ukitizama mahandaki kama yale yaliyoko Micheweni yanayochimbwa, baadae wakishachimba wale makampuni wakimaliza kujenga barabara wanakwenda zao. Sasa sisi wameshatuachia hali ya uharibifu mkubwa wa mazingira hapana kinachorudi tena. Mheshimiwa naomba sana na hili tuliangalie sana kwa kina kirefu sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika,suala jengine ambalo nilitaka nilizungumze kidogo ni hii suala la mabadiliko ya tabia nchi. Mheshimiwa naomba sana kupitia Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na kuwa elimu imeshatolewa sana kwa wananchi lakini tuendelee kuwapa elimu wananchi wetu ili wajue kutokana na hali ya mabadiliko ya tabia nchi ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa sote ni mashahidi kama sasa hivi hali ya upatikanaji wa mvua zilivyokuwa zikipatikana mwanzo kiasili, zote zimebadilikabadilika. Mvua zinanyesha zile alizozitegemea kama zinyeshe kipindi fulani basi zinakuja mvua kipindi kingine. Kwa hivyo, naomba wananchi wetu wapewe elimu kwa hali ya juu, ili na wao wajue kuhusu hali ya mabadiliko haya ya tabia nchi inayokuja.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati hii sitaki nichangie sana niwanyime wenzangu wale ambao wa kamati nyengine basi tuwape uhuru na wao wachangie zaidi hoja yetu, ili kuona kwa sisi tutatia baraka zetu na hotuba yetu tumesoma basi niliona na mimi niseme mawili matatu. Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia taarifa zilizowasilishwa mbele yetu taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ambayo imeonesha utekelezaji katika Ofisi hizi, lakini pia ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kuhusu Ofisi hii ya Viongozi Wakuu wa Kiserikali.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuipongeza serikali na mawaziri kwa kuweza kutekeleza baadhi ya maagizo yaliyotolewa katika kipindi kilichopita, na tumeona hapa namna ya utekelezaji katika maeneo mbali mbali. Lakini pili nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu pamoja na kamati yake kwa kuweza kufanya shughuli zao katika maeneo mbali mbali ambayo tumeona taarifa mbali mbali kupitia maeneo mbali mbali waliyoyatembelea ikiwemo Unguja, Pemba na Tanzania Bara.

Lakini wametuonesha namna ya Idara hizi na taasisi hizi zinavyokabiliwa na changamoto mbali mbali. Lakini pia Mhe. Naibu Spika, tumeona maoni na ushauri wa kamati wa serikali juu ya taasisi hizo, lakini pia tumeona maagizo ambayo yametolewa na kamati kwa taasisi hizo.

Mhe. Naibu Spika, yote haya ni katika kuona kwamba serikali yetu hii ya Mapinduzi Zanzibar inavyowajibika kwa wananchi na kuona moja kwa moja namna ya uwajibikaji wake. Na kwa kuwa zoezi hili Mhe. Naibu Spika, mwaka huu ni mwaka wake wa pili kuanza, basi tutaona namna ya utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, katika taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais juu ya utekelezaji wa maagizo mbali mbali, ambayo jana Mhe. Kaimu Waziri wa Ofisi hiyo alituelezea juu ya maagizo hayo lakini namna ya serikali ilivyoweza kutekeleza maagizo hayo. Kuna maagizo karibu 39 ambayo serikali iliagizwa na amejaribu kueleza moja baada ya jengine namna ya utekelezwaji wa maagizo hayo. Kwa mara nyengine tena tunapongeza kwa hatua hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi niko kwenye agizo nambari 5 ambalo Kamati iliiagiza serikali juu ya suala la malipo kwa wale waliofiwa na jamaa zao katika ajali ya *MV Spice Islander* na kutaka jitihada zichukuliwe ili kuona

wale wote ambao walistahili kupata malipo yao basi waweze kupatiwa hiyo fidia. Mhe. Waziri hapa ametueleza kwamba wale wote waliostahili kulipwa malipo hayo kwa kuonesha vielelezo sahihi wameshalipwa na hivi sasa hakuna madai yoyote ya watu wenye vielelezo vinavyohusika na ajali hiyo ambao hawakulipwa fedha hizo.

Hiyo ni taarifa nzuri lakini ninachotaka kumwambia Mhe. Wazir, bado wapo watu wana madai yao na bado wanailalamikia serikali na wameshawasilisha barua katika ofisi yako na mimi bahati nzuri niliwahi kupata juzi juzi tu nakala za barua hizo. Nimejaribu kuzitafuta sana jana ili nije nazo nimeshindwa kuzipata, lakini walinileta ambao bado wanalalamika, na barua walizonileta ni malalamiko yao ya awali lakini na barua za ukumbusho juu ya malalamiko yao na juu ya fidia ya watoto wao ambao ni miongoni mwa watoto waliopoteza maisha lakini hadi wananileta barua hizo juzi bado hawajalipwa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kusema kwamba bado serikali inahitaji kuliangalia zaidi jambo hili, nitajaribu kuzitafuta kwa umakini zile barua ili baadae niziwasilishe Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tuone na ikiwezekana nitakwenda na mlalamikaji aeleze yeye mwenyewe, lakini ninachotaka kusema bado malalamiko yanaonekana yapo, na kwa kuwa wamenijia wawili naamini pengine wapo na zaidi ya wawili. Kwa hivyo bado suala hili linahitaji kuendelea kufanyiwa kazi kwa sababu madai inaonekana bado yapo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wa maagizo ni agizo nambari 32 ambalo Mhe. Waziri, amejaribu kujibu nasema amejaribu lakini majibu yake hayakukidhi juu ya suala la muwekezaji wa hoteli ya *Cristal Resort Limited* ambayo muwekezaji huyu amefadhili ujenzi wa Kituo cha Polisi Paje ambapo imeelezwa kwamba anawanyanyasa wananchi wa eneo hilo. Kwa hivyo iko haja ya Jeshi la Polisi kuchukua hatua ya kuikomesha hali hiyo na kuliondoa bango linaloonesha ufadhili ya nyumba hizo.

Sasa Mhe. Waziri amejibu kwamba tayari Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeliagiza Jeshi la Polisi kufuatilia malalamiko ya wananchi wa Paje kuhusiana na muwekezaji wa Hoteli ya *Cristal* ya kuwadhalilisha wananchi wa eneo hilo na kulichukulia hatua ipasavyo. Sasa hapa kulikuwa kunahitaji hiyo hatua, palikuwa hapahitaji maelezo, palikuwa panahitaji hatua ambazo tayari zimeshachukuliwa. Ndio maana nikasema amejitahidi kujibu lakini halijakidhi yale matarajio ya Kamati. Kwa hivyo, tulikuwa tunahitaji sasa hatua zilizochukuliwa juu ya kadhia hiyo katika agizo namba 32.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya maeneo mawili, maeneo mengine mimi kwa upande wangu sina matatizo, ninayo juu ya utekelezaji lakini nimeyaona zaidi maeneo haya mawili katika ripoti ya Mhe. Waziri juu ya utekelezaji wa maagizo, lakini nije kwenye ripoti kamili ya Kamati ambapo Kamati hii inasimamia Ofisi tatu, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora, Ofisi ya Makamu wa Pili na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, hili halipo moja kwa moja lakini ningependa kuitumia nafasi hii nalo kulisema suala la hali ya usalama ya Zanzibar katika kipindi hiki. Kwa kweli hali ya usalama katika nchi yetu inaonekana sio nzuri na sisi tunaliangalia zaidi Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa majukumu haya. Katika kipindi cha hivi karibuni Mhe. Naibu Spika, kumetokea mambo mengi sana, vitendo vingi sana vinafanyika lakini la kusikitisha utakuta vitendo vinafanyika lakini wahusika hawakatwi. Sasa wananchi wameshaanza kuwa na wasiwasi, wameshaanza kuzungumza kwamba inakuwaje kunafanyika matendo mara moja, mbili, tatu, nne, lakini hatusikii habari ya kukamatwa kwa wahusika.

Sasa hivi kumeibuka kikundi cha watu wasiopungua 10 wana silaha, wamekuwa wakivamia katika baadhi ya maeneo wanapora wananchi mali zao, wanachukua fedha zao baadae wanaondoka wala husikii habari yoyote. Hivi Jeshi la Polisi linafanya kazi gani?

Sisi tumekuwa tukisikia taarifa wenzetu Bara katika Mkoa kama wa Dar-es-Salaam ambao una idadi kubwa sana ya watu, lakini unasikia tendo limefanyika asubuhi jioni unapata ripoti. Ndugu Suleiman Kova anatoa taarifa tumewakamata wahusika fulani na fulani katika tendo hili, lakini kwetu yanafanyika matendo mengi lakini husikii taarifa yoyote. Sasa tumekuwa na mashaka ya vyombo vyetu hivi vya Ulinzi na Usalama ambavyo tumeviweka kwa ajili ya kulinda usalama wa wananchi na mali zao, kulikoni? Vimeanza kutupa mashaka kwamba pengine inaweza kuwa ni moja kati ya wahusika wa mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, juzi nataka niliseme hili kwa makusudi, kabla ya sherehe wakati tukielekea kwenye kilele cha sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi, kikundi cha Askari wa Polisi katika jimbo langu walimvamia mama mmoja katika nyumba yake usiku, kwa bahati ameweka televisheni ukumbini vijana wa pale mtaani wanakwenda kuangalia mpira, unajua siku hizi watu wanapenda mipira ya nje sana Manchester na Liverpool, amefungua mlango wengine wako ndani wengine wanaangalia, ghafla Kikosi cha Polisi kikavamia kikapiga marungu, wakavunja TV, wamevunja vitu mbali mbali mle ndani.

Sasa unajiuliza hii ni aina gani ya ulinzi? Hawa wanaokwenda na silaha na kuiba mali za watu hawakamatwi, lakini hawa ambao wamekaa ndani ya majumba yao wanaangalia starehe zao wanavamiwa, kwa kweli inasikitisha sana.

Lakini hata zile hatua zenyewe, kwa sababu yule mama na mumewe walichukua hatua ya kwenda Kituo cha Polisi Mwanakwerekwe kwenda kueleza, kwa bahati kile kikosi cha polisi kilichokwenda pale wanakifahamu ni kweli kimetoka katika Kituo cha Polisi Mwanakwerekwe. Mhe. Naibu Spika, wamekwenda *CID* kuangalia ile hali ilivyotokea na hasara iliyopatikana pale zaidi ya shilingi laki nane vifaa walivyovunja. Sasa kwa nini wanafanya hivyo? Kwa nini polisi wawe wanachukua hatua za aina hiyo kuvunja vunja mali za watu? Lakini hata zile hatua juu ya vitendo vile zinaonekana hazijaweza kuchukuliwa.

Mambo haya Mhe. Naibu Spika, yanafika pahala hata wakati mwengine wanasiasa wetu wanalazimika kujiuzulu kwa matendo kama haya yanayofanywa na wafuasi wao. Juzi tu mawaziri wamejiuzulu, wamewajibika kisiasa kutokana na vitendo hivi vya polisi. Sasa jana na leo yanatokea tena matendo kama haya wanakwenda wanavamia, lakini hata yule Mkuu wa Kituo haonekani kwamba lile jambo ana hatua anazozichukua.

Hili Mhe. Naibu Spika, mimi nimelipururia kidogo, naangalia lakini sitokubaliana na kitendo kile kilichofanyika kwa wananchi wangu wa Jimbo langu la Magomeni, walichofanyiwa na Jeshi la Polisi kutoka Kituo cha Polisi Mwanakwerekwe bado napururia, lakini nalisema leo kwamba ni matendo ambayo yanafanyika, badala ya polisi kushughulikia wale wahalifu wanaokwenda na silaha wanavamia katika majumba ya watu sasa wasiokuwa na hatia.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ofisi yake, wananchi wanafika pahala sasa wanajiuliza uko wapi usalama wao na mali zao na serikali ipo, vyombo vyake vipo, tunashukuru wanalipwa mishahara mizuri sana kwa ajili ya kufanya kazi hii, lakini hakuna yanayofanyika.

Lakini *at the end* hata hizo *patrol* zinazopelekwa ndio hivyo hivyo zinavamia maeneo ya watu wasiokuwa na hatia. Kwa hivyo hili nimesema nilizungumze kwa makusudi tuone jinsi wananchi wetu wanavyokata tamaa na vyombo vyao hivi na hali ya usalama wao na matendo sasa hivi yanayoendelea kukua kila siku.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ripoti hii mwenzangu Mhe. Hija Hassan Hija, ameizungumza hapa katika taasisi hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Baraza la Wawakilishi na suala la *echo* katika chumba hiki. *Echo* Mhe. Naibu Spika, katika ukumbi huu toka tumeanza Baraza jipya hili limezinduliwa humu tuliligundua hili, toka siku ya kwanza ya kuzinduliwa Baraza katika ukumbi huu, lakini imebaki bado ni hadithi tu, kesho kutwa tunamaliza miaka mitano mwaka ujao, mimi naamini kama hakuna hatua zinazochukuliwa za makusudi kuondosha hali hii tutamaliza mwaka huu na Baraza lijalo litakuja na litakuwa linazungumzia hali hii ya *echo.* Kwa nini tunakuwa hivyo?

Mhe. Naibu Spika, suala hili tunatumia nguvu kubwa, mawaziri wanatumia nguvu kubwa kuwasikiliza watu, wakati mwengine unaambiwa hebu rudia, rudia, inakuwa haipendezi. Wakati mwengine ili uipate basi inabidi uinamie hapa kwenye *mike* ili upate kusikiliza vizuri, tunapoteza *energy* kubwa sana katika hali kama hii. Mimi nimuombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ofisi yake sasa ichukue hatua ili kuona kwamba jambo hili linaondoka, si vizuri kila wakati kuwa tunazungumza jambo hilo kwa hilo na hakuna hatua zinazochukuliwa. Miaka mitano ni mingi sana kushughulikia jambo kama hili.

Mhe. Naibu Spika, katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Ofisi ya Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Kwa kweli wamekuwa wakifanya shughuli nzuri, lakini suala hili la madawa ya kulevya ambapo sote tunakubali kwamba ni janga la taifa. Tumekuwa tukishuhudia matukio mbali mbali yanayofanywa na wasafirishaji, watumiaji wa madawa ya kulevya yanayoendelea kufanyika. Ripoti hapa bado inasema miongoni mwa changamoto inazozikabili ni kuendelea kuwepo kwa watumiaji na waingizaji wa madawa ya kulevya nchini.

Mimi Mhe. Naibu Spika, nimuulize Mhe. Waziri au niiulize serikali hivi tumeshindwa kudhibiti hali hii? Maana visiwa vyetu hivi ni vidogo sana, hata idadi yetu ya watu si kubwa kila mmoja anamjua mwenzake sio kama eneo kubwa la kushindikana kudhibiti jambo hili. Kwa sababu hawa watumiaji wa madawa ya kulevya wanajulikana walimo. Mimi leo Mhe. Waziri, ukinambia nikupeleke katika maeneo yanamotumiwa basi nitakupeleka, nitakwambia nyumba hii, nyumba ile, kwa sababu watumiaji wapo na wanakaa nje, wanajipanga barazani kuanzia mwanzo mpaka mwisho, ukipita nje kabisa unawaona, mbona hawaendi kwenye nyumba zote wanakuwa wanavamia kwenye nyumba moja.

Mhe. Naibu Spika, ukienda Kwahani pale, ukienda Miembeni wanakaa foleni pale 10, 15 wamejipanga wamejiinamia katika nyumba moja na ile

nyumba sio kama iko peke yake, imezungukwa na majumba tele kila mmoja anajua pale pana jambo fulani linafanyika.

Sasa inapofika taarifa kwamba bado jambo hili linaendelea kwa kweli inakatisha tama. Kwa sababu moja kati ya changamoto inayoikabili tume hii ni kuendelea kwa uingizwaji na utumiaji wa madawa ya kulevya nchini, hiyo ndio changamoto inayoendelea. Mimi nadhani sasa hili jambo tulikomeshe, vijana wetu kwa kweli wanaathirika vibaya, ambapo tunasema hizi ndio nguvu za taifa wanaathirika vibaya. Na tukiachilia bado kuendelea kuingizwa madawa nchini vijana wetu wataendelea kuathirika, lazima serikali ione umuhimu wa kupambana na jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wamekuwa wana mashaka juu ya viongozi wao kuhusu hili, hilo lazima tuseme ukweli, wana mashaka kwamba biashara hii inadhibitiwa na wakubwa na wana haki ya kusema hivyo na wana haki ya kuwa na mashaka hayo. Kwa sababu kama wakubwa wapo wanachukia madawa ya kulevya kwa nini wanashindwa kupambana nayo. Wenzangu wamesema juu ya mfano wa mabegi yaliyoshikwa Uwanja wa Ndege, madawa mengine tumepata mifano yanayopitishwa katika Viwanja vya Ndege vya Dar-es-Salaam na Kilimanjaro na jinsi watu wanavyohusika.

Mhe. Naibu Spika, nataka nikwambie watu jinsi gani wanavyohisi kwamba wakubwa wanahusika. Hivi karibuni kuna askari moja polisi alikuwa yuko Uwanja wa Ndege hapo wa Zanzibar, alitaka kumpekua mfanyabiashara mmoja ana *briefcase*, akamwambia bwana nina mashaka ndani ya *briefcase* yako nataka nione kilichomo ndani. Yule mfanyabiashara akamuuliza *briefcase* hii? Akamwambia naam, nataka nijiridhishe na kilichomo. Akamwambia *briefcase* hii huwa haipekuliwi hapa, akamwambia mimi nataka kupekuwa kwa sababu nina mashaka sasa unitoe mashaka. Akamwambia basi inaonekana wewe umeshachoka kufanya kazi hapa Uwanja wa Ndege. Aliiweka *briefcase* yake pale akafungua anajua mwenyewe zile nambari zake kwa bahati hamna kitu, mna ma-*document* tu mle, akamwambia haya angalia, akaangalia akamwambia sasa nimeridhika funga *briefcase* yako. Siku ya tatu amehamishwa kutoka Uwanja wa Ndege akapelekwa Kaskazini katika vituo vidogo.

Sasa hii Mhe. Naibu Spika, inaashiria nini? Siku ya tatu kahamishwa, na amri ya kuhamishwa imetoka kwa mkubwa katika Jeshi la Polisi, kamhamisha kutoka hapa kampeleka Kaskazini na yeye alimwambia inaonekana ushachoka kufanya kazi hapa. Sasa yanapotokea mambo kama hayo ndio maana wananchi wanasema kuwa biashara hii ni ya wakubwa. Hivi mtu mdogo anaweza kumhamisha kwa siku mbili askari wa polisi kutoka hapa kumpeleka eneo jengine?

Kwa hivyo, haya mambo lazima tupambane nayo, suala la madawa ya kulevya ni janga, kwa kweli vijana wetu wanaathirika kwa kiasi kikubwa, biashara hii haitufai kama tumeona ndio njia muafaka ya kupata utajiri basi biashara hii haifai kwa wananchi wetu, lazima serikali, wizara ichukue kila juhudi kuhakikisha jambo hili tunapambana nalo.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni juu ya suala la uharibifu wa mazingira. Changamoto hii inaikabili Idara ya Mazingira na nasema kwamba uharibifu wa mazingira bado ni tatizo ndani ya jamii.

Mhe. Naibu Spika, kama ilivyo madawa ya kulevya suala la mazingira ni suala ambalo liko wazi. Sasa hivi tunashukuru kwamba wizara imeweza kuelimisha jamii kupitia vyombo mbali mbali juu ya athari za mazingira, uharibifu wa mazingira ukoje. Kwa hivyo, kila chombo, kila mwananchi anajua kwamba nikifanya hivi maana yake ninaharibu mazingira na athari za mazingira wananchi wengi wanazifahamu, lakini leo inasikitisha kwamba nchi yetu hii ndogo suala la uchafuzi wa mazingira limekuwa kubwa, limekua kiasi hata cha uwezo au ukubwa wa eneo letu, lakini wanaohusika na masuala haya ya mazingira wapo wanaangalia tu, wanakodolea macho, kulikoni?

Tumeshuhudia baadhi ya mahoteli yanajengwa kinyume na taratibu za mazingira, hivi ujenzi ule ndio tuseme hauonekani, wahusika hawauoni. Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Mikoa hawaoni kama ule ni uchafuzi wa mazingira, Halmashauri za Wilaya hazioni kama huyu mtu anakwenda kinyume. Mtu anaambiwa kwamba unapojenga nyumba katika maeneo ya fukwe jengo lako liwe zaidi ya mita 30 kutoka katika ufukwe wa bahari, hivi mita 30 hatuzijui? Lakini mtu anajenga mpaka juu ya fukwe anazungusha ukuta, mpaka chini ya bahari halafu leo tunalalamika kwamba maji yanapanda katika baadhi ya maeneo kama Kisiwapanza, haya yote yanatokana na uchafuzi wa mazingira. Tunachafua mazingira yetu halafu athari inakuja baadae, wakati huo sijui tutakuja kukimbilia wapi, leo visiwa vimekuwa vinaendelea kuliwa.

Sasa hivi Kisiwapanza ukienda kule yale maeneo ambayo wakulima walikuwa wanalima yameshaingia maji ya bahari, sijui baadae watalima wapi. Kama yameingia katika maeneo ya mashamba kesho na keshokutwa yataingia katika maeneo ya makaazi tutakwenda kuhamia wapi. Hili lazima tulione na lazima serikali ichukue hatua. Taasisi hizi ni lazima zishirikiane kuona kwamba uchafuzi wa mazingira huu wa makusudi unakomeshwa.

Kwa sababu uchafuzi wa mazingira Mhe. Naibu Spika, uko wa aina nyingi, upo ambao unasababishwa na wakubwa wetu huko duniani ambao ndio wanaotuletea mambo ya *climate change*, masuala ya viwanda. Hilo hatuna uwezo nalo, hatuwezi kukabiliana nalo kwa sababu wamekuwa wakaidi mno kupunguza masuala haya kwenye viwanda vikubwa, lakini mengine yako ndani ya uwezo wetu. Masuala ya kukata miti ovyo yako ndani ya uwezo wetu.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri, changamoto kama hii kuendelea kuwemo ndani ya vitabu haipendezi, tungependa katika ripoti ijayo basi ioneshe kwamba hali ya uchafuzi wa mazingira kwa visiwa vyetu imepungua kwa kiasi kikubwa, kwetu itakuwa ni faraja tena ni faraja kubwa. Lakini kuendelea kupata *statement* kama hizi za kwamba bado tatizo katika jamii la uchafuzi wa mazingira linaendelea kwa kweli haliashirii maendeleo makubwa katika maeneo haya.

Nimuombe sana Mhe. Waziri, suala la mazingira ni muhimu kwa sababu linagusa uhai wetu, linahitaji kusimamiwa ipasavyo kuona kwamba kila mtu kwa upande wake anadhibiti mazingira. Taasisi za Serikali, Wakuu wa Wilaya wanatakiwa washirikiane naye sana Mhe. Waziri katika eneo hili.

Kwa sababu Waziri na Idara yake ya Mazingira ni moja, lakini katika kila eneo kuna uongozi wa serikali kuanzia kwa Sheha, ndani ya shehia kuna serikali, ndani ya wilaya kuna serikali, ndani ya mkoa kuna serikali, hivi kama tutashirikiana kwa pamoja katika kila eneo jambo hili kweli litashindikana? Mimi naamini haliwezi likashindikana hata kidogo. Suala hili la uchafuzi wa mazingira katika maeneo yetu basi litakuwa ni hadithi.

Kwa hivyo, tujitahidi katika kuona kwamba mambo haya tunapambana nayo kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu na vizazi vyetu. Kwa sababu bado nchi hii na visiwa hivi tunavihitaji, sisi kesho tunaondoka kuna keshokutwa tunaacha watoto na wajukuu zetu na wao wangeona wavikute visiwa viko katika hali nzuri na wao waendelee kuvitumia.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, mimi sina zaidi niiunge mkono ripoti hii, niipongeze serikali kwa utekelezaji wa maagizo ya Kamati mbali mbali yaliyotolewa, na niombe sana kuyasimamia haya ambayo katika ripoti hii yamo maagizo yaliyotolewa na kusikiliza ushauri wa Kamati. Kwa sababu kamati hizi ni muhimu zinafanya kazi kuisaidia serikali, itakapoweza kutekeleza haya maana yake matatizo mengi yataweza kuondoka.

Baada ya maelezo hayo nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono ripoti na namna ya utekelezaji wa ripoti hiyo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) kwa kutujaalia kuwa hai na wazima, na leo tukaweza kuendelea na shughuli zetu katika kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi. Nikushukuru na wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia ripoti hizi za utekelezaji wa ripoti za mwaka uliopita za kamati kutoka katika Ofisi hizi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, lakini pia ripoti ya mwaka huu ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwapongeze wote waliowasilisha ripoti zao kwa ufasaha mkubwa na zenye kufahamika. Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nianze na Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora. Kabla sijaanza kusema ni kwamba muda huu wa dakika kumi hautanitosha kwa hivyo nitatumia kadiri inavyowezekana na baadae *Inshaallah* nitakuja kumalizia jioni kama ulivyokwishatangulia kusema.

Katika Ofisi ya Rais Mhe. Naibu Spika, kuna mambo kadhaa ambayo yametajwa, lakini na mimi nianze kwanza na ile ripoti ya Mhe. Waziri kwa mwaka uliopita.

La kwanza lile agizo nambari moja. Hoja yangu Mhe. Naibu Spika, inalingana na Mhe. Salmin Awadh Salmin alipozungumzia suala la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na agizo linalohusu suala la mwekezaji wa *Cristal*. Kuna agizo linalotaka Jeshi la Polisi lichukue hatua na ofisi inaripoti kwamba hatua zimechukuliwa, lakini bila ya kueleza hizo hatua ni hatua gani, sasa ripoti kama hizi Mhe. Naibu Spika, zinatupa matatizo sana.

Kwa sababu kwa chombo kama hiki tunategemea ripoti ya serikali iwe inajitosheleza, hapa pana vyombo viwili vikubwa sana Mheshimiwa vya mihimili ya dola. Kuna muhimili wa utendaji kwa maana ya serikali na kuna muhimili wa kutunga sheria na kusimamia shughuli za umma ambalo ni Baraza la Wawakilishi. Sasa katika kiwango hiki tungetegemea ripoti za serikali ziwe *comprehensive*.

Mhe. Naibu Spika, katika agizo la kwanza kuhusu Wazanzibari walioko nchi za nje. Hapa panasemwa kuwa, idara imeendelea na mchakato huo kwa kufanya mazungumzo na Jumuiya za Wazanzibari walioko Canada, Marekani na Uingereza.

Maelezo: Wazanzibari waliopo katika maeneo hayo wanaendelea na juhudi za kutafuta wawekezaji na misaada kwa ajili ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, haya maelezo hayana kitu, nadhani kwa chombo kama hiki ingepaswa tuambiwe kwamba hayo mazungumzo yaliyofanyika yamefanyika vipi, kama kulifanyika vikao vingapi, kumepatikana nini, lakini ikiwa namna hii tu maelezo haya hayajitoshelezi Mhe. Naibu Spika.

Lakini la pili ni agizo la pili vile vile, hapa mimi nilikuwa naomba kusaidiwa zaidi.

Agizo la pili linahusu kutafuta jengo ofisi ambayo itakuwa nje ya jengo la Ikulu ili kurahisisha *DIASPORA* kupata fursa ya kuitembelea ofisi yao kiurahisi zaidi. Katika maelezo wamesema kwamba kwa hatua ya awali idara inayoratibu Wazanzibari wanaoishi nje imehamishiwa katika jengo lililokuwa linatumiwa na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (*ZIPA*). Sasa mimi sikulijua lipi, lakini kama Mhe. Waziri kakusudia ile nyumba ambayo zamani ikiitwa Nyumba ya Ndege, kwa maana lile jumba jeupe ambalo liko jirani na Ikulu. Jengo lile tunavyojua sisi lilipewa Kamisheni ya Utumishi wa Umma na wao wenyewe wakalalamika kwamba ofisi haiwatoshi pale.

Hata karibuni pia tukapata taarifa na nilipewa taarifa mimi kwa sababu ni Mwakilishi wa jimbo lile ya hao wakuu wa hivyo vyombo, kwamba lile jengo kwa lugha tuliyozowea kusema limedata, kuwa lina ubovu. Sasa kuna suala la kwamba lina ubovu lakini hapo hapo lile limekabidhiwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambao wenyewe wanalalamika kuwa haliwatoshi, halafu tunasema tutaipeleka na idara hii ya Kuratibu Wazanzibari walioko Nchi za Nje kwa maana ya *DIASPORA.* Nilikuwa naomba maelezo kwamba hivyo kweli patapatikana ufanisi?

Mhe. Naibu Spika, vile vile niulizie kuhusu agizo nambari tano. Kuharakisha upatikanaji wa hatimiliki ya majengo ya Ikulu pamoja na yale ya serikali. Katika maelezo tumeambiwa jengo la Ikulu ya Mnazi Mmoja tayari imeshapatiwa hatimiliki halafu zikatajwa na hatimiliki za majengo mengine ambazo ziko katika hatua za utekelezaji, lakini nilichokiona ni kwamba kwanza haya yaliyoorodheshwa hapa majengo yenyewe yote ni ya Unguja tu, sasa nikajiuliza yale yalioko Pemba, *state lodges* ambazo ziko Pemba je, zile zinazo hatimiliki? Kama hazina kwa nini tumetoa maelezo kwa upande mmoja tu.

Lakini pili niulize Mhe. Naibu Spika, kwamba kwa kipindi hiki tangu ilipotoka ripoti ya mwaka jana mpaka mwaka huu iwe bado hatua za

utekelezaji zinaendelea? Ndio yale Mhe. Salmin Awadh Salmin aliyokuwa ameyazungumza hapa, kwamba mengine mambo madogo madogo yanapochukua muda mrefu sana hayakamilishwi unajiuliza tunahitaji miaka mingapi ili tuweze kukamilisha maagizo na kila siku chombo hiki kinatoa maagizo mapya. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hilo nisaidiwe maelezo.

Halafu Mhe. Naibu Spika, agizo nambari 12 limezungumzwa kutengenezwa kwa barabara iendayo katika jengo la Ikulu la Chake Chake barabara imekamilika. Hiyo hainipi shida, lakini hapa nina swali, hizi *state lodges* au majengo ya serikali haya tunategemea yatumike kwa ajili ya kuhudumia viongozi wetu wanapofika katika maeneo yale kwa sherehe mbali mbali za kiserikali?

Karibuni Mhe. Naibu Spika, sisi Kamati yetu ya Mawasiliano na Ujenzi ilikuweko Pemba kwa shughuli zake na ikawa imesadifu ni kipindi ambacho cha wiki ya mwisho ya sherehe za Mapinduzi. Wakati tuko pale Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tatu, Mhe. Benjamin William Mkapa alikuwa anakuja kwa ajili ya kwenda kufungua skuli ambayo imepewa jina lake.

Lakini pale pale ikatokea hitilafu ya mawasiliano Mhe. Naibu Spika, ilielezwa kwamba akija atafikia hiyo *State Lodge* ya Chake Chake, lakini dakika za mwisho akaja akawekwa pale nilipo mimi *Alhaqiir* Ismail Jussa na *Alhaqiir* mwenzangu Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa tumefikia katika *Hifadhi Hotel* inayomilikiwa na *ZSSF*. Sasa tukaulizana sisi wenyewe kwa wenyewe kwamba haileti picha nzuri. Kwa hivyo, nilikuwa naomba maelezo Mhe. Naibu Spika, kuhusu hilo.

Nikitoka hapo mimi naomba utaratibu wangu iwe nikitoka katika ofisi naingia moja kwa moja katika ripoti ya kamati ya mwaka huu ili nikiacha ofisi iwe nimeacha.
Jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo ningependa kulizungumzia kwenye Ofisi ya Rais na hili nishawahi kusema. Hivi sasa tuko katika mwaka 2014 tayari, mimi naelewa na naheshimu kabisa kwamba mwenye mamlaka kwa mujibu wa Katiba yetu ya Zanzibar kuanzisha ofisi mbali mbali katika serikali na kuziteulia wakuu wake ni Mhe. Rais, lakini niliwahi kusema Mhe. Naibu Spika, kwamba nadhani kwa ukubwa wa serikali ambayo Mhe. Rais alikuwa kaiunda hasa ukilinganisha kuna maeneo mengi ambayo…

Mhe. Naibu Spika, naona unaniangalia.

Mhe. Naibu Spika: Ndio, naona muda umekwisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Basi bora niliache nitakuja kulizungumzia jioni. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa ushirikiano wenu wa tangu asubuhi hadi saa hizi. Kwa hivyo, naakhirisha kikao hadi saa kumi na moja za jioni ili tuje tuendelee na yaliyosalia.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunamalizia kwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu dakika zake 20. Baade tunawakaribisha mawaziri na baadae mwenyewe Mwenyekiti wa kamati aweze kuhitimisha na tuweze kusoma ripoti nyengine.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuendelea pale ambapo nimekuwa nimemalizia kabla ya kuakhirisha kikao cha asubuhi.

Mhe. Naibu Spika, nilianza kwa kuchangia yale ambayo yamo katika ripoti ya Utekelezaji wa maagizo ya mwaka uliopita ambayo yamo katika Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora. Mhe. Naibu Spika, nikasema kabla ya kuingia ripoti nyengine ningekwenda kwanza katika ripoti ya kamati ili nikimalizana na ofisi hii iwe nimemaliza na nimeingia kwenye ofisini nyengine.
Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nilianza kwa kuelekezea kwamba tumeingia mwaka 2014. Tunakaribia sasa kumaliza mwaka wa nne tangu serikali hii iingie madarakani na nikasema naheshimu kwamba mwenye mamlaka ya kuanzisha ofisi na kuwateuwa Wakuu wa Ofisi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni Mhe. Rais. Lakini nikasema kama na sisi ni chombo cha kuishauri serikali tuna wajibu wa kuelekeza au kushauri pale ambapo tunaona haya mapungufu.

Moja Mhe. Naibu Spika, niliokuwa nikilizungumza mara kwa mara ni suala la ukubwa wa serikali. Lakini bado Mhe. Naibu Spika, naamini kwamba kuwa serikali yetu kwa kuwa na wizara 16 na Mawaziri wasiokuwa na wizara maalum 3 na Manaibu Mawaziri kama sikosei 8. Nadhani Mhe. Naibu Spika, hii ni idadi kubwa sana ya viongozi wa kisiasa. Kwa maana ya Mawaziri wa Serikali ya nchi ndogo kama yetu. Kwa hivyo, bado Mhe. Naibu Spika, mimi nitumie bafasi hii kumuomba sana Mhe. Rais kuna haja

ya kutizama tena muundo wa serikali yake ili kupunguza gharama ambazo zinatumika kuendesha serikali hii.

Mhe. Naibu Spika, baadae nitakapochangia Ofisi ya Makamo wa Pili nitazungumzia suala ambalo tumelikuta takribani karibu mawizara yote tuliokwenda la uingizwaji wa fedha kiasi kidogo mno katika bajeti za matumizi ya kawaida, kiasi ambacho kinakwaza utendaji wa serikali yenyewe. Sasa naukubwa wa serikali ikiwa kubwa maana yake hilo linaathiri pakubwa zaidi. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba nichangie hilo.

Jengine, Mhe. Naibu Spika, nilitaka kuzungumzia kidogo juu ya mamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi. Mhe. Naibu Spika, tangu serikali hii ya awamu ya saba kuingia madarakani imeleta sheria nyingi sana, na nyingi zina malengo mazuri, na tumezipitisha. Lakini bado kuna mtihani mkubwa sana katika utekelezaji wa hizo sheria zenyewe.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilitegemea kwa kuanzia kwa mamlaka hii ingelikuwa angalau ripoti za Baraza la Wawakilishi ambazo zilikuwa zikiwasilishwa humu ndani ambazo zimetaja mambo mbali mbali, ambayo yenyewe kwa mujibu wa Sheria ya Haki, Kinga na Fursa za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ripoti zile haziwezi kutumika kama ni ushahidi mahakamani. Lakini kwa sababu zina kesi za kuashiria au tuhuma zinazoashiria masuala ya rushwa na uhujumu uchujumi basi mimi ningetarajia kwamba mamlaka wangepata pa kuanzia.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wengi sana wanalalamika na kuonesha kidole kwa serikali katika mambo mengi ambayo tunaamini kuna rushwa na uhujumu uchumi. Mhe. Naibu Spika, mambo haya yanakuwa yanajadiliwa hapa na yakawa majibu kwa serikali hayatoshelezi yanawapelekea wananchi kuongeza wasi wasi wao. Kwa hivyo, nilikuwa nategemea kwa mamlaka hii basi angalau tuione kwa kuanza kazi kwa kuanzia katika ripoti zile ambazo zimeletwa Baraza la Wawakilishi hapa katika mambo mengi ya kuanzia.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Hapa Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nianze na hii ripoti au taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ambayo ilisomwa hapa na Kaimu Waziri.

Mhe. Naibu Spika, tunasikitika kwamba tunasoma na tunachangia hapa. Lakini Mawaziri wahusika wenyewe hawapo. Na hii inaonyesha dalili za udhaifu katika utendaji wa serikali hasa inapozungumzwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ambayo kazi ni kuratibu utendaji wa shughuli za serikali.

Mhe. Naibu Spika, Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais hayupo anaemkaimia nae hayupo hata sijui nani anachukuwa maagizo haya. Lakini kwa kawaida Mhe. Naibu Spika, ofisi ambayo hapapaswi kukosekana mtu wa kukaimu katika mfumo wowote wa Kibunge ni Ofisi za Uratibu wa shughuli za kiserekali. Hapa hatumuoni mtu Mhe. Naibu Spika, kwa muda huu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hii si picha nzuri kwa utendaji wa serikali.

Lakini katika hilo hilo ukurasa wa 9 wa ripoti iliyosomwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, pamezungumziwa migogoro ya ardhi na limetajwa humu na katika ripoti hii ambayo alikuja akaisoma. Mhe. Kaimu Waziri, pia migogoro ya ardhi imo katika ukurasa wa 16.

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohd Sheni katika ziara zake za kutembelea Mikoa ya Unguja na Pemba amewaagiza viongozi wa Mikoa hiyo wakiwemo Wakuu wa Masheha, Wilaya na Mikoa kulipatia ufumbuzi suala la matatizo ya ardhi katika maeneo yao. Kwani kwa kiasi kikubwa viongozi hao ndio waliosababisha migogoro hiyo.

Mhe. Naibu Spika, tumesema mara nyingi katika Baraza hili kwamba yule anaesababisha tatizo nae mwenyewe ikiwa ni sehemu ya tatizo hawezi akalimaliza tatizo lile. Tukitaka serikali itafute njia ya kushughulikia suala hili. Kikao kilichopita Mhe. Naibu Spika, palikuwa na ripoti hapa ya Kamati Teule inayochunguza migogoro ya ardhi imeonesha uzito na ukubwa wa tatizo hili. Mimi nilitegemea kwa hatua hii tusingepata majibu kama haya kutoka katika serikali. Tulitegemea tupate maelezo mengine na njia ya ufumbuzi isiyokuwa hii ambayo Mhe. Rais kaisema tangu mwaka wa mwanzo alipoingia madarakani 2011 na mpaka leo imeshindwa kuzaa tija yoyote badala yake migogoro ipo pale pale. Kwa hivyo, nategemea nimeigusa Ofisi hii basi Ofisi ya Makamu wa Pili ije itupe jawabu jengine la kuridhisha.

Lakini si hilo tu Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 10 wa ripoti hii ya kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa wamezungumzia Idara ya Maafa. Katika sehemu hiyo Mhe. Naibu Spika, wameelezea jinsi idara hii ambayo imeshindwa kufanya kazi zake kwa sababu haina vifaa, haina utaalamu na hata sheria yake imepitwa na wakati.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka kuungana na kamati na mimi sitaki kwenda kwenye maelezo makubwa kutafuta ushahidi. Ushahidi kwamba idara hii bado haijaweza kujisaidia chochote Zanazibar ni ajali ambayo imetokezea karibuni wakati MV. Kilimonjaro ilipokuwa inasafiri kutoka Pemba kuja

Unguja. Mhe. Naibu Spika, kumeundwa kamati ya kuchungunza sababu lakini labda kutokana na hali yake kamati ile haikupewa uzito kama zile ajali zilizopita.

Mhe. Naibu Spika, kinachonisikitisha mimi ni kwamba moja ya sababu zilizotajwa ni kwamba hali ya hewa ilikuwa mbaya. Sasa mimi najiuliza katika wiki ile Mamlaka ya hali ya hewa ya Tanzania mfululizo ilikuwa ikitoa ripoti za kina juu hali ambayo ilivyochafuka baharini. Upepo mkubwa mpaka ukubwa wa mawimbi ukitajwa, tulikuwa tunapewa taarifa mpaka kwenye simu zetu.

Sasa tunashangaa kunapokuwa kumeshatolewa tahadhari kubwa kama ile vipi Idara ya Maafa isichukuwe hatua za tahadhari kuzuia usafiri katika kipindi kile mbali na mamlaka nyengine. Idara ya Maafa si kazi yake tu ninavyoelewa mimi kukabili tu maafa, lakini pamoja na kukidhi kunapotokezea tayari tahadhari zinapotolewa. Kwa hivyo, ndio nikasema badao Idara hii haijaweza kumsaidia Mzanzibari. Tuna haja sana ya kutizama haya mambo ambayo ilikuwa nayo.

Vyenginevyo Mhe. Naibu Spika, kila siku tutaendelea kuyatolea kafara maisha ya wananchi wetu kwa sababu vyombo vilivyopewa dhamana ya kuwajibika haviwajibiki katika maeneo yake. Kwa hivyo, naomba hili akija huyo mtu ambae sasa hivi simuoni hapa, aje anipe majibu ya kina anaewakilisha Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo naungana na kamati liko ukurasa wa 12 ni kuhusu haja ya kuweka kumbukumbu za viongozi wetu wa kitaifa. Mimi nakubaliana nalo kabisa. Mhe. Naibu Spika. Marekani wana utaratibu mzuri sana kila Rais ambae anamaliza muda wake huwa kuna nyumba ya kumbukumbu ambayo nyaraka zote ambazo zilikuwepo kwenye kipindi chake, zile ambazo zimekwisha muda wake zinawekwa pale, hata nyaraka, na taarifa za mambo mbali mbali ambayo yanamuhusu Rais yule unazipata pale.

Kwetu sisi ni kazi kubwa sana Mhe. Naibu Spika. Mimi karibuni nilishiriki katika kuandaa kitabu ambacho tulikizindua cha miaka 50 ya Mapinduizi, kumbu kumbu za picha. Unasaka picha za baadhi ya viongozi waliotumikia kwa muda wa miaka 10 huzipati! Kwa hivyo, huyo ana muda mrefu katumikia picha zake zina mtihani kuzipata.

Kwa hivyo, nilikuwa nadhani kuna haja kweli ya kuweka nyumba za kumbukumbu za viongozi wa kitaifa kwa Zanzibar ili isijekuwa tabu kuja kupata historia pale itakapohitajika.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Kiwanda cha Upigaji chapa. Hapa Mhe. Naibu Spika, mimi natafautiana na kamati. Kamati kwa mwaka wa pili mfululizo inaandika ripoti kushauri kwamba kiwanda hiki kifanywe kuwa shirika ili kujiendesha chenyewe kiweze kujitegemea.

Kwa sababu dhana ya kuwa na mpiga chapa wa serikali ni dhana ambayo imejengeka katika nchi nyingi hasa za Jumuiya za Madola. Pengine hata zisizokuwa za Jumuiya za Madola. Ni kwamba pale ni pahali ambapo nyaraka zote za serikali zinachapishwa. Leo hakina uwezo hata wa kuchapisha, hivi vitabu vingi vimechapishwa nje lakini vikibeba ruhusa ya mpigaji chapa wa serikali. Mimi nilikuwa nadhani leo ukikigeuza kikiwa shirika kitafanya biashara, ile dhana nzima ya kudhibiti siri za serikali haitopatikana.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, mimi suala la kubinafisisha naunga mkono na kuna haja ya kulipatia vifaa kukijengea utaalamu. Lakini kukifanya shirika nahisi kwamba kitapoteza ile dhana nzima ya kuwa mchapaji rasmi wa Nyaraka za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, haraka haraka niende kwenye Baraza la Wawakilishi ambalo pia linasimamiwa na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Kwa maana ya shughuli zake za kiutawala pale. Hapa Mhe. Naibu Spika, wengine wameshazungumzia mambo mengi sitaki kuzungumzia kadhia inayowakuta Wawakilishi. Kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maadili na nidhamu. Inatakiwa kama Mjumbe tayari keshatoa taarifa hiyo kwako tusubiri tutizame

Lakini mimi nataka kusema kwa jumla kuna haja kutizama tena katika Baraza la Wawakilishi mambo mbali mbali yanayohusu utawala. Moja Mhe. Naibu Spika, naomba tuitizame tena Ofisi ya *Hansard*. Hakuna kazi ngumu kama kazi ya kuweka kumbukumbu za *hansard.* Sisi tunazungumza hapa kuna watu saa zote wanahakikisha kwamba kila neno linalozungumzwa wanalipata vile ambavyo limezungumzwa, ni kazi ngumu sana.

Mhe. Naibu Spika, nadhani wakati umefika kuangalia kwanza posho zao ofisi ya *hansard*. Posho ambalo wanalipwa ni posho dogo sana ukilinganisha na uzito wa kazi zake. Lakini na hata madhara ya kazi ile kwa sababu saa zote inabidi wavae maspika yale katika mashikio yao, kila wakati wako kwenye kompyuta mambo yote haya yana athari zake katika maisha ya biaadamu na afya zao. Nilikuwa nadhani kuna haja ya kuangaliwa.

Lakini si hapo tu Mhe. Naibu Spika, hata utunzaji wa kumbukumbu zenyewe za *hansard*. Mhe. Naibu Spika, mimi nasikitika kwamba nchi yetu baada ya

kwenda mbele tunarudi nyuma. Leo nimekwenda kuyachukuwa makusudi haya, hii ni kumbukumbu ya *hansard* ya Bunge la Ghana, ukiambiwa kuwa hii ni kumbukumbu ya mazungumzo ya watunga sheria wa nchi, unajua kweli hapa pameheshimiwa, ile hadhi yake na namna ya kiwango cha utunzaji wa kumbukumbu za *hansard*.

Lakini Mhe. Naibu Spika, hiki kitabu ni cha karibuni cha mwaka 2009 Ghana. Sisi mwaka 1986 tumeshafikia hadhi hiyo. Hii hapa *(hapa Mjumbe alikuwa anaonesha mfano wa vitabu)* ni kumbukumbu ya majadiliano ya Baraza la Wawakilishi, ukitizama Mhe. Naibu Spika, hiki kinahadhi hasa ya kuitwa kwamba hizi ni kumbukumbu za Chombo cha kutunga Sheria cha nchi. Huu ni mkutano wa nne sehemu ya pili tarehe 4 Juni hadi tarehe 7 Juni 1986.

Lakini Mhe. Naibu Spika, inasikitisha tumetoka hapa tunarudi huku, sasa hii tunapiga hatua au tunaserereka kurudi nyuma. Mhe. Naibu Spika, usije kuona hili gamba ukadhani kwamba ndio ubora umeshuka kwenye gamba tu. Humu ndani hizi karatasi Mhe. Naibu Spika, si za kuchapwa, hizo ni karatasi ambazo zimechapishwa katika kompyuta zetu za kawaida na ku-printiwa zetu za kawaida. Ile kuweka vitabu vya kumbukumbu za *hansard* kama inavyotakiwa haiko katika Baraza la Wawakilishi. Mhe. Naibu Spika, tusiwasimamie wengine tuanze humu ndani.

Kwa hivyo, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hili liko chini yake maana yake bado ule mswada haujaletwa ukapitishwa hapa kwenye Baraza la Wawakilishi. Nadhani kuna haja ya kutizama na kuweka kumbukumbu vizuri za mazungumzo ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, kikao kilichopita hapa nilikuja na *hansard* nikazisoma hapa za mwaka 1931 za Baraza la Kutunga Sheria. Sasa huko tulikotoka zilikuwa zikichapwa vizuri 1931. Mhe. Naibu Spika, leo tuko 2014 tunarudi hali hii wakati mpaka kwenye miaka 80 tumeshafika hapa. Sasa kwa nini mbali ya hayo mengine yaliyokuwa yametajwa hapa kwamba hata tatizo dogo la *echo* tu Mhe. Naibu Spika, mwaka wa 4 tunamaliza bado tumeshindwa kupata ufumbuzi. Tatizo dogo tu tutawapa imani wananchi kweli tutaweza kuyapatia ufumbuzi matatizo yao makubwa kabisa Mhe. Naibu Spika, sidhani.

Mhe. Naibu Spika, muda unasonga haraka haraka nilitaka nizungumzie Bunge la Katiba. Wamelitaja katika ripoti yao Kamati ukurasa wa 14. Mhe. Naibu Spika, awali kabisa wakati wa kukusanya maoni ilipokuwa kazi imeanza baadhi yetu tulitaka serikali itafute njia ya kuwa na msimamo wa pamoja wa Wazanzibari, kujua nini wanakitaka katika mjadla ule.

Serikali ikatujibu humu humu ndani ya Baraza kwamba haitaki kuingilia maoni ya wananchi. Kwa hivyo, inawataka wananchi wawe huru na wananchi wameshamaliza kazi yao, na tume imeshamaliza kazi yake kubwa. Imebakia kuwasilisha rasimu yake kwenye Bunge la Katiba tu. Lakini bado Wazanzibari wamegawanyika katika mtizamo.

Hivi serikali mpaka leo haioni kwamba kuna haja yenyewe kama Baraza la Mawaziri, maana ndio chombo kikuu cha nchini kwa maana ya sera, kukaa na rasimu na kuja na muongozo ambao utawaongoza Wazanzibari na ikiwezekana kuwaunganisha ili kama Zanzibar kujua nini itarajie. Nini itegemee na nini wasemaji wa Zanzibar watakaokwenda kwenye Bunge la Katiba wakipiganie kwa ajili ya maslahi ya Zanzibar. Kwa nini serikali inakwepa wajibu wake katika hilo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, ilipotakiwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa hapa Rais wa nchi wakati ule Mhe. Dr. Aman Karume hakuonea haya wala kulionea aibu, alilisimamia na serikali ikawaongoza wananchi kupata mambo ambayo walikuwa wanaamini kwamba lina maslahi na nchi hii. Hili ni kubwa zaidi kuliko lile. Hili linazungumzia maslahi yetu, mambo ambayo tunayapigia kelele miaka nenda miaka rudi katika mfumo huu wa Muungano.

Kwa nini leo serikali inaona tabu kutoa msimamo. Pale awali ilisema haitaki kuingilia wananachi, wananchi wameshamaliza na kwa mujibu wa Jaji Warioba anasema maoni ya wananchi ndio yale ambayo wameyaandikia rasimu. Sasa bado kuna tofauti ya mtizamo kwa nini serikali inakwepa kuchukuwa wajibu wake wa kuongoza Wazanzibari ili kuwa na msimamo wa aina moja katika Bunge la Katiba kujua Wazanzibari wanataka nini.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa naomba kuzungumzia kidogo Ofisi ya Makamu wa Kwanza ili nisije kuinyima haki ya kuchangiwa hata kidogo.

Mhe. Naibu Spika, mwenzangu amezungumza hapa kwanza na mimi niunge mkono ripoti ya kamati katika suala la dawa za kulevya. Bado Mhe. Naibu Spika, kuna hatua fulani imepigwa lakini bado kuna tatizo na kama alivyosema Mhe. Salmin Awadhi tujiulize. Kwa sababu humo mitaani sehemu za mikusanyiko za vijana wanaotumia tunazijua. Sasa kwa nini wakakusanyike katika nyumba fulani wasije katika nyumba yangu mie. Bila ya shaka kuwa kuna kitu wanakifata pale. Sasa hiyo haitoshi kuwa muongozo kwa wale wanaosimamia sheria kujua nani wauzaji na nani wasambazaji wa dawa za kulevya.

Lakini isitoshe Mhe. Naibu Spika, suala la kuwekwa kituo cha Serikali baada ya kutegemea *Sober house* za watu binafsi. Bado kimekuwa ni kilio cha

kamati hii kila mwaka. Nadhani serikali inataka ije kutwambia hapa ina mpango gani kuhusu hili.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mbali ya hili pamezungumzwa hapa suala la uchafuzi wa mazingira ndio suala langu la mwisho. Kuna uchafuzi na uharibifu wa mazingira, wengi wameuzungumzia uharibifu wa mazingira. Mimi sitaki kuongezea kwa sababu nitakuwa narejea yale yale. Lakini kuna uchafuzi wa mazingira hali ya mitaa yetu haina usafi wa mazingira hata kidogo. Kama kuna jambo tumefeli basi ni hapo.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba Mhe. Waziri, atakapokuja aje anisaidie. Wao ndio wasimamizi najua kuna mamlaka mbali mbali katika Baraza la Manispaa, kuna Halmashauri za Wilaya na kuna wasimamia maji machafu na mitaro yake. Lakini kama wao Ofisi ya msaidizi wanachukuwa hatua gani kuona suala hili linapatiwa ufumbuzi. Na lile ambalo kamati imelitaja kuwa kuna miradi mingine mikubwa ya uwekezaji inakiuka sheria za mazingira kwa sababu *ZIPA* inashindwa kufanya wajibu wake. Kwa hivyo, waziri akija aje atwambie kwamba wana mpango gani kuwabana *ZIPA* ili kuona kwamba sheria za mazingira zinafuatwa ipasavyo na kunafanyika tathmini ya mazingira kabla ya kuruhusiwa mradi na Ofisi ya *ZIPA*.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme kwamba tumezipokea ripoti zile za serikali kama nilivyosema nyingi bado zinahitaji maelezo. Lakini ile ya kamati kwa kiasi kikubwa ukiondoa yale maeneo machache ambayo uliyosema natafautiana nao. Naunga mkono na nawatakia kila la kheri katika utendaji wao. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kwa mara nyengine tena jioni hii kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali waliochangia ripoti yetu hii ya utekelezaji katika Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora katika mwaka wa fedha uliopita.

Mhe. Naibu Spika, naomba awali nismhukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa wenyeviti Mhe. Hamza Hassan Juma, ambae ndie mwenyekiti wa kamati yetu. Kwanza kama alivyosema ingekuwa vyema kwamba ripoti hizi tukazipitisha kwenye kamati wakaweza kuziona ili mambo kama yale yasijirejee tena katika ripoti zao. Maoni yake hayo tumeyasikia na tutajitahidi mara ijayo basi tusifanye kosa hilo.

Kwa kweli mengi haya Mhe. Naibu Spika, waliyoagiza mwaka jana tumeyazungumza katika vikao vyetu mbali mbali kwa njia moja au nyengine

kama alivyosema. Kwa kweli tumeyajibu lakini kwa vile viporo vilivyobaki tutajitahidi kuona kwamba tumeyasawazisha.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru Wajumbe wote ambao wamechangia ripoti zetu hizi na maelekezo, maswali pamoja na ushauri mbali mbali waliotupa katika kuendeleza mbele utekelezaji wetu katika wizara, basi tumeupokea. Niseme tu siku zote unaposema Mhe. Ismail Jussa Ladhu, unapoweka kitu kwenye *Matrix* basi inakuwa kwa kweli ni *summary*, najua Mhe. Ismail Jussa, alikuwa anataka atueleze *DIASPORA* kwa kirefu. Kweli hayo mambo yapo lakini sasa kwenye *Matrix* siku zote inakuwa kwa kifupi tu.

Lakini *inshaallah* tutajitahidi hiyo kwa kifupi basi iweze kuelekezeka kwa urahisi zaidi ili mtu aweze kufahamu. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma, alizungumza na kutupongeza sana serikali kwa suala zima la kufanikisha sherehe kubwa ya Mapinduzi kutimiza miaka 50. Tunazipokea pongezi zetu. Lakini niseme hii ni kazi yetu ya pamoja na zaidi niseme tumshukuru zaidi Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ambae ndie aliekua Mwenyekiti wa kamati yetu ya Sherehe na Mapambo. Yeye alikuwa ndie Jamadari mkubwa wa mipango yoye.

Lakini na yeye nae hakufanya kazi peke yake alikuwa na kamati nzito kabisa na Makamo Mwenyekiti nilianza mimi baadae nikampa kijiti Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikao na Idara maalum. Yeye tumeona kwa uzito wa Tawala za Mikoa, basi Makamu mwenyekiti awe anasimamia yeye. Unajua sherehe ni watu na yeye ndie mwenye watu Tawala za Mikao yote, Wilaya, Shehia zote ndie dhamana yeye.

Kwa hivyo, Mhe. Hamza Hassan Juma, pongezi zetu tunazipokea kama tunavyosema kuwa shukurani hizo na mimi nizirudishe kwenu nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi kwa ujumla na sote kwa kufanikisha shehere hizo.

Mhe. Makame Mshimba rafiki yangu nakushukuru sana kwa ushauri mbali mbali uliotoa hasa kwa *CAG* kwamba atengenezewe sheria nyengine ili awe kama ana meno ya kutekeleza mambo yake. Hilo tumesikia na tutazidi kukaa na kuangalia sheria yake inasemaje kwanza, kama kuna sheria ya kutengeneza kanuni basi tutafanya hivyo laa hakuna tutaangalia utaratibu mwenginge.

Lakini kwa manitiki yake ripoti zake tunaziona na tunasema tu kwamba kwa kweli ripoti za *CAG* zinafanyiwa kazi, isionekane kwamba labda zinasomwa tu halafu tunazidharau, hata kidogo. Sisi bila ya kuficha kabisa serikalini

tunazivalia njuga, tunavunja kazi, tunazikalia, tunazipita, kuanzia sisi mawaziri, manaibu na watendaji wakuu wote na kila waziri anatakiwa ajibu zile hoja za *CAG*.

Kwa hivyo, naomba nimuhakikishie Mhe. Makame Mshimba usione kwamba labda ripoti za *CAG* zinadharauliwa, hata kidogo. Kwa hivyo, anatimiza wajibu wake kwa upande wake halafu anatuwachia sisi serikali nasi tutimize wajibu wetu. Halafu Mhe. Makame Mshimba alizungumzia suala la kitengo cha rushwa. Kitengo cha Rushwa maana yake ni kile kitengo cha Mamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi.

Nakumbuka Mhe. Ismail Jussa Ladhu, nae alizungumza kwamba mbona hatuoni hali yao, mbona na utekelezaji wao. Nataka kusema kwamba hiki kitengo ni kipya nakumbuka sote tulipitisha hii sheria hapa. Lakini kwa kweli suala lile linahitaji hekima na busara kubuwa sana katika utekelezaji wake.

Baada ya kupitisha sheria ndio tukaingia kazini sasa kwanza kufanya chombo chenyewe kiweje nani akae wapi. Baada ya kumaliza sasa tutafute watu au wafanyakazi, na chombo kama hiki lazima kitafute watu ambao wana wajibu mkubwa wanakuwa watu wazuri sio kila mmoja umfanye anafaa katika chombo hiki.

Baada ya kupata tija tunayotaka tutapata hasara. Kwa hivyo, kwa kweli uliona tumechelewa lakini mimi ninachosema bora kidogo kidogo kwa chombo kama hiki kukipanga vizuri, utafute watu ambao wanaweza kufanya kazi vizuri na halafu tuanze.

Kwa hiyo, baada ya kuwapata hawa watu kuwa- *identified* wamepewa mafunzo ya kutosha tena ya kijeshi kabisa, ya kinidhamu, na ya kimaadili. Walifunzwa kama miezi miwili. Wakachukuliwa wazuri kabisa, na baada ya kupata mafunzo tukawaambia kuwa nendeni kazini. Kwa hivyo, kitengo hiki hatari sana tayari kiko kazini toka mwezi Septemba mwaka jana. Na hayo aliyoyasema Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba ripoti baada za Baraza na nyenginezo sasa tayari tunawapa hizo kazi waanze.

Lakini kama nilivyosema mambo haya yanataka uadilifu mkubwa kabisa, umchunguze mtu ukweli na upate uhakika. Ttusije kuoneshana vidole umefanya kumbe hakufanya. Na tukamwacha yule aliekuwa kafanya tukamchukuwa asiefanya. Sasa nakuombeni tu tukipe ushirikiano mkubwa chombo hiki ni kizuri kitatusaidia katika kuwajibika sote ipasavyo.

Halafu Mhe. Makeme Mshimba alizungumzia suala la Ikulu ya Micheweni. Hili nalo Mhe. Subeit Khamis Faki nalo alilizungumza, vile vile Mhe. Ismail Jussa Ladhu na wengine. Nataka kusema tu kwamba Ikulu ya Michweni Mhe. Naibu Spika, tumefika pazuri tuliunda *Task Force* ndogo ya mawaziri watatu, Waziri wa Fedha, Waziri wa Nchi (AR) Ikulu na Utawala Bora, pamoja na Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum. Kwa kweli hapo tuliwasiliana kabisa na Mhe. Waziri wa Fedha na yeye amenijulisha ambae tulimwachia kazi ya mwisho.

Akanambia kwamba tumeunda timu ya pamoja kama nilivyosema Tawala za Mikoa, Ikulu na Fedha. Michoro itatuongoza na msimamizi wa ujenzi ni *engineer* wa Ikulu maarufu pale Ndugu Machungwa. Tumeanza kutafuta pesa kwa ajili ya kujenga jengo la viongozi kama tulivyopanga. Labda hii ni mipango sasa niseme imeshaelekea, lakini sasa tatizo ni nini, lile tatizo tulilokuwa nalo tumelikwamua vipi. Tumemwita ndugu yetu *contractor* ambae niseme aliyekuja baadae, maana yake *contractor* wa mradi ule ni marehemu.

Huyu bwana alikuwa London ndugu yake huyo *contractor*. Tukakaa nae yeye akatoa hesabu zake kwa urefu kabisa na sisi tukampa hesabu zetu. Katibu Mkuu wa Fedha kupitia Mhasibu Mkuu akatoa pesa zote ambazo marehemu alilipwa. Sasa yeye kwa bahati mbaya anadai kwamba kuna malipo anahitaji.

Kwa hivyo. tulichuana siku nyingi kwa suala hili, lakini mpaka dakika ya mwisho tukamwambia wewe lete vielelezo vyako vyote. Akaleta vielelezo vyake na sisi tukampa vile tulivyomlipa, kakubali kwamba kweli hatudai, isipokuwa sisi tunamdai kwa kiwango kile cha kazi alichofanya na kwa kweli inaelekea ni kama tumemlipa zaidi.

Sasa tukasema basi tufanye *reconciliation* hapo alipofika ili tupate *the way forward*. Tumeogopa tusije tukampa mtu mwengine akaanza ujenzi halafu yeye tena akaja akatupeleka Mahakamani. Tukaona bora tukubaliane nae tusafiane nia. Na *alhamdulillah* kazi hiyo Mhe. Waziri wa Fedha, Mhe. Haji Omar Kheir na mimi tulikaa pamoja hilo tumelimaliza na mwenyewe kakiri. Sasa hivi ndio tunakuja hii awamu ya pili tunapitia michoro upya ili tuone hatua gani na tuongeze nini. Tumegundua kwamba kweli kuna mapungufu katika vibanda vya ulinzi, ukuta wenyewe ule na baadhi ya mambo. Ile ni Ikulu Ndogo lazima kuwe na mambo ya kuongeza sio ilivyo hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Subeit Khamis Faki, bahati mbaya yupo nje lakini kama anaiona machoni vile ilivyo haijawa bado kuitwa kwamba ni *State Lodge*. Sasa ninachotaka kusema tu kwamba *alhamdulillah* sasa

tumeshakubaliana, yule bwana tumemalizana nae, sio tumemalizana kama tumegombana, kwa nia safi kabisa na yeye inaelekea kakubali. Sasa tunaanza kazi ya awamu ya pili kuipitia michoro, kuweka sawa mambo, ili ujenzi uanze rasmi.

Na bahati nzuri pesa tume-*budget* katika mwaka huu wa fedha. *Inshaallah* hazitorudi kazi tutaanza. Kwa hivyo, kwa upande wa ile *Rest House* ya Micheweni niseme hivyo tu kwamba nia ipo na ari ipo, na *inshaallah* sasa mambo yameshakaa sawa tutayamaliza.

Halafu alifuata Mhe. Ismail Jussa Ladhu wa Mji Mkongwe. Alituuliza Wazanzibari walio nchi za nje, kama nilivyosema ameona kidogo pana ufinyu wa ile habari. Ni kweli pale kama nilivyosema tumeweka kwa kifupi, lakini kazi yetu kubwa sasa tuliyonayo hivi sasa kwenda ulimwengu mzima kuwatafuta Wazanzibari waliopo huko nje, kama Ulaya, Marekani, Marekani ya Kusini, nchi za Kiarabu, India na kwengineko. *Alhamdulillah* wazanzibari tumetapakaa ulimwengu mzima kutafuta maisha.

Sasa lengo letu kuwashawishi kwamba warudi nyumbani, au wasirudi nyumbani lakini hizo *benefits* zao au mambo wanayoyavuna huko basi wafaidishe ndugu zao au maendeleo ya nchi yao. *Alhamdulillah* tunawatumia na hao waliorudi hapa. Hawa waliorudi ndio waliotusaidia kuwajua wale waliopo kule, sasa hiyo si kazi ndogo. Kuna wengine unajua wanapenda wajulikane, wengine hawapendi wajulikane, inabidi lazima tutumie hekima na busara.

Sasa katika kuwaorodhesha tunatengeneza *web site* ili tuwe kama mtandao wa kuulizana hali na kujuana. Tunawaita Ikulu kidogo tunazungumza nao, kwa hivyo hii kazi nayo inahitaji busara, inahitaji hekima pia. Unajua kama nilivyosema kuna wengine labda wangependa mambo yao yafahamike, lakini wengine yasifahamike.

Kuna kile kikundi cha *Help Age,* kuna baadhi ya Wazanzibari waliokuwa Canada kule wamefungua hospitali Shangani pale, wamejikusanya wenyewe wamejenga hospitali Unguja Ukuu pale, na wamekarabati madarasa. Hospitali ya Shangani pale wanang'oa meno vizuri tu tena kwa bei nafuu ukilinganisha na wengine. Sasa hiyo ndio juhudi tunayofanya ya kuwakusanya Wazanzibari, tija kama hizo walete nchini kwetu. Kwa hivyo, hiyo nakiri Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba hayo maelezo labda machache hapo lakini *inshaallah* kwa siku za mbele tutayaongezea nyama zaidi.

Jengo la *ZIPA* kwamba ni bovu, Kamisheni ya Utumishi imeondoka. Sasa sisi tunasema hawa *DIASPORA* tunawapeleka kule namna gani? Lakini

nafikiri Mhe. Ismail Jussa Ladhu sasa hivi ukipita utaona mabadiliko ya jengo lile. Kwanza Utumishi wameshahama siku nyingi sana, lakini na hawa wengine wote nao tumewahamisha wasije wakaangukiwa kama ulivyosema.

Kwa hivyo, tumewahamisha na ukarabati sasa hivi umeshafikia *stage* nzuri sana. *Inshaallah* nafikiri ndani ya miezi miwili mitatu kama itatimia watarudi watumishi. Jengo zuri na nakualika kama Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, tulimualika kwa nafasi yake kwa sababu na yeye alituhoji suala hili twende mkalitembelee hakuna wasiwasi. Jengo zuri linakalika na lina nafasi kubwa kabisa.

Halafu Mhe. Ismail Jussa Ladhu, aliuliza suala la hatimiliki. Ni kweli tumekamilisha ya Ikulu tu, nyengine nasema utekelezaji wake unaendelea. Unajua hatimiliki kuna mtiririko sio kama kuandika tu karatasi. Kwanza maeneo yale yapimwe, yahakikiwe, halafu hiyo hatimiliki ni kazi ya mwisho kabisa ambayo asaini Mhe. Waziri. Kwa hivyo, ni kazi kubwa kidogo inachukua muda mrefu na hatupi bure Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati nae tumlipe. Kwa hivyo, inahitaji tuingize kwenye bajeti hayo majengo yote tumlipe kwa pesa. Kwa hivyo, ninachosema kwamba kazi nzuri umeuliza Pemba kweli, tulisema kwanza tuanze Unguja tukishamaliza tutaelekea Pemba.

Pia, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, aliuliza suala la Mhe. Rais Mstaafu Mzee Benjamin William Mkapa, kwa nini kalazwa kwenye Hoteli ya Hifadhi ambayo umelala yeye. Kwanza nataka kusema Hoteli ya Hifadhi si mbaya sana, mimi najua hoteli kama ile sijui kama ina nyota gani, labda Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo atatwambia kama *three stars.* Lakini kuna vyumba maalum ambapo Waheshimiwa wenye hadhi kama Rais Mstaafu wanalala pale. Mhe. Makamu wa Mwanzo analala pale, Makamu wa Pili na viongozi wengine. Kwa hiyo, *suite* kama zile mtu mdogo kama mimi siwezi kulala, lakini kama una fedha yako Mhe. Jussa hata wewe unaweza kulala.

Sasa mimi nime-*check* na wenzangu wa Ikulu kule Pemba wakanambia hakukuwa kwa kweli na maombi ya Mzee Benjamin William Mkapa kukaa Ikulu. Utaratibu wenyewe wa Sherehe na Mapambo ndio walioandaa ratiba wakampangia kwenda kuizindua ile skuli ya Benjamin Mkapa. Kwa hiyo, akapangiwa kulala pale na karidhika kabisa, kaondoka vizuri.

Kwa kweli hatuthubutu kwamba apangiwe mahala halafu sisi tukapangue hata kidogo. Kwa kweli wamenambia hawakukuwa na taarifa ile, sijui Mhe. Ismail Jussa Ladhu, aliipata wapi taarifa hiyo kwamba alipangiwa kule.

Lakini nataka kusema tu kwamba hakupangiwa, hiyo taarifa nimefuatilia na nimehakikishiwa kwamba kwa kweli hakupangiwa.

Jengine Mhe. Salmin Awadh Salmin, nae alizungumza, tunamshukuru sana kwa ushauri wake na yote ambayo ametueleza. Amezungumzia zaidi upande wa polisi hilo namwachia mwenzangu Kaimu Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili atakuja kulizungumzia.

Lakini nataka kuzungumza tu kwamba tunazungumzia masuala kama haya ya polisi, haya masuala ni yetu sote lazima tuwasaidie wenzetu hawa, wao wana sehemu yao. Lakini na sisi tuwasaidie nakusudia kama *informal*, haidhuru tunawa-*inform* hayo mambo hatukuyatoa wana sehemu yao, lakini kuna mambo na sisi tuwasaidie. Na tunashukuru walitupa ushauri wa ulinzi shirikishi au Polisi Jamii na katika maeneo yetu unakwenda vizuri sana. Na Mji Mkongwe kwako Mhe. Ismail Jussa Ladhu, na kwengineko wanafanya vizuri sana katika suala hili. Namwachia mwenyewe Mhe. Haji Omar Kheir, atakuja kuliweka sawa.

Kwa ufupi Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Wizara yetu niseme *quiry* kubwa ndio hizo, kama kuna mengine ambayo nimeyasahau basi naomba iwe bahati mbaya, lakini tutayashughulikia na tutayazingatia katika utendaji wetu. Na yote niseme kwa ujumla ushauri wenu tumeupokea, tutauzingatia katika utendaji wetu, *inshaallah* yasirudi tena kwa mwakani. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais) Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wameyasema. Lakini kama ilivyo kawaida ni utaratibu kwamba ripoti hii inayowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inatakiwa mwakani tulete majibu juu ya yale yote ambayo yamezungumziwa ndani ya ripoti hii.

Kwa hivyo, yapo mambo nitayagusia kwa umuhimu wake na yapo mambo naomba Wajumbe waridhie kusema kwamba tutakwenda kuyafanyia kazi kama ulivyo utaratibu wetu. Vyenginevyo tutakuwa tunafanya *duplication*, leo tutakuwa tunatoa majibu na baadae tutatakiwa tulete majibu ya maagizo na ya ule ushauri wa Kamati.

Mhe. Naibu Spika, nataka nichukue fursa hii kuwapongeza wale wote ambao wametoa maoni yao, maoni yao ni muhimu sana kwa hatma ya nchi yetu.

Lakini mimi sitaki nitaje Mjumbe mmoja mmoja isipokuwa nitataja zile *issues* ambazo zimejitokeza katika maoni yaliyotolewa hasa katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais au katika ripoti yetu ile ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

La kwanza kwa umuhimu wake nataka nilizungumzie suala lile la mgogoro wa ardhi linalomhusu mwekezaji wa *Crystal's Resort Limited* kule Paje ambalo lilizungumzwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mhe. Hamza Hassan Juma, lakini vile vile, lilizungumziwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Waheshimiwa wengine.

Nataka niseme kwamba nakubaliana kwanza na ushauri wa Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Kama mamlaka zinazohusika zimeshatoa maelekezo na bado mwekezaji hajatii amri hii, naomba niseme kwa sababu Wizara yangu imetajwa, kwamba imepeleka taarifa inayohusu Tawala za Mikoa na Idara Maalum, Mikoa imepeleka taarifa na Halmashauri zimechukua hatua za kupeleka taarifa. Nataka nimhakikishie Mhe. Hamza Hassan Juma, kwamba mimi na yeye tutafuatana twende tukamwone huyo mwekezaji aliyekuwa hasikii ni wa aina gani katika nchi hii. Hataki kusikiliza maelekezo ya Serikali. Sasa wakati huo tutaona yeye au sisi kama yale maelekezo ya Serikali hataki kuyafuata. Na kama hataki kuyafuata kwa sababu zile ambazo Waheshimiwa Wajumbe wamezisema basi tutawaona na hao wanaompa deko hili ambalo analifanya hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo lilijitokeza ni kwamba Wizara zikae na Kamati kabla pengine hazijawasilisha Ripoti za Serikali hapa Barazani. Mimi nadhani si vibaya hata kidogo kufanya hivyo, lakini sina hakika na utaratibu. Utaratibu unasema kwamba Kamati inawasilisha ripoti zake ndani ya Kamati za Kudumu. Kamati za Kudumu zikishatoa maelekezo yake nafikiri kwa sababu ndizo Kamati hizo hizo ambazo zinafanya shughuli za kila siku za kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Si tatizo wakati ule Kamati inafanya shughuli zile za ufuatiliaji wa shughuli za Wizara na shughuli hizi nazo zikawa zinazungumzwa ili tukawa tunazungumza lugha moja tunapokuja hapa.

Vyenginevyo ni kweli mimi naona umuhimu wa kufanya hivyo. Lakini mimi ushauri wangu au Serikali inashauri kwamba kwa sababu Kamati ndizo hizi hizi ambazo zinafanya kazi za kuzifuatilia Wizara kwa kazi za kila siku, basi ni vizuri kazi hizi zikawa zinafanyika wakati ule Kamati ambapo inazifanya. Wizara itakuwa inazo zile hoja na maagizo, lakini vile vile, Kamati zitakuwa

zinajua wameiagiza nini Wizara katika kipindi cha mwaka ule wa bajeti unaofuata.

Kuhusu suala la kadhia ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Limezungumzwa hapa sana, alianza kuzungumza Mhe. Waziri wa Afya, akalitolea maelezo Mhe. Hija Hassan Hija, akafuata Mhe. Subeit Khamis Faki na wengineo wamelizungumza.

Lakini tatizo lililojitokeza kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub katika Hospitali ya Mnazi Mmoja halikuwa la kupendeza na halikustahili kujitokeza kwa Mjumbe wa Baraza. Jambo linaloweza kuchunguzwa na Kamati ya Maadili na Kinga za Wajumbe ikiwa tu litafikishwa mbele ya Kamati hiyo, kanuni ya 119 (2) (a) inatoa mamlaka kwa Kamati hiyo kuchunguza na kutoa maamuzi ya masuala mbali mbali yakiwemo yale yanayohusu kinga, fursa, mamlaka na madaraka ya Wajumbe.

Lakini masuala hayo yawe yamepelekwa mbele ya Kamati na Spika au Mjumbe yeyote wa Baraza. Hivyo, Mjumbe akiona kuwa kuna jambo linalohusu mambo hayo yaliyotajwa anaweza kulipeleka suala hilo mbele ya Kamati ya Maadili kwa ajili ya kuchunguzwa.

Sasa kwa sababu utaratibu wa kikanuni upo, mimi nadhani Mhe.Naibu Spika, unayo mamlaka hiyo ya kuweza kuelekeza tufanye nini juu ya suala hili. Nisingependa kuendelea zaidi katika kulizungumzia suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo limejitokeza ni suala zima la madawa ya kulevya yaliyokamatwa Uwanja wa Ndege. Mimi sitaki kuzungumzia utaratibu mzima wa Serikali, Waziri muhusika atakuja kuzungumzia. Mimi nataka nizungumzie hili suala la hatua gani zimechukuliwa juu ya tukio lile ambalo limefanyika.

Mhe. Naibu Spika, kama alivyosema Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na Waheshimiwa wengine, jambo hili kweli limetokea na baada ya kutokea kweli ilitokea purukushani ya kuchukuliwa baadhi ya watumishi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Na mimi kama Kaimu Waziri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais nilipokea suala hili, na baada ya kulipokea niliagizwa na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nilifuatilie kwa ukamilifu ili kujua hatma ya jambo hili ikoje.

Kwanza nataka nikiri ni kweli pamekamatwa madawa ya kulevya, na baada ya hilo tatizo lililojitokeza la kukamatwa wafanyakazi wa mamlaka ambao walituhumiwa tuliona kwamba kweli hao vijana watoke kwa dhamana. Lakini wakati huo huo, Serikali tumefanya juhudi kubwa ya kwenda

kuangalia kumbukumbu za *CCTV* na tumepata baadhi ya mambo sitaki niyaeleze hapa. Na Serikali inaendelea kuangalia kumbukumbu za *CCTV* kwa kipindi cha mwezi mzima tuone *movement* yule aliyeyachukua yale mabegi akayafikisha pale ambapo yamekamatwa. Na bila shaka tumeshaanza kupata watu ambao wanahusika, ningeliomba Baraza la Wawakilishi likatustahamilia Serikali.

Na katika hili si katika yale mambo yanayojitokeza siku zote, nataka niseme tutu imepata kiziwi. Kwa hili kwa sababu tumeshaanza kuona waliohusika ni nani, basi. Serikali tutakuja kuleta taarifa mbele yenu, lakini kwa sababu ya taratibu za kipelelezi si vizuri kabisa tukaanza kulitolea maelezo hapa leo. Lakini kwa kweli ni jambo ambalo sisi kama Serikali hatulifurahii kwa sababu linatia aibu ya nchi yetu. Kwa hivyo, nakuombeni Waheshimiwa Wajumbe mtuamini kwamba hili jambo tunalifanyia kazi na tumeshaanza kupata taarifa nyingi zinazohusu jambo hili na wahusika ni akina nani. Tustahamilieni tukamilishe taratibu ili hatimae Serikali ijue inachukua hatua gani juu ya hao watu ambao wamehusika.

Agizo jengine lile lililosemwa kuhusu suala la watu wanaodai katika meli ile ya *Spice Islander*. Mimi sitaki nikatae, lakini kwa ushahidi tulionao katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ilionesha kwamba watu walimalizika. Lakini kama wanajitokeza watu wengine ambao wanadai mimi nadhani Mhe. Salmin Awadh Salmin, tushirikiane kuweza kuwapata hao watu wahusika waje katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili tufuatilie tuone ukweli wa mambo.

Na kama kweli hawa watu watakuwa hawajapata haki yao Serikali haina nia ya kumdhulumu mtu yeyote yule, basi watapata haki yao lakini lazima tupate vielelezo vya kutosha. Kwa hivyo, Mhe. Salmin Awadh Salmin, tutakuomba sana tushirikiane na wewe ili kuona ukweli wa jambo hili, na kama yupo mtu hajapata haki yake basi aweze kupata haki yake.

Kuhusu suala la usalama wa Zanzibar. Ni kweli hivi karibuni limejitokeza suala la wimbi la uhalifu mkubwa wa kutumia silaha za moto. Nataka niwahakikishie kwamba Serikali kupitia vyombo vya ulinzi na usalama tutajitahidi sana kuona kwamba jambo hilo linadhibitiwa na kuwatoa khofu wananchi. Kwa sababu tukiwaachia wananchi wetu wakiendelea kujawa na khofu nadhani hatima yake ni kwamba nchi haitatawalika. Kwa hivyo, sisi kama Serikali tutajitahidi sana nchi hii iweze kutawalika kwa hali ya amani, utulivu na usalama.

Vile vile umezungumzia juu ya suala la wafanyakazi wa Jeshi la Polisi kuvamia kwenye nyumba ya mtu binafsi na kwenda kufanya vurugu na

kuharibu baadhi ya mali. Nataka nikuhakikishie kwamba Serikali italichukulia hatua jambo hili, na wale wote ambao walihusika na jambo hili wakibainika kwamba wana makosa basi watachukuliwa hatua zinazofaa.

Pia umezungumzia suala la mfanyabiashara aliyefunguliwa *briefcase* pale na kumwambia ofisa wa uwanja wa ndege kwamba unaipenda kazi yako. Bado nataka nilirejee kama lile la mwekezaji wa *Crystal.* Watu wa namna hiyo hatuwezi kuwastahamilia wakaweza kuikamata Serikali yetu mkononi. Serikali hii hakuna mwenye mkono mkubwa wa kuweza kuifumbata. Kwa hivyo, mimi nataka nikutoe wasiwasi Mhe. Salmin Awadh Salmin, kwamba kama hilo wamelisema sisi tutamfuatilia na kama kweli ana tabia hiyo basi tutamwona kama yeye anaweza akaikunyata Serikali.

Lakini nataka nikuthibitishie ule uhamisho uliofanyika kwa yule mfanyakazi ni uhamisho wa kawaida wala hauhusiani na jambo hilo. Ipo shaka kwamba kwa sababu yule mfanyabiashara alisema vile inawezekana ukawepo wasiwasi kwamba pengine suala lile ndilo lililompelekea aweze kuhamishwa. Lakini pamoja na kwamba ilikua uhamisho wa kawaida sisi tutamfuatilia huyo mfanyabiashara ili tujue je, anao mwenendo na utaratibu wa kutumia nafasi ya biashara yake akaweza kuidhalilisha Serikali? Na kama yupo basi Serikali itamwona na itajua nini iweze kukifanya.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo limejitokeza ni suala la *echo* ya Baraza la Wawakilishi. Suala hili kweli ni la muda mrefu na sote ni mashahidi, na sote hatulipendelei. Tunapokuwa hapa ni kweli kabisa tunapata tabu.

Lakini ninachotaka kusema ni kwamba Baraza lilichukua hatua. Kampuni mbali mbali zimealikwa kufanya kazi hii. Lakini ikabainika kwamba gharama ambayo inatakiwa na hizo kampuni ni kubwa haimo ndani ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Sasa mimi nadhani zipo kampuni sitaki nizitaje kwa sababu si utaratibu mzuri kuzitaja kampuni ambazo bado hazijafika kwenye mamlaka ambayo inahusu.

Sasa mimi naomba muiamini Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi. Na kwa sababu ni Wajumbe nyinyi nyinyi ndio mnaopitisha bajeti, basi mimi nadhani cha msingi tukubaliane tutumie utaratibu wa ki-Serikali wa matumizi ya fedha tuweze kulitatua tatizo hili.

Limezungumzwa sana suala la Mchapaji Mkuu wa Serikali. Na mimi nataka nikubaliane kabisa kwamba wapo waliotoa wazo hasa Kamati imesema ni vizuri tangu mwaka jana taasisi hii iwe inajitegemea. Lakini yapo mawazo kwamba unapoifanya taasisi hii kuwa inajitegemea itakuwa ya kibiashara zaidi kuliko kuweza kufanya kazi za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba Idara hii ya Uchapaji hivi sasa ni idara na ndipo alipo Mchapaji Mkuu wa Serikali. Na hivi sasa Serikali imewekeza fedha nyingi katika Kiwanda kile cha Uchapaji. Zipo mashine ambazo zimeanza kufanya kazi na mfano hai mtauona katika baadhi ya vitabu vyetu tulivyovitumia katika sherehe. Ilifika pahala dakika ya mwisho tukaamua kufanya marekebisho ya ratiba, lakini Idara ya Mchapaji Mkuu wa Serikali ikaweza kuifanya kazi hii bila kupeleka kazi hii nje.

Kwa hivyo, ni nia ya Serikali kwamba hii Idara ya Uchapaji kuifanya kuwa ni Kituo cha Mchapaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuchapisha machapisho mbali mbali ya Serikali, na kuweka usiri wa *document* zile za Serikali kama nchi nyengine zilivyo. Serikali imewekeza pesa nyingi na itaendelea kuwekeza ili kuihuisha ile Idara iweze kukidhi mahitaji ya Serikali.

Lakini inapotokezea kwamba kuna kazi zinatakiwa kufanywa kutoka nje ya Serikali, nadhani hilo hatufungwi kuweza kuzifanya kazi hizo. Na vile vile ikifikia pahala kwamba Mchapaji Mkuu wa Serikali anao uwezo wa kujiendesha kutokana na mapato ambayo anayapata nadhani hilo halina tatizo.

Kwa hivyo, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu na hasa Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ambaye amekuja hata na mifano amezungumzia pia suala la *hansard*. Nitalizungumzia suala la *hansard* lakini katika eneo hili la Mchapaji Mkuu naomba niishie hapo. Kwa kweli kama zilivyo nchi nyengine na sisi tunapaswa kuwa na Mchapaji Mkuu wa Serikali ambaye atachapisha mambo mbali mbali yanayohusu suala la *documents* za serikali.

Suala la migogoro ya ardhi kama nilivyokwisha kusema kwenye ule mgogoro mmoja, lakini kama munavyojua Waheshimiwa Wajumbe itakapofika sekta husika ninafikiri na yeye atakuja kutoa maelezo. Lakini ripoti ya migogoro ya ardhi ya Kamati Teule imewasilishwa tu kwenye kikao cha Baraza la Wawakilishi kilichopita.

Ni vizuri tukasubiri serikali itakuja na majibu gani, pengine isiwe na yale ambayo tumeyaweka kutokana na maagizo ya kamati, inaweza ikawa na majibu mazuri hasa kutokana na yale maelekezo na michango ambayo Waheshimiwa Wajumbe mulikuwa mukichangia na yale mambo ambayo yalijitokeza katika ripoti ile.

Sasa isingekuwa vyema tukaanza kutoa majibu ya ripoti ya Kamati Teule ya ardhi kabla ya muda wa taarifa ile kutoka serikalini haujafika. Tusubiri muda

ufike wa kuleta taarifa ile, bila shaka wakati huo ndio utakuwa wakati muafaka wa kuweza kuyachambua. Haya yaliyojitokeza kwenye ripoti au kwenye utekelezaji wa ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ni yale ambayo aliagizwa na kamati na sisi tumeyajibu kwa mujibu wa vile ambavyo yameagizwa. Lakini kwa ukamilifu wake kuhusu migogoro ya ardhi ningeomba Baraza hili Mhe. Naibu Spika, tukasubiri wakati huo.

Suala jengine lililojitokeza kwenye mjadala huu ni kuhusu suala la kuhamiwa kwa nyumba ya Spika. Mimi ninadhani sasa hivi tutoe ahadi ya mwisho kama serikali kwa kushirikiana na Baraza la Wawakilishi kwamba Mhe. Spika, mara tu baada ya kurudi kwenye Bunge la Katiba atahamia rasmi kwenye nyumba yake. (*Makofi*).

Yapo matatizo ambayo yamejitokeza ya ukosefu wa maji safi na salama. Inaonekana kimechimbwa kisima pale, lakini bado hakitoi maji. Tunadhani kwa muda huu wa kipindi cha miezi miwili tatizo la maji safi na salama katika nyumba ya makaazi ya Mhe. Spika, litakuwa limekamilika. Sasa sisi kama serikali tunasema tutakaporudi kwenye Bunge la Katiba pengine wakati huo bajeti imeanza, Mhe. Spika, atakuwa ameshahamia kwenye nyumba yake ile ili iweze kutumika kama vile ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mafunzo ya rasimu ya Katiba, limezungumzwa pia kwa Wajumbe. Katika kikao cha bodi ya mradi wa kuimarisha vyombo vya kutunga sheria unaoratibiwa na *UNDP*, suala la mafunzo kuhusiana na Bunge maalum ulionekana kuwa na umuhimu mkubwa na hivyo kukubaliana kufanyika warsha kwa Wajumbe na Wajumbe wengine wa Bunge Maalum kutoka Zanzibar. Matayarisho ya semina hiyo yameanza na Wajumbe watajuulishwa rasmi tarehe na mahala ambapo warsha hiyo itafanyika.

Lilijitokeza pia suala la kuzungumzia suala la msimamo. Mimi ninadhani kama serikali tuache sasa hivi katika kipindi cha kwenda kwenye Bunge la Katiba, tuache Waheshimiwa Wajumbe wenyewe wa Bunge la Katiba kufuatia maoni watakayopewa na wananchi wao twende tukatoe maelezo yetu, tukajenge hoja, tunataka Katiba ya namna gani. Lakini kama serikali kama tunavyosema siku zote, hatuwezi kuwa na msimamo wa kusema tuwaambie nini Waheshimiwa Wajumbe wa Bunge la Katiba.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla nilikuwa na hayo ya kuweza kuyaeleza, yale mengine kama nilivyosema mwanzo, yapo mengine tutayaleta rasmi wakati muafaka tutakapowasilisha utekelezaji wa maagizo yale ambayo tutakuwa tumeagizwa na kamati hii ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Ninataka nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wake kwa kushirikiana na sisi katika kutukosoa na kutushauri juu ya mambo mbali mbali na kwa hakika mambo yote ambayo wanatushauri yanatusaidia au yanaisaidia sana serikali katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru tena *Allah* kwa kutujaalia uzima wa afya na kuweza kuwepo tena hapa kuendelea na shughuli zetu kwa manufaa ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

Na ninapenda pia nitangulie kwa kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kuweza kuwasilisha ripoti yake ya 2013/2014. Lakini vile vile, kutoa maoni na ushauri zaidi juu ya yale ambayo tumeyajibu kutokana na ripoti ya 2012/2013.

Nimuhakikishie kwamba ofisi yangu inachukua na inapokea ushauri na maagizo yote kwa ajili ya kuyafanyia kazi, kwani ndio chachu ya utekelezaji bora wa shughuli zetu za kila siku ndani ya ofisi.

Mhe. Naibu Spika, kuna jumla ya wachangiaji watano ambao wamepata nafasi na fursa ya kuchangia uwasilishwaji wa majibu ya maagizo, lakini pia ripoti ambayo imewasilishwa na mwenyekiti. Kwa ufupi sana na ninaomba nitangulie kuwataja:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2.Mhe. Hija Hassan Hija
3.Mhe. Subeit Khamis Faki
4.Mhe. Salmin Awadh Salmin
5.Mhe. Ismail Jussa Ladhu

Mhe. Naibu Spika, nitapenda kuyazungumzia yale ambayo bado hayajatolewa maelezo yanayohusiana na ofisi yangu. Nitapenda kuyaunganisha kwa sababu yanafanana niyajibu kwa pamoja isipokuwa yale ambayo kivyake-vyake basi nitayajibu peke yake.

Na ninaomba nianze kwa suala zima la uharibifu na uchafuzi wa mazingira ambao karibu Wajumbe wote hawa wamelizungumzia kiaina yake. Na ni-*quote* ile *statement* ya Mhe. Salmin Awadh Salmin, kwamba anasikitishwa sana kwamba kila tukija tunasema bado tunachangamoto ya uharibifu wa mazingira.

Mhe. Naibu Spika, ndio ukweli wenyewe na ofisi yangu itaendelea kuripoti hivyo mpaka pale hali itakapokuwa nzuri, basi tutawaambia Wajumbe pamoja na wananchi kwa ujumla hali halisi ilivyo. Ni vyema tueleze ule uhalisia wenyewe. Kwa sasa kwa kweli uharibifu na uchafuzi wa mazingira ni mkubwa mno ndani ya visiwa vyetu pamoja na jitihada kubwa inayofanywa na ofisi yangu na wadau wengine wa mazingira.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Subeit Khamis Faki, alilielezea kwamba katika wachafuzi wa mazingira ambao wanaongoza kwa muono wake yeye ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika shughuli zake za ujenzi wa barabara, pale inapokwenda kuchimba vifusi katika maeneo na kuacha mashimo ambayo hayarejeshwi katika hali yake iliyokuwa au angalau kuweza kuziba kwa kiasi fulani.

Naomba niahidi ndani ya Baraza hili kwamba kulikuwa na mapungufu ndani ya sheria ya mazingira ambayo kwa sheria mpya ambayo asubuhi hii nilisema kwamba tutaileta ndani ya Baraza hili, mianya hiyo imezibwa na sasa kutakuwa na mkataba maalum kwa yeyote ambaye anataka kuchimba raslimali iliyoopo, aidha kwa shughuli yake mwenyewe ya maendeleo au kwa shughuli za serikali za maendeleo, basi kuweza kuweka mkataba wa kuweza kurejesha hali iwe nzuri katika maeneo ambayo amechimba maliasili hiyo, iwe ni kifusi, mawe na aina hiyo ya maliasili. Kwa hivyo, hilo huenda tukapata ufumbuzi wake hivi karibuni.

Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na Mhe. Hija Hassan Hija, wote walieleza kwamba bado Idara ya Mazingira iendelee kutoa kwa jitihada kubwa sana taaluma kwa jamii juu ya uhifadhi wa mazingira na suala zima la athari ya mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, hili tunalichukua tunalifanyia kazi na tutaendelea kuongeza jitihada katika kutoa elimu hiyo.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye suala la Mtambuka. Suala gumu, zito na la kimataifa na hili ni suala zima la mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Waheshimiwa wote ambao nimewataja hapa wamegusia suala hilo na wameonesha hisia zao kwa kuzungumza kwa ukali sana.

Kwa kweli hata mimi mwenyewe ninaona ule ubaya uliopo, sote hata serikali pia inaona ubaya na uzito wa suala hili la dawa za kulevya, linavyoathiri maendeleo ya nchi yetu, vijana wetu. Lakini vile vile, kwa upande linavyoongeza maambikizo ya gonjwa la Ukimwi kwa sababu suala la dawa za kulevya, hasa katika suala la utumiaji linakwenda sambamba na kuongezeka kwa gonjwa la Ukimwi.

Kwa hivyo, serikali inafanya jitiahda kubwa, lakini leo itakuwa mara ya pili au tatu ninaendelea kutoa taaluma hii ndani ya Baraza. Baadhi ya Wajumbe wamesema kwa nini tumeweza kuzuia suala zima la magendo ya karafuu, lakini tunashindwa na suala la usafirishaji wa dawa za kulevya?

Mhe. Naibu Spika, ningeomba Wajumbe watofautishe kidogo ugumu wa masuala haya mawili. Suala la usafirishaji na matumizi ya madawa ya kulevya ni zito sana kuliko suala la kuzuia magendo ya karafuu. Kwanza ukiangalia kwamba suala lenyewe linawagusa wadau wengi; ni suala ambalo ni Mtambuka kuliko suala zima la magendo ya karafuu ambalo linawagusa wadau, lakini sio wengi kama ilivyo hapa.

Lakini pili, kwamba hili suala lenyewe ni la kimataifa. Mataifa yote duniani yamo katika kupigana na suala hili la usafirishaji na matumizi ya madawa ya kulevya. Hasa sasa vita hivi vimepamba moto kwa sababu kuhusisha fedha chafu inayopatikana katika usafirishaji wa dawa za kulevya na matokeo ya kigaidi ambayo yameenea katika dunia. Kwa hivyo, vita vya usafirishaji wa dawa za kulevya sasa hivi vimepamba moto na mataifa yanakuwa makini sana na kuna jitihada za pamoja katika kuhakikisha kwamba suala hili linapata mafanikio.

Lakini pia, suala hili linawahusisha wahalifu ambao wana fedha nyingi. Mhe. Naibu Spika, watu wahalifu wanaokamatwa na dawa za kulevya, kwao wao kutoa hongo ya dola laki nne mpaka dola laki tano kwa mzigo mdogo wa dawa, kwao wao hiyo sio neno, kubwa tofauti na magendo ya karafuu, unaweza ukaona ule uzito wake. Hawa ni watu ambao kwa sababu ni biashara wanaendelea nayo na biashara inayoingiza mamilioni ya fedha, wapo tayari kutoa hongo ya aina yoyote.

Sasa Mhe. Naibu Spika, huu ni ugumu kidogo tunaupata, lakini pia siku za nyuma nilieleza na ninaendelea kurejea kusema kwamba tunapata taabu vile vile vikosi vyetu vya ulinzi na usalama katika kupambana na usafirishaji na uingizwaji wa dawa hizi kutokana na hali ya nchi yetu kuwa ni kisiwa na kuwepo kwa bandari nyingi ambazo sio rasmi. Lakini vile vile, kuwepo kwa bahari kuu ambapo Mhe. Naibu Spika, inasemekana hata tuliona katika kesi moja ambayo yalikamatwa madawa katika bahari kubwa, maboti na mameli yanakuja huko na yanashusha katika viboti vidogo vidogo.

Mhe. Naibu Spika, vikosi vyetu bado havina vyombo vya kutosha kuweza kufanya *patrol* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba dawa hizo hazishushi na kuingizwa ndani ya visiwa vyetu. Hata hivi karibuni tena, nje ya maji tu, maji makuu ya Tanzania kumekamatwa tena mzigo mwengine ukiwa nao uko katika hatua za kusafirishwa.

Kwa hivyo, hili suala kidogo ni zito na ni gumu na ni tofauti tunavyoliangalia kama kupiga marufuku magendo ya karafuu na serikali imeweza mara moja. Serikali haikukaa tuli. Katika jitihada hizi Mhe. Naibu Spika, mara baada ya kuanza awamu hii tuliona kwamba sheria ya dawa za kulevya ina mapungufu makubwa na inatoa mwanya kwa wahalifu wasafirishaji wa dawa za kulevya
kuweza kutoka. Tumeifanyia marekebisho na hivi sasa Mhe. Naibu Spika, katika sheria ya zamani kama ulikamatwa na kosa la kusafirisha dawa za kulevya ulikuwa unaweza kupewa dhamana.

Mhe. Naibu Spika, sheria tumeirekebisha na sasa kama umekamatwa na kosa la kusafirisha dawa za kulevya, dhamana haipo kabisa katika suala hili. Kwa hivyo, tumeifanyia marekebisho vipengele hivyo, lakini pia na vipengele vyengine, kiwango chenyewe anachokamatwa nacho mtu, labda kwa kusema kwa matumizi ya dawa au kwa matumizi ya *abuse* unga wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, hatua nyengine ambayo serikali imechukua ni kuandaa *road map*. Nini *road map*. Mhe. Naibu Spika, tulikaa kama serikali tukaona suala hili lenye wadau wengi, ni lazima wakutanishwe wote kwa pamoja, walikutanishwa vyombo vya ulinzi na usalama ikiwemo Polisi, wadau wa Mahakama, Ofisi ya *DPP*, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, watu wa *Customs*, watu wa bandari, watu wa *airport*, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na wengine ambao tuliona kwa aina moja au nyengine wanaguswa na suala hili walikutanishwa kwa pamoja na kuweza ku-*way forward*, nini kifanyike ili tupate nafuu dawa hizi zisiwe zinaingizwa ili na vijana wetu wawe salama.

Mimi ninakubaliana na wengi kwamba tukipita njiani tunawaona wengi maskini ndugu zetu tayari wamekuwa wagonjwa; mimi ninawaita wagonjwa na kwa kweli kimataifa sasa hivi wale sheria yoyote inawakamata ni wahalifu kwa sababu wanatumia dawa, lakini wale ni wagonjwa wanahitaji tiba na ndio kuwepo kwa hizi *rehab centres* na *sober houses* ambapo kama wapo tayari wale kuacha inakuwa kidogo tunaweza kuwasaidia.

Lengo la serikali ni kuzuia kwa kiasi kikubwa unga usiingie na imani yetu kwamba utakupokuwa haujaingia, basi hata hawa wanaovuta mapusha hawa wadogo wadogo wanaouza nao, watakuwa hawaupati na vijana wetu na nchi yetu itakuwa salama.

Hata hivyo, hawa wanaovuta unga nao sio kwamba tumewaachia, wao kisheria ni wahalifu na wanakamatwa na wanashughulikiwa vile vile. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kwa kuona pia mambo haya ni ya kimataifa kwa sasa hivi serikali inashirikiana moja kwa moja na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusiana na mambo ya uhalifu na mambo ya dawa kulevya.

Kuna mashirikiano ya karibu na kupitia wao tunapata elimu na tunategemea pia kupata mawazo mapya na pia kusaidiwa vifaa kama tutakubaliana huko mbele, kama uwezo utakuwepo tumepeleka *proposals* zetu za kusaidiwa ili kuweza kutusaidia katika mapambano hayo, lakini vile vile, kuwapatia *training* watu wetu waliopo katika sekta mbali mbali ambao wanaguswa kwa aina moja au nyengine, lakini suala hili zima la usafirishwaji na matumizi ya dawa za kulevya.

Mhe. Naibu Spika, naomba tu Wajumbe watuamini kwamba serikali hailipendi wala hailifumbii macho, lakini kuna tatizo moja naomba nilieleze na wenzetu watusikie wadau wengine; nao ni vyombo vya ulinzi na usalama, Polisi na Mahakama. Kwa kweli tunahitaji watu hawa wawe waadilifu, lakini vile vile, hata sehemu zetu za bandari na uwanja wa ndege, kwa sababu hizo ndio njia pia zinatumika.

Kama juzi tumesikia hivi sasa Waziri anayekaimu Ofisi ya Makamu wa Pili, akitueleza juu ya kadhia ile ya kukamatwa kwa mabegi pale. Sasa unakuwa unajiuliza yale yalionekana, lakini pengine mangapi yamepita bila ya kuonekana. Kwa hivyo, tunahitaji uadilifu kwa watu wetu wote wanaofanya kazi kwa madhumuni ya kuwa-*save* vijana wetu, kwa madhumuni ya kuipenda nchi yetu.

Mahakama nayo iwe adilifu, lakini mmoja anayehusika na suala hili awe muadilifu. Ofisi ya Mkemia Mkuu nayo iwe muadilifu isiwe tunafika wakati unapeleka unga unaambiwa ilikuwa ni saruji sio unga. Kwa hivyo, haya yote yalizungumzwa katika kikao cha pamoja kwa madhumuni ya kuweza kupunguza tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, nia ya serikali ni njema na tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe watuunge mkono katika vita hivi kwani vinaathiri jamii nzima, karibu wote tuliomo humu kama si mtoto, basi ndugu yake mtu ameathirika na dawa hizi. Kwa hivyo, tumuombe Mwenyezi Mungu atusaidie, lakini kwa jitihada za pamoja vile vile kuweza kushirikiana katika vita hivi.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo limeelezwa pia na hili sasa la Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Alieleza lini tutahakikisha kwamba miradi yote ambayo inapitia *ZIPA* haipatiwi *certificate* ya kuanza kufanya mradi huo bila ya kufanyiwa tathmini za athari za kimazingira. Nilieleza asubuhi, lakini ninarudia kusema tena kwamba mahusiano ya karibu na mashirikiano kati ya *ZIPA*, Kamisheni ya Utalii, Idara ya Misitu, Idara ya Mawasiliano, Idara ya Mipango Miji na Vijiji, Idara ya Ardhi na Wilaya, Halmashauri hizo mbali mbali, sasa yameimarishwa na nia kwamba yataweza kutusaidia.

Lakini vile vile, sheria mpya ya mazingira ambayo tutaileta hapa yamezingatia mapungufu yaliyokuwepo na hili nalo lina ufumbuzi wake katika sheria hiyo mpya ambayo tutakuja nayo.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo Mhe. Ismail Jussa Ladhu, amelieleza na mimi ninakubaliana naye kwamba ni kweli usafi wa miji yetu haujawa katika kiwango cha kuridhisha kabisa. Ingawa kuna juhudi mbali mbali zinaendelea kuchukuliwa na taasisi mbali mbali zinazohusika.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais mara kwa mara imekuwa inatoa amri na matamko ya kuzuia kutupa taka taka ovyo katika maeneo yanayoleta athari na mazingira katika jamii vile vile. Amri hizo pia zinatolewa kwa Manispaa na hata Halmashauri nyengine zozote husika na kuweza kuwaelekeza jinsi gani ya kuweza kuweka mji safi na kutafuta maeneo ambayo yatakuwa muafaka kwa ajili ya utupaji wa taka.

Aidha Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais hivi sasa imo katika hatua ya kutayarisha mkakati wa taifa wa usimamizi wa taka taka ambao utafuatwa na Halmashauri zetu na ni imani yangu kwamba Halmashauri zitashirikiana na ofisi yangu katika kuhakikisha kwamba mkakati huo unafikiwa. Vile vile, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais hushiriki katika kuhamasisha jamii kwenye shughuli za usafi na mazingira katika maeneo yao, lakini vile vile, kwa kutoa elimu katika makundi mbali mbali ya jamii.

Mhe. Naibu Spika, naona mengi ambayo yameelezwa hapa nimejaribu kuyatolea majibu kama alivyosema mwenzangu pengine mengine yamo katika maagizo ya kamati ya 2013/2014 ambayo tutakuja kutoa maelezo zaidi. Niwashukuru sana Wajumbe ambao wamepata nafasi ya kuchangia na kuikubali ripoti yangu ambayo nimeiwasilisha hapa na niendelee kuwaomba kwamba wazidi kutupa mashirikiano na sisi tupo kwa ajili ya kusikiliza ushauri na maoni yao ili ufanisi wa taasisi zetu uwe bora zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena naomba nikushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kusimama mbele ya Baraza lako hili tukufu kuweza kutoa ufafanuzi kwa Waheshimiwa mbali mbali ambao waliochangia ripoti hii ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, ninadhani kama ulivyoona kwamba ripoti hii ya Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ina maeneo mapana sana hasa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Na kwa kuwa Wajumbe wengi hawakuweza kuichangia.

Kwa hivyo, inaonesha yale majawabu ambayo yaliyotolewa mwanzo Waheshimiwa Wajumbe kwa kweli waliweza kuridhika na utendaji wa serikali.

Kwa hivyo, tunaishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi kubwa na nzuri ambayo waliyoifanya na ndio maana hata michango ya Wajumbe haikuwa mengi sana. Kwa hivyo, vile vile, sio Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tu, lakini hata Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Utawala Bora, na vile vile Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kwa kiasi fulani kwa kweli ripoti za mwaka uliopita, kwa kweli zimeonesha ufanisi mkubwa hasa katika utekelezaji wa mambo mengi ambayo kamati yangu iliweza kuagiza. Sasa nitajaribu tu kuzungumza machache ambayo yaliyojitokeza katika michango ya Wajumbe ili baadae niweze kuhitimisha, niwape nafasi Waheshimiwa Mawaziri waende wakayafanyie kazi yale ambayo yaliyojitokeza katika ripoti ya mwaka huu.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe ambao waliopata kuchangia ripoti yetu hii, ni:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2.Mhe. Hija Hassan Hija
3.Mhe. Subeit Khamis Faki
4.Mhe. Salmin Awadh Salmin
5.Mhe. Ismail Jussa Ladhu

Lakini kwa Waheshimiwa Mawaziri ambao waliochangia ripoti yetu hii Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora, lakini vile vile, Kaimu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Haji Omar Kheir, pia akamalizia Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kimsingi ripoti yetu Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mambo mengi ambayo tuliyoyazungumza katika ripoti hii ni mengi ambayo yali-*reflect* katika ripoti ya mwaka uliopita. Kwa hivyo, mengi ambayo tumejaribu kuyashauri vile vile yalikwisha kutolewa majibu na serikali.

Sasa labda tu nianze mambo machache ambayo yaliyozungumzwa na nitaanza lile ambalo alililozungumza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, lakini vile vile, Mhe. Salmin Awadh Salmin na Mhe. Ismail Jussa Ladhu pia wamelirejea. Lakini hata Mawaziri mawili Mhe. Omar Haji Kheir na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, wamelizungumzia suala hili la kadhia ya madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika, lazima tukubali hivi vita vya madawa ya kulevya, hivi vita sawa sawa na mapambano dhidi ya Ukimwi. Kwa kweli tunatakiwa kila mtu lazima ashiriki katika mapambano haya, tukisema tumuachie Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa kweli hili suala tutakuwa tunamtupia zigo na kwa kweli hatoliweza.

Sasa mimi ninashauri sana serikali yetu, lakini vile vile, ninaishauri zaidi serikali kutusikiliza zaidi hapa tunapotoa maoni katika kamati. Mhe. Naibu Spika, tulijaribu kuzungumza katika vikao vilivyopita, hasa ilikuwa kwenye bajeti ya serikali. Leo limezungumzwa suala la madawa ya kulevya, kilo 30 zilizopatikana katika uwanja wa ndege wa Zanzibar hivi majuzi. Madawa yale mpaka leo anaambiwa mwenyewe hajulikani.

Lakini tunashukuru taarifa ya Mhe. Waziri, pale na ninamuomba sana Mhe. Waziri, pamoja na kwamba umekaimu hii nafasi, lakini huu mzigo ninataka Mhe. Waziri, mwenye wizara husika akija ushirikiane naye katika kuhakikisha alau tunaanza kukamata, alau tupate pa kuanzia.

Lakini Mhe. Naibu Spika, leo hili lina nyanja nyingi, kwanza tuulize kilo 30 tumeshazoea askari wetu kukamata sijui kete ngapi mtaa wa Kwahani, Jang'ombe, Kwamtipura. Lakini leo kilo 30, mabunda yaliyokuwepo pale.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi ninataka nizungumze kwamba sasa hivi Tanzania Bara imekuwa ni kituo cha madawa ya kulevya. Na inatumika sana Tanzania Bara kuondoshea madawa ya kulevya kusafirishia nchi za nje. Tumeshashuhudia katika hiki kipindi kifupi Uwanja wa Ndege wa Dar-es-Salaam madawa mengi yanakamatwa ambayo yanapelekwa Afrika ya Kusini.

Sasa leo tumejaribu kulizungumza sana hili na hili ninaliomba sana serikali ijaribu zaidi kuliangalia. Leo kuna wafanyakazi hapa Zanzibar ambao ni wawekezaji katika sekta ya usafirishaji, wameanzisha utaratibu wa kupakiwa mizigo katika vyombo vya usafiri, ikishafika hapa Zanzibar mizigo ile baada ya kuachiwa wenye mizigo wakaiteremsha, makampuni yale yale yanachukua tena usafiri yanampelekea mtu mpaka dukani au nyumbani kwake.

Mhe. Naibu Spika, hii ni moja katika sehemu ya kusafirishia hayo madawa ya kulevya na inawezekana pengine hizo kilo 30 zilikuja katika njia hiyo. Leo pale mzigo ukishafika katika meli, yanakuja magari ya mwenye meli ile ile, anapakia na kuyaleta mitaani, tunajua kuna kitu gani ambacho kilichopelekwa, inawezekana kwamba yeye hakuhusika moja kwa moja, lakini wale wahalifu wamekwishaona sasa hivi Zanzibar kuna njia ya mkato,

kwamba unaweza kupakia madawa yako Magomeni, ambapo sasa hivi ndio kituo kikubwa yanaposafirishwa madawa, ukaja zako mpaka bandarini ukisha unamkabidhi mfanyabiashara fulani mkubwa hawezi kuhojiwa na huku ana magari yake anakupelekea mpaka kwako.

Mwenyezi Mungu atuepushie mbali. Tunaweza kukuta mapolo yale yametoka Dar-es-Salaam yakapakiwa kwenye meli, yakajakuteremshwa chini ya nyumba ya kiongozi fulani. Mwenyezi Mungu atuepushie mbali yasijekuteremshwa chini ya nyumba yangu. Hii ni hatari, mzigo unapofika bandarini ni lazima ufanyiwe uhakiki.

Sio leo mtu anapakia mzigo huku halafu anautia kwenye meli yake, anaupeleka mpaka dukani au kwake, tumeona wapi. Mhe. Naibu Spika, leo kilo 30 zimepatikana uwanja wa ndege, kesho zitakuja kilo 50 hapo nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, keshokutwa tunazindua nyumba ya Spika, anaweza kuwekewa chini ya mlango, itakuwa ni sawa sawa na zigo la mwizi kama lililotupwa uwanja wa ndege hajulikani mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, haya tunayozungumza mtaona kama ni masihara, lakini kwa kweli hizo ni moja katika njia za kurahisishia. Maana yake mtu mwenye madawa ya kulevya akimpata mtu wa kumsafirishia, *Wallah* halibebi. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, suala hili nilikuwa najaribu kulizungumzia sana, kwa sababu Dar-es-Salaam hivi sasa imekuwa ni kituo kikubwa sana cha kusafirishia madawa ya kulevya kwenda Afrika ya Kusini na nchi nyengine. Sasa leo ni hapa kwenye uwanja wa ndege wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka niwapongeze wale walioanza kuyaona, kwa sababu yale yasingekamatwa kama hayakuonekana. Ile ngoma mimi najua sio ya mwanzo, ile imebaunzi tu, maneno ya watoto wa mjini. Ile kwa kweli imebaunzi, mtu kakosea *step* ngoma kaiwacha. Lakini kama alivyosema Mhe. Waziri, hatujui kilo ngapi tayari zimekwishapita katika utaratibu huu.

Mhe. Naibu Spika, ndio maana nikasema hii vita iwe kama ni mapambano dhidi ya Ukimwi, tushirikiane sote. Hoja aliyoizungumza Mhe. Salmin Awadh Salmin, pamoja na kwamba Mhe. Kaimu Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kaijibu katika lugha nyepesi, ninaamini lugha ile nyepesi na yeye kapewa vile vile. Mhe. Naibu Spika, naomba hili kwa huyu askari aliyeonesha uwadilifu akataka kumsachi mtu mkubwa sana katika nchi hii, akakataa kusachiwa, baadae akakubali, akamwambia wewe kama hutaki kazi, basi nitakuonesha. Je, vita hii askari mwengine pale uwanja wa ndege ataweza kumpekua mtu huyu.

Kwa hivyo, mimi nashauri, hatuingilii majukumu ya kazi, lakini tunaomba askari yule aliyempekua huyo mkubwa baadae akaondolewa kituoni arejeshwe, ili aendelee kufanyakazi yake na atusaidie katika mapambano dhidi ya madawa ya kulevya. Vinginevyo Mhe. Naibu Spika, hawa ndio tutakuwa tunawapa vichwa, hawa matajiri Mhe. Naibu Spika, wana matatizo, tunawapenda, lakini wana matatizo yao. Wao waache waendelee kumiliki makampuni yao, waendelee kuwa na utajiri wao, lakini kwa kuwa bendera tunayo sisi, basi askari wetu waachiwe wafanyekazi.

Mhe. Naibu Spika, leo haiwezekani mfanyabiashara atowe amri ili askari abadilishwe kwenye kituo. Mhe. Naibu Spika, hiki kitu kwa kweli hakikubaliki, na naiomba sana serikali. Hatuingilii majukumu ya upangaji wa kazi, lakini matukio ya mazingira yaliyotokezea, haya ndio yanayosababisha askari wetu ambao wanajitolea muhanga kupambana na madawa ya kulevya, wanavunjika moyo katika hali kama hiyo.

Mhe. Naibu Spika, suala hili nilitaka kulizungumza kwa nguvu kubwa, ili tuoneshe na sisi kwamba wale wote ambao wako tayari kupambana na mtu yeyote ambaye anataka kuvunja sheria za nchi hii, basi sheria ichukuwe mkono wake. Lakini hao ndugu zetu au askari wetu wasiweze kuadhibiwa au wasichukuliwe hatua za kutishwa tishwa.

Mhe. Naibu Spika, suala la *echo* ya Baraza nafikiri hili suala limeshazungumzwa sana na nadhani Mhe. Waziri, hili nitaomba tena uondoke nalo ili uweze kulifanyia kazi, ingawa umezungumza kuwa utalifanyia kazi, suala hili kwa kweli linatusumbua sana.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni suala la udhalilishaji wa hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Nadhani maelekezo yako Mhe. Kaimu Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, nafikiri umeshamuachia Mhe. Naibu Spika, juu ya meza yake tuangalie kanuni zetu ili lifanyiwe kazi. Tukiendelea kulirejea hili, basi itakuwa ni sawa sawa tunakiuka kanuni zetu kwa kurejea. Kwa hivyo, mimi naomba hatua zichukuliwe ili nidhamu iendelee kurejea ndani ya serikali na pia kwa Waheshimiwa Wajumbe.

Jengine ambalo alilizungumza Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, alilizungunza na Mhe. Kaimu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kuhusu suala la elimu ya katiba na mafunzo. Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani wakati umefika kama Wazanzibar maoni yao tumeshayasikia, kila mmoja lisema alivyokua anahisi yeye. Sasa kitu ambacho kimebakia ni *conclusion*, yaani kufanya *summary* kwa yale mambo ambayo Wazanzibari wengi waliyachangia, ni kitu gani ambacho wanakihitaji.

Mhe. Naibu Spika, katika rasimu ile ya katiba kuna mambo mengi sana ambayo wananchi, hata wale ambao wanatofautiana lugha zao za kisiasa, lakini mambo yale walikuwa wanayarejea kama ndio nyimbo yao. Kwa hivyo, kuna baadhi ya mambo mengi walikuwa tayari wamekubaliana na kuna baadhi waliyotofautiana, watatubakishia sisi kama wanasiasa, naamini tutafika pahala tutayaweka pahala pazuri.

Mhe. Naibu Spika, kitu ambacho mimi ninakiomba, kama alivyosema Mhe. Waziri, hiyo semina ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Zanzibar, vile vile na Wabunge wa Zanzibar watakaokwenda katika Bunge la Katiba, Mhe. Naibu Spika, ni lazima tupate muda tutathmini, tujadili na hizo tofauti zikijitokeza hapo ndio itakuwa njia rahisi ya kuweza kuzirekebisha, kuliko tofauti hizi Mhe. Naibu Spika, tukenda tukaonekana kule katika Bunge la Katiba, tunakwenda kuanza kubishana wenyewe kwa wenyewe.

Tukiangalia Mhe. Naibu Spika, Bunge la Katiba hawatoki Wabunge wa CUF au Wawakilishi wa CUF na Wawakilishi wa CCM, zikaangaliwa je wapi wengi, wa CCM walisema hivi wa Zanzibar na wapi wengi wa CUF, walisema hivi kwa upande wa Zanzibar. Tukienda kule tukishaingia tu kwenye boti sote tunaitwa Wajumbe wa Bunge la Katiba kutoka Zanzibar na kule hakuna waziri wala hakuna mtu yeyote, kule sote tunakuwa jora moja.

Kwa hivyo, sasa kama uwaziri tunauwacha bandarini, kama uchama tunauwacha bandarini, kule tunakwenda Wabunge wa Bunge maalum la Katiba. Ndio maana kule hata sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutaitwa Wabunge wa Bunge maalum la Katiba, hata hao wanakuja sijui 62, basi wataitwa Wabunge maalum wa Bunge la Katiba. Sasa je, tunapokwenda kule tukaanza kwenda kubishana. Mhe. Ismail Jussa Ladhu,kasimama anasema lake, Mhe. Hamza Hassan Juma, kasimama anasema lake na Mhe. Asha Bakari Makame na yeye vijembe vyake, vijembe kwenye Bunge la Katiba havitokwenda kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kwamba serikali yetu wanasema kwamba serikali haina msimamo, lakini bado tukirudi katika kumbukumbu zetu, Serikali ya Zanzibar ina *documents* nyingi ambazo iliomba marekebisho mbali mbali kabla hata hii zana ya Bunge la Katiba. Basi hata yale hatuwezi tukapewa tukaambiwa serikali ya Zanzibar ilitaka kirekebishwe hiki na hiki, wala haikuingia katika mfumo, basi hata yale tuweze kuyajua.

Vyenginevyo Mhe. Naibu Spika, itakujakuwa vita vya panzi neema ya kunguru, baada ya haya tunayoyapigia kelele, basi yatakuja kuzidi na wakati huo tukishakumaliza Bunge la Katiba, basi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, atakuwa anazungusha kiti pale pyaaa; kwa sababu yale tuliyokuwa

tunamuhoji hapa kama yeye ni mratibu wa shughuli za Muungano, atasema si ndio mshaamua sasa na yeye tutamuhoji nini hapo. Tutakuja kuwa hatuna mtu wa kumlaumu na wakulaumiwa tutakuwa sisi wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kwanza itabidi tupate muongozo, je, katika Bunge la Katiba kutakuwa kuna kula kiapo kule, maana yake hapa tulipokuja katika Baraza na Bunge la Jamhuri ya Muungano tunakamatishwa msahafu. Je, kule, sasa hayo pia hatuyajui. Kwa hivyo, masuala kama hayo ni lazima yapate maandalizi, watu wajuwe kuna nini, kutakuwa na nini.

Vile vile, kuna kanuni, je, kule tunatakiwa tukazungumze dakika ngapi, hatujui. Leo msahafu ule, *Astaghfirullah Laadhim*, lile rasimu la Dk. Warioba ukaambiwa ukachangie kwa dakika tano, basi yatakuwa yale aliyoyaandika yeye, basi yatakuwa ndio yale, huna namna ya kuyarekebisha.

Kwa sababu kifungu Mhe. Naibu Spika, unatakiwa unataja bwana Warioba kasema hivi na mimi kwa maoni yangu nasema hivi, halafu unachambua. Leo rasimu lile ukipewa dakika tano halafu hakuna maandalizi yoyote *Wallah* litakuja kurudi vile vile. Sasa mimi naogopa wananchi wasije wakatuhukumu vibaya. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana ni lazima tuwe na kikao cha pamoja.

Mhe. Naibu Spika, jengine katika hili hili, leo sisi angalau tuna a, b, c, d katika vyombo vya kutunga sheria. Lakini je, hao wabunge maalum 62 kutoka Zanzibar angalau wana a, b, c, d ya kuweza kuchangia masuala ya katiba. Sasa ni lazima tupate maelezo hapa kidogo itakuwa vipi, ili baadae tujuwe mambo yatakuja kwenda vipi. Mhe. Naibu Spika, katika hili nilikuwa nina mengi, lakini nitakuja kuzungumza katika hiyo siku ambayo Mhe. Waziri, kama alivyosema ataiandaa, ili tupate ufafanuzi wa kutosha na tuweze kwenda kuwakilisha wananchi wa Zanzibar, kwa lengo moja la kuweza kuboresha na kubadilisha maisha ya watu wa Zanzibar, lakini vile vile, na wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea Mhe. Subeit Khams Faki, alizungumzia kadhia ya Ikulu ya Micheweni. Mimi nafikiri Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais,ameyaeleza vizuri na kwa bahati nzuri alisema kwamba wameingiza ndani ya bajeti ya mwaka huu, lakini sasa naona niko *quarter* ya pili na bajeti inakaribia.

Je, kweli hizi fedha wataweza kuzihifadhi ili ziweze kutumika kule, kwa sababu mimi kamati yangu katika mzunguko wa mwisho kabla ya kuja katika bajeti, nitataka kuona, kwa sababu tumeona kuna mapungufu katika uingizaji wa *OC*, lakini huku tayari kuna fedha zimeshatengwa. Sasa kama

itakuwa mkandarasi atakuwa hayuko tayari, basi fedha hizi ziangaliwe na zitumike katika maeneo mengine ili haya mapungufu yaliyokuwepo mengine katika idara nyengine yaweze kufanya kazi. Lakini sisi tunavutiwa zaidi tukiona hii Ikulu ya Micheweni ikiwa inafanyiwa kazi.

Vile vile, Mhe. Subeit Khamis Faki, alizungumzia suala la mazingira. Mhe. Waziri, ameshajibu sina haja ya kurejea. Mabadiliko ya tabia ya nchi sina haja ya kurejea. Lakini suala alilozungumza Mhe. Salmin Awadh Salmin, ambapo Mhe. Ismail Jussa Ladhu, aliligusia pia katika ripoti yetu suala la Muwekezaji wa Hoteli ya *Cristal.*

Mhe. Naibu Spika, sisi tunasikitika sana, mwekezaji huyu sio kuwadhalilisha wananchi tu, mpaka Waheshimiwa Wawakilishi ameshawadhalilisha na mpaka Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ameshadhalilishwa, mpaka aliyekuwa mjumbe wangu wa kamati ambaye ni Mwenyekiti wetu wa Baraza Mhe. Mgeni Hassan Juma, ameshadhalilishwa, Mkurugenzi wa Idara ya Ardhi ameshadhalilishwa na mwekezaji huyu huyu na maneno yake ndio yale yale kwamba ameiweka mkononi serikali, naamini, tutu imepata mwenyewe, kama alivyosema mwenyewe.

Kwa kuwa sasa hivi hii Idara ya Tawala za Mikoa ambapo moja kwa moja iligusiwa, mimi naamini Mhe. Haji Omar Kheir ni mtendaji mzuri, akiamua kufanya lake, basi atafanya na hili itakuwa sio lake, hili ni letu.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini tukikaa pamoja, nashukuru tulipotoka pale Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ulininong'oneza akaniambia utawaagiza mawaziri ili walifanyie kazi suala hili. Naamini suala hili tukenda na mawaziri wahusika, tukilifanyia kazi, basi ndani ya wiki moja suala hili litakuwa limepatiwa ufumbuzi na yule mwekezaji atafanya shughuli zake na wananchi wataweza kufanya shughuli zao. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, tukienda katika mpango kama huu, basi mimi naamini wananchi wetu wataridhika na utendaji wa chombo chetu hiki cha kutunga sheria.

Mhe. Naibu Spika, suala la uvamizi wa Jeshi la Polisi kwa nyumba ya mwananchi wa Jimbo la Magomeni, kwa kweli Mhe. Naibu Spika, hata mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati nasikitika sana. Katika duru ya pili tutakapozungumza na Kamishna tutajaribu kumpa maelekezo ya ziada. Lakini kwa kuwa serikali ipo na imeshalisikia hili, naamini litaweza kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza askari hana sheria ya kumpiga mtu, askari anatakiwa kama pahala pana fujo, basi yeye aende akatulize fujo. Kama kuna mwananchi anatakiwa kituoni, inavyotakiwa anapelekewa tu barua, basi

mwananchi anakwenda mwenyewe. Sasa leo inapofika pahala kwamba askari wanaingia katika nyumba ukumbini wanawapiga watu na starehe zao, kwa kweli hili ni jambo la kusikitisha sana na naiomba serikali ilichukulie hatua za kinidhamu, hasa kwa hawa askari ambao inaonesha kidogo wanataka kuiharibia sifa Jeshi la Polisi, lakini pia wananchi.

Askari polisi Mhe. Naibu Spika, wanatakiwa ndio kimbilio la wananchi, sasa isifike pahala leo mwananchi akimuona polisi aanze kufunga milango, sasa akija jambazi je, atafungua milango, kama askari atafunga milango na je, akija jambazi atafanya kitu gani.

Kwa hivyo, kadhia hii kwanza tunakupa pole sana Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa wananchi wako kupata kadhia kama hii, lakini naamini na serikali imeshasikia itaweza kulifanyia kazi kama inavyostahili. Hali ya usalama wa nchi kama alivyosema Mhe. Salmin Awadh Salmin. Ni kweli hilo kundi tumelisikia, limeanza kujitokeza na lina silaha. Kwa hivyo, ni lazima tutafute utaratibu za kujua hizi silaha waliingia nazo kwa kupitia wapi.

Mhe. Naibu Spika, huu utaratibu wa kuingia vitu nchini una mambo mengi, nilizungumza suala la madawa ya kulevya. Inawezekana hata hizo silaha walipewa watu wakazisafirisha na vyombo vyao, halafu baadae wakaja watu wakapelekewa majumbani kwao. Kwa hivyo, hizi silaha vile vile tunaomba sana Jeshi la Polisi kwa kupitia serikali liweze kufanyiwa kazi. Suala la *Echo* nafikiri limeshazungumzwa. Suala la madawa ya kulevya, Mhe. Salmin Awadha Salmin, nafikiri nimeshalizungumza. Suala la mazingira Mhe. Waziri, amejibu vizuri.

Mhe. Naibu Spika, namalizia suala la Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Suala la mwekezaji wa Hoteli ya *Cristal* nafikiri tumeshalizungumza, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, atatowa maelekezo, lakini Mhe. Waziri, ameshalizungumza. Suala la *Diaspora* alizungumza Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Mimi namshukuru sana Mhe. Waziri, kwa kutoa maelezo, lakini bado na mimi kama Mwenyekiti wa Kamati, naomba kitengo hiki cha *Diaspora*, bado hakijatengewa fungu la kuwafuata hao Wazanzibari ambao tunawataka. Mhe. Naibu Spika, sisi tunajua Wazanzibari wako dunia nzima, lakini kuna maeneo ndio kuna ile *dumpor* hasa ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilipata bahati na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, tulipokwenda Marekani Siyato, wale Wazanzibari kule wamefurahi na wamesema ni kiongozi wa mwanzo katika ripoti yao wanamueleza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Sasa Mheshimiwa wewe ndio waziri wa *Diaspora* sasa hivi, wako wengine na safari hii, hebu tengeneza mazingira

tukutengenezee fungu zuri ili uende ukawatafute hawa, wako wengi na hawa utakapokwenda kuna mambo ambayo wataisaidia Zanzibar, lakini kuna mambo ambayo ukawaelekeze ili uwasaidie na wao.

Kuna Wazanzibari wengine wako kule hohe hahe, tena tunawaambia jamani simfanye tena mrudi, mpaka *passport* wameuza wengine, hata cha kurudia huku hawana.Kwa kweli wanasikitisha, Mhe. Balozi machozi yalitaka kumtoka. Kuna Wazanzibari badala ya wao waisaidie Zanzibar, basi kuna Wazanzibari kule ambao wanahitaji kusaidiwa angalau wawe na utaratibu mzuri.

Vile vile, kitu ambacho tumekiona wanahitaji elimu, tumekwenda pale Siyato kuna ile *Chamber of Commerce* ya Afrika ambapo kuna Waethiopia, Waganda, Wakenya na nchi za Afrika ya Magharibi, hakuna hata Mzanzibari mmoja au Mtanzania aliyekuwemo katika ile *Chamber of Commerce* ya Afrika na ile *chamber* inafanya nini, inawaunganisha wafanyabiashara wa nchi za Afrika na wale wafanyabiashara wakubwa wa Marekani, tena Marekani kuna soko kubwa sana la bidhaa, hata Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, nafikiri hayupo hapa, lakini wale *Cospo* walisema vipi, karafuu kama itakuwa katika ile *brand* yenyewe hasa kwa masharti maalum wakikubaliana na *ZSTC*, basi watafunga mkataba na *ZSTC* haitouza karafuu popote, watainunua wao na katika bei ambayo itakuwa ni nzuri.

Tena wanasema kama watakubaliana na *ZSTC*, basi wataweza kuwafahamisha namna gani ya ulimaji bora, *packing* bora, lakini vile vile, watatoa misaada kwa wakulima wa zao la karafuu, ambapo kazi hiyo tayari wameifanya Uganda kwa wakulima wa kahawa.

Mhe. Naibu Spika, wakulima wa kahawa kule wameshirikiana na *Cospo*, wafanyabiashara kule Marekani wao ndio wauzaji wakubwa dunia nzima wa kahawa. Kwa hivyo, wao wanainunua kahawa ya Uganda, lakini vile vile, wanatoa misaada na mikopo na kuwasomesha wale wakulima namna gani ya kuweza kufanikiwa. Kwa hivyo, mimi naamini tukitumia njia hizi za kuweza kuwaelimisha watu wetu na waliahidi na wao mwakani watakuja kutembelea Zanzibar, nitaomba sana Mhe. Wazir, ukutane nao ili tuone ni namna gani na Wazanzibari wanaweza kujiunga katika zile *Diaspora*.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya nimekuja na *copy* ya *BL* pale katika hii ziara ya Marekani tuliyokwenda na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, tayari kwa jitihada za *Diaspora*, hawa vijana wetu wa Kizanzibari waliokuwepo nje, tayari zile kompyuta 250 za kuanzia walizomuahidi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, zimeshatumwa kwenye kontena, *copy* ya *BL* ile pale tunayo. Kwa hivyo, tunaandaa utaratibu sasa hivi na sio kompyuta tu, kuna vitabu

5,000 na kuna vitabu vyengine wanavikusanya. Kwa sababu waliposikia hawa viongozi wa Zanzibar wanakwenda, kwa kweli wengi walikuwa na hamu ya kuweza kutaka kutoa misaada mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, sio hao tu, kuna wengine tarehe 27 wanatoka California ambao walimualika Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lakini kutokana na *shedow* hawakuwahi kwenda. Wao watakuja Tanzania na walimtaka Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, awaalike Zanzibar ili waje kuangalia mazingira ya Zanzibar na kuangalia ni maeneo gani wataweza kutusaidia.

Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, wakija wale kutoka California, kwa sababu wao pia walitaka kuanzisha *Sister City* yaani Mji wa Zanzibar na Mji wa California. Kwa hivyo, nafikiri wewe ndio watakuwa wageni wako zaidi ili kuwakabidhi kwa Mhe. Meya, tukipata ule ushirikiano, basi tutaweza kupata pengine magari ya taka na vitu vyengine wataweza kutusaidia katika hayo mambo ya *Diaspora*.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, *Diaspora* kama ulivyosema maelezo yake ni mafupi, lakini kwa kweli kazi kubwa wameanza kufanya na sisi tutaendelea kuwapa mashirikiano. Lakini kama tulivyosema fungu la fedha bado ni dogo, Mkurugenzi yule anatakiwa apate nafasi ili aweze kuwasiliana nao katika maeneo mbali mbali.

Kwa kumalizia Mhe. Naibu Spika, suala la kadhia ya *MV* Kilimanjaro II iliyotokea hivi juzi, tunashukuru kwamba kuna kamati ambayo imeshaundwa, basi itowe taarifa mapema ili tuweze kuona namna gani serikali yetu inashughulikia masuala kama hayo. Mambo mengine ambayo alizungumza Mheshimiwa kuhusu uchafu wa mazingira, nafikiri Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ameshaeleza.

Kwa hivyo, nadhani Mhe. Naibu Spika, pamoja na kwamba Waheshimiwa Mawaziri wametoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo, lakini kama tulivyosema utaratibu wetu baada ya marekebisho ya ripoti za kamati, basi tunategemea mwakani tutaweza kuletewa kwa maandishi ili kuona hatua za utekelezaji zinakwenda vipi. Isipokuwa tu lile moja ambalo Kaimu Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, alivyoeleza kuwa Kamati Teule zikae na wizara. Najua kidogo lilimchanganya hajui, kwa sababu kama ripoti imeshaletwa tena kamati irudi vipi ikae na wizara.

Mhe. Naibu Spika, kuna ripoti ya mwanzo kabisa, ile ilikuwa ni ripoti mtambuka, ni tofauti na hizi ripoti nyengine. Hizi ripoti nyengine zilikwenda *specific*, kuna ripoti ya ardhi, kuna ripoti ya Shirika la Umeme, lakini ile ripoti ya mwanzo ilikuwa ni mtambuka, kuna mambo mengi ambayo

yalichanganya ya serikali. Tuliwahi kukaa na Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kikao kimoja, tukajaribu kumu-*highlight* yale maeneo ambayo tulihisi bado hayajafanyiwa kazi na mpaka leo hayajafanyiwa kazi, ndio maana tukaomba kwamba waziri asione tabu, akae tena na sisi.

Kwa sababu kuendelea kukaa na madukuduku ambapo kuna mambo mengine tukishauriana tu na serikali ikiyatekeleza, mimi nafikiri itakuwa haina haja kila siku kuendelea kuhoji mambo hayo kwa hayo.

Lakini masuala ambayo tunajaribu kuyazungumza zaidi na ambayo yataweza kuisaidia serikali kusimamia majukumu yake, vile vile kama kuna baadhi ya maeneo ambayo upotevu wa fedha za serikali unaendelea kutokea, basi nafikiri mianya ile iweze kuzibwa ili fedha ziingie serikalini.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wajumbe wangu wa kamati, hasa Mhe. Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu ambaye kidogo hali yake ya kiafya sio nzuri, alifanya kazi kubwa ya kuandaa ripoti hii, kwa sababu kipindi kirefu nilikuwepo safarini, lakini kwa ufanisi mkubwa ripoti yenyewe mmeiona ilikuwa haina matatizo ya aina yoyote. Kwa hivyo, tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe afueni Mhe. Makamu Mwenyekiti wangu wa kamati, ili
arudi Barazani tuendelee kushirikiana katika majukumu yetu ya kitaifa. Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache naomba kuwasilisha, ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kamaliza kufanya majumuisho Mwenyekiti. Sasa naomba Waheshimiwa Wajumbe, wale waliokubali ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2013/2014 wanyooshe mikono. Waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunawashukuru kwa ushirikiano mzuri na michango mizuri kwa wajumbe waliopata nafasi ya kuchangia, lakini naamini na wale wote waliokuwa hawakupata nafasi ya kuchangia kwa kuwa wameunga mkono, basi na wao pia wamechangia. Baada ya kumaliza hii katibu tuendelee.

Mhe. Kaimu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa mara nyengine kunipa fursa hii

ili kutoa taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya kamati kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Utumishi wa Umma. Kama tunavyoelewa Waheshimiwa Wajumbe kwamba mwenzetu yuko katika safarini kwenye matibabu. Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema na awajaalie madaktari awape uwezo wa kuweza kuirejesha afya yake, tumuombe Mwenyezi Mungu ampe afya njema ili arudi tuje tushirikiane naye katika kazi zetu za ujenzi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwasilishe utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, kuhusu Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma katika kipindi cha mwaka 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, tunaanza na Idara ya Sera na Utafiti.

Agizo namba moja
Kamati ilitaka kujua mchanganuo wa pesa zilizotumika katika kukamilisha mradi wa *e-government*, kwani zile ni kodi za wananchi. Hivyo, kuna ulazima ziwekwe bayana ili kila mwananchi ajuwe ni kiasi gani mchango wake umehusika katika mafanikio ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Utekelezaji
Wizara yetu haikuwa msimamizi mkuu wa mradi huu, bali iliyokuwa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ndio ilikuwa msimamizi mkuu. Hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naiomba kamati yako iendelee kuwasiliana na wizara ya fedha ili kupata mchanganuo mzima wa matumizi ya mradi husika.

Agizo namba pili
Kamati pia inazidi kukumbushia juu ya uanzishwaji wa Bima ya afya uharakishwe, ili wananchi hususan watumishi wa umma waweze kufaidika kama utafiti ulivyobainisha. Hili sio suala la kusubiri hasa ukizingatia maslahi ya wafanyakazi bado hayaridhishi kuweza kumfanya mtumishi kuweza kumudu mahitaji yake ipasavyo.

Utekelezaji. Hatua kadhaa zimekwisha kufikiwa katika kufanikisha suala hili ikiwemo kukamilika kwa ripoti ya utafiti wa wahusika wengine juu ya utayari wao kukamilika tathmini ya uwezekano wa uwanzishwaji wa Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar. Hatua ya sasa inayoendelea ni ya kumuajiri mtaalamu atakayesarifu Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar.

Agizo namba tatu
Kamati inapongeza kitengo cha wizara kwa kupitia idara yake ya mipango kuweza kufanikisha zoezi la kuingiza taarifa za watumishi wa umma katika

mtandao. Wizara nayo inapokea pongezi kutoka kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Agizo namba nne

Kamati inaishauri ofisi zote za serikali zikamilishe matayarisho ya matumizi ya mkonga wa taifa ili na sisi tuweze kwenda na wakati na pia kuzidisha ufanisi katika kazi. Shauri hilo tumelipokea na tayari tumeshaanza kulifanyia kazi kwa kutoa toleo lenye kumbukumbu nambari OR/KWK/01/06 VOL I/C/01 la tarehe 19/12/2013, lenye kuzitaka ofisi zote kujiandaa na matayarisho ya mkonga.

Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa.

Agizo Nambari Tano. Kamati inaendelea kusisitiza haja ya serikali kuharakisha makubaliano na Serikali ya Oman, ili tuweze kupatiwa misaada hasa ukizingatia hali ya nyaraka zetu zilivyo hivi sasa sio nzuri, kuna haja ya makusudi ya kuzifanyia matibabu na kuziweka katika mfumo wa *digital* nyaraka zote za serikali.

Mkataba wa mashirikiano juu ya uhifadhi wa nyaraka kati ya Serikali ya Zanzibar na Oman, upo katika hatua za mwisho za utekelezaji.

Agizo Namba Sita

Idara izidi kutoa mafunzo katika taasisi za serikali na hata zile za binafsi, kwani kamati imegundua hadi sasa maeneo mengi ya kuhifadhia nyaraka hayapo katika hali nzuri na usalama wa kuhifadhia kumbukumbu hizo.

Utekelezaji

Kazi ya kutoa mafunzo na maelekezo muhimu ya usimamizi ya nyaraka kwa wizara,idara, mashirika na taasisi za umma unafanyika kwa kufanya ukaguzi wa kumbukumbu, vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu na taaluma ya utumiaji wa mfumo bora wa kuhifadhi kumbukumbu.

Agizo Namba Saba

Jengo la nyaraka Pemba lililokuwepo katika hali mbaya sana, kwa hivyo tunaiomba serikali iwapatie idara hii jengo la zamani la Mkuu wa Mkoa ili shughuli za ofisi ziendelee kwa ufanisi zaidi.

Utekelezaji

Mazungumzo ya kuliomba jengo la zamani lililokuwa la Mkuu wa Mkoa yanaendelea kati ya Waziri wa Kazi na Utumishi wa Umma na Waziri anayehusika na majenzi. Kwani imeelezwa kwamba Mkuu wa Mkoa alipohama jengo hilo alilirejesha serikalini.

Agizo Namba Nane
Kamati inaomba Wizara kununua kifaa maalumu cha kudhibitiwa hewa kote Unguja na Pemba ili kiweze kuzuia unyevu wakati kinapowashwa kipoza hewa katika sehemu za kutunzia nyaraka.

Utekelezaji
Agizo hili litafanyika katika mwaka huu wa bajeti 2013/2014.

Agizo Namba Tisa
Kupatiwa usafiri ili kuweza kupunguza uzito wa kazi za kutembelea wizara zote za serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa lengo la kukusanya kumbukumbu na kuzipeleka katika Idara ya Nyaraka kwa kuhifadhiwa kitaalamu zaidi.

Utekelezaji
Shauri hili limepangiwa kutekelezwa katika mwaka huu wa bajeti wa 2014/15.

Agizo Namba Kumi
Kamati inaipongeza Idara ya Nyaraka kwa kuweza kufanya ukaguzi wa kumbukumbu katika Ofisi ya mrajis wa nyaraka Wete, Ofisi ya Wakfu Chake Chake, Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani, Hospitali ya Wete, kwa lengo la kufanya ukaguzi wa vyumba vya uwekaji kumbukumbu tuli na hai.

Utekelezaji
Pongezi hizi tunazipokea na tutazidi kuendeleza kazi hizi za ukaguzi.

Agizo Namba Kumi na Moja
Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Watumishi, Idara hii ilikuwa kamati inaishauri wizara kwa kupitia Idara yake ya mafunzo ya Wananchi kuwa ifanye tafiti ili iweze kujua hapa Zanzibar kuna upungufu wa aina gani wa wataalamu na aina gani ya mafunzo ambayo ni muhimu zaidi kwa lengo la kuongeza ufanisi. Idara ya mafunzo na maendeleo ya watumishi, tayari imeanza kuandaa rasimu ya muongozo wa tathmini ya mahitaji ya mafunzo ambapo rasimu ya awali imekamilika. Lengo la muongozo huu ni kuwa na mpango mkuu wa mafunzo ili kujua mahitaji ya wataalamu katika utumishi wa umma na kutafuta aina gani ya mafunzo ambayo ni muhimu zaidi kwa ajili ya kuongeza ufanisi serikalini.

Agizo Namba Kumi na Mbili
Kamati ilishauri idara izidishe kutafuta wahisani zaidi ili watumishi wetu wapate fursa mbali mbali za mafunzo ya juu kwa lengo la kuimarisha utendaji kazini.

Ofisi yetu kwa niaba ya Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Watumishi imepokea ushauri wa kutafuta wahisani zaidi na tayari idara imeanza kutembelea balozi mbali mbali kwa lengo la kufanikisha jukumu hilo.

Idara ya Mipango ya Rasilimali watu. Idara hii ilikuwa na agizo namba tatu. Kamati inaishauri wizara kwa kupitia taasisi yake kuangalia kwa umakini uwezo wa serikali na watumishi inaowahudumia. Kwani imegundulika kuna ofisi nyingi za serikali zina wafanyakazi wengi zaidi ya mahitaji yake. Hivyo serikali iwatumie vizuri hawa watumishi iliokuwa nao kabla ya kuongeza wengine. Kwani kuongeza idadi kubwa ya watumishi serikalini ni kuipa mzigo mkubwa serikali. Hivyo kuna haja ya kuanzisha utaratibu wa kuzikagua ofisi zetu.

Utekelezaji
Mhe. Spika, maombi ya nafasi mpya yanapowasilishwa kabla ya kukubali wizara kupitia Idara ya Mipango Rasilimali Watu inazingatia muundo wa taasisi na majukumu yanayotekelezwa na mahitaji ya wataalamu kulingana na sheria zinazoelekeza. Kwa mfano sheria ya ununuzi inataka kila taasisi ya umma kuwa na kitengo chake cha manunuzi. Aidha hivi sasa idara inapitia hali halisi ya watumishi wa umma ili kugundua uwezo wao, mahitaji halisi na ziada. Kazi hiyo itakapokamilika itasaidia sana katika upatikanaji wa watumishi kwa mujibu wa nafasi ziliopo.

Tume ya Utumishi Serikalini
Tume ya Utumishi Serikalini ilikuwa na Agizo Namba Nne kupitia Wizara.

Agizo
Kamati inaishauri Tume itoe ushirikiano mzuri kwa taasisi za serikali hasa pale zinapopeleka mahitaji ya wafanyakazi kwa lengo la kuziba nafasi au ajira mpya. Aidha Tume iharakishe kutangaza nafasi hizo na pia kuwapatia watu wenye sifa zinazofaa kwa lengo la kuongeza ufanisi kazini.

Utekelezaji
Kwa kawaida Tume ya Utumishi serikalini inatoa ushirikiano wa kutosha kwa taasisi za serikali wakati inapotekeleza majukumu yake iliyojipangia kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011. Katika utekelezaji wa jukumu la kusimamia shughuli za ajira ambazo zimethibitishwa na kupata ridhaa ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma katika mpango wa Rasilimali watu wa mwaka husika na kabla ya kuzitangaza nafasi hizo Tume hukaa na Wizara husika kutathmini sifa zinazohitajika na baada ya kutangaza na kupokea maombi ya nafasi za kazi, Tume pia hufanya usaili kwa mashirikiano na Wizara husika ili kuwapata

waajiriwa ambao wizara na taasisi inawahitaji kwa mujibu wa sifa na vigezo vilivyoainishwa.

Agizo Namba Kumi na Tano
Kamati inashauri Tume kuchukua hatua za ziada inaposimamia shughuli za ajira. Kwani hivi sasa kumejitokeza wimbi kubwa la vyeti vya udanganyifu hasa kwa wale wanafunzi wanaosoma nje ya nchi, kama vile India, Malaysia na kwengineko. Huwa wanatengeneza vyeti visivyotambulika hata huko walikotoka. Hivyo Tume izidishe jitihada zake kuhakikisha wanapambana na changamoto hiyo.

Utekelezaji
Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Nam 2 ya mwaka 2011, kifungu cha 78 kinabainisha kuwa kitengo cha GSO, ndicho chenye mamlaka ya kufanya uchunguzi. Kwa sifa za kielimu na vyeti na tabia ya muombaji wa nafasi za ajira serikalini. Hivyo Tume kwa kawaida hutoa mashirikiano makubwa na kitengo cha GSO, ili kuwabaini vijana ambao wamefanya udanganyifu katika kupata vyeti. Pale ambapo waombaji watabainika kuwa wamedanganya, basi ajira zao husitishwa mara moja.

Agizo Namba Kumi na Sita
Kamati inashauri Tume inapotangaza nafasi za kazi, sifa za ajira isiwe ni vyeti peke yake. Kwa hivi sasa kumejitokeza wimbi kubwa la ubadhirifu wa mali za serikali na wizi uliokithiri hasa kwa hizi ajira zinazolewa kwa wataalamu. Hivyo Tume ifanye kazi ya ziada kwa kushirikiana na GSO ili kupunguza tatizo hili na upoteaji wa mali za serikali.

Utekelezaji
Tume kwa kawaida kabla ya kutoa kibali cha ajira kwa muombaji wa nafasi ya kazi, tunahakikisha kuwa orodha ya waombaji wote wanaotarajiwa kuajiriwa inawasilishwa GSO kwa ajili ya uchunguzi kwa madhumuni ya kubaini vijana wenye tabia mbaya. Baada ya uchunguzi wa awali ndipo vijana hao huajiriwa wakati uchunguzi zaidi wa kitabia huwa unaendelea wakati wapo kazini.

Agizo Namba Kumi na Saba
Kamati pia iliagiza Tume ya Utumishi Serikalini ijenge tabia ya kutembelea maofisini ili kuweza kubaini jinsi gani nidhamu maofisini ilivyoshuka na watu kufanya kazi kwa mazoea bila ya kujali, haki na wajibu wao wanapokuwa kazini.

Utekelezaji
Katika mwaka wa fedha 2013/ 2014 Tume imepanga kutembelea katika Wizara na Taasisi za Serikali ili kufanya ukaguzi wa waajiriwa wapya walioajiriwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha Tume imechukua na itafanyia kazi, ushauri wa Kamati wa kutembelea maofisini na kufanya ukaguzi wa nidhamu kwa wafanyakazi.

Kamisheni ya Utumishi wa Umma
Kamisheni ilikuwa na agizo Nam. Kumi na nane,

Agizo

Uhaba wa watendaji katika kutatua hili, kamati inashauri kuwaajiri watendaji wenye sifa ili Kamisheni iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kamisheni imepata ongezeko la watumishi 17. Watumishi 4 wamehamishiwa Kamisheni kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na watumishi 13 ni waajiriwa wapya.

Agizo Namba Kumi na Tisa
Uelewa mdogo wa Sheria ya Utumishi wa Umma Nam 2 ya mwaka 2011 kwa Makamishna. Katika kufanikisha hili Kamati ilishauri kupatiwa taaluma ya sheria hii Makamishna kwa kuwa ndio kitendea kazi kikuu cha Kamisheni.

Utekelezaji
Makamishna wamepatiwa mafunzo kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011, kupitia mikutano mbali mbali iliyoandaliwa na Kamisheni juu ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Agizo Namba Ishirini
Ukosefu wa jengo la kudumu la Ofisi ya Kamisheni. Tunashauri Kamisheni ipatiwe jengo la kudumu hasa ikizingatiwa kuwa ofisi wanayofanyia kazi shughuli zao sasa ni finyu.

Utekelezaji
Kamisheni imepata jengo la kukodi ambalo ni mali ya Shirika la Bandari Zanzibar. Jengo hilo lipo Maisara, mkabala na Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Agizo Namba Ishirini na Moja
Maslahi madogo kwa Kamisheni. Kamati inashauri kupatiwa maslahi yanayostahiki Makamishna ili kulinda hadhi yao. Suala hili limepokelewa na linaendelea kushughulikiwa na Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

Agizo Namba Ishirini na Mbili
Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya watumishi. Kamati imesisitiza kuwepo kwa Mawasiliano ndani na nje ya Wizara ili wananchi wapate kuelewa mabadiliko na mwenendo mzima wa serikali.

Utekelezaji
Idara imeupokea ushauri huu na programu maalumu zitatayarishwa ili kuwaelimisha wananchi.

Agizo Namba Ishirini na Tatu
Kamati inashauri Idara hii kuvitumia vyombo vya habari kama televisheni na radio ili watumishi wazijue huduma zinazotolewa na idara husika.

Utekelezaji
Idara inaendelea kutoa uelewa kwa taasisi za serikali juu ya shughuli mbali mbali zinazofanywa na idara.

Agizo Namba Ishirini na Nne
Kamati pia ilishauri serikali kupandisha maslahi ya wafanyakazi, kila itakapoona hazina yake inaongezeka kwani watumishi hawa wote wanafanya kazi, kwa uzalendo tu. Kazi wanazozifanya hazilingani na kima cha mshahara wanachopewa, hasa ukilinganisha na ukali wa maisha uliopo hivi sasa.

Utekelezaji
Serikali imekuwa ikifanya marekebisho ya mishahara kadri ya uwezo wa Hazina unapoimarika, yakiwemo marekebisho ya mishahara ya Oktoba mwaka 2011 na Oktoba mwaka 2013.

Agizo Namba Ishirini na Tano
Kamati pia iliishauri serikali kuzuia taasisi pamoja na mashirika yote yanayotoa mishahara kiholela ambayo yanawasababisha watumishi wengine kujisikia wanyonge hasa ukizingatia kazi wanazozifanya wapo sawa lakini maslahi yametofautiana sana.

Utekelezaji
Agizo hili lilitekelezwa kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi pale alipotoa tolea maalumu lenye kumbukumbu Nam BLM/11/4/C2 la tarehe 23, Septemba 2013 lenye kuelezea kutofuatwa kwa sheria ya utumishi wa umma kuhusu uhamisho wa wafanyakazi na marekebisho ya mishahara kwa baadhi ya mishahara kwa baadhi ya mashirika na taasisi zinazojitegemea na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Agizo Namba Ishirini na Sita
Chuo cha Utawala wa Umma kilipewa agizo. Kamati iliipongeza wizara kwa kufuatilia kwa ukaribu zaidi madeni ya Wizara na taasisi zinazodaiwa na Chuo na kuzitaka taasisi hizo kuharakisha ulipaji wa madeni yao. Hii ni hatua nyengine ya maendeleo kwani pindi zinapopatikana hizo pesa ambazo chuo inazidai taasisi za serikali, zitasaidia katika mambo ya kuimarisha na kukifanya kiendelee wakati wote.

Utekelezaji
Chuo kimekuwa kikiendelea na juhudi za kufuatilia ulipaji wa ada za mafunzo mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuzifuatilia taasisi zenye madeni. Zoezi hili kwa kiasi kikubwa limepunguza wimbi la wadaiwa. Kwani katika mwaka wa fedha 2011/12 taasisi zote zilizokuwa zikidaiwa zimesawazisha madeni hayo. Jitihada hizi bado zinaendelea.

Agizo Namba Ishirini na Saba
Kamati pia ilishauri serikali kwa kupitia Ofisi ya Idara Maalumu kuweka utaratibu wa Ulinzi kwa Taasisi zote za Serikali na sio ulinzi wa kutumia virungu bali ni ulinzi wa kutumia silaha, ili wahalifu wasiweze kufanya uhalifu wao katika vyombo vya serikali.

Utekelezaji
Agizo hili limepokelewa na ushauri huu ukiwa ni pamoja na kushirikiana na wizara katika kuziomba Idara maalumu kutupatia ulinzi utakaokuwa unalindwa kwa silaha.

Agizo Namba Ishirini na Nane
Kamati pia inakipongeza chuo kwa hatua yake iliyofikia ya ujenzi. Hivi sasa imeweza kukabili lile tatizo la kuhamahama kila siku na kupelekea wanafunzi kusoma hadi muda wa usiku. Kitendo ambacho sio kizuri hasa kwa hadhi ya chuo.

Utekelezaji
Tunapokea pongezi hizi huku tukiwa tunafuatia kwa kina umalizaji wa ghorofa ya kwanza ya jengo letu la chuo liliopo huko Tunguu.

Agizo Namba Ishirini na Tisa
Kamati inashauri kuharakishwa kwa mapitio na marekebisho ya Sheria Nam. 1 ya mwaka 2007 ya Chuo cha Utawala wa Umma na kutoa mapendekezo ya msingi ili chuo kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kitaalamu zaidi.

Utekelezaji
Chuo kimeshachukua hatua za awali za marekebisho hayo ambapo rasimu ya mabadiliko hayo yanatarajiwa kujadiliwa katika kikao cha Kamati Tendaji ya Wizara kabla ya kupelekwa sehemu nyengine zinazohusika.

Agizo Namba Thalathini
Idara ya Ajira, kwa kupitia progaramu ya kazi nje nje. Kamati inapendekeza kuwa Kamati za Wilaya zihusishe masheha, Wabunge, Wawakilishi na madiwani ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa uhakika.

Utekelezaji
Wizara imelipokea agizo hili la Kamati na inaendelea kulifanyia kazi. Masheha wamekuwa wakihusishwa kwa karibu sana ingawa sio wajumbe katika kamati hizi. Katika kuendelea na utekelezaji wizara itaendelea kuwahusisha kwa karibu sana Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi na madiwani kwa ushauri. Wizara inaamini kuwa ushauri wao ni muhimu sana katika kutatua tatizo la ajira.

Agizo Namba Thalathini na Moja
Kamati imeagiza wizara kuandaa utaratibu utakaoweza kudhibiti idadi ya wafanyakazi wa kigeni wanaoingia nchini. Kwa hali ya sasa ya kuwapa uhuru mkubwa makampuni ya kigeni kuja na wafanyakazi wao inawakosesha fursa za ajira wazawa wenye sifa za kuajirika.

Utekelezaji
Katika kutekeleza agizo hili wizara imeimarisha ukaguzi kazi katika sehemu zote za kazi ili kuhakikisha kuwa wageni waliokuwepo wanafanya kazi zile zilizoruhusiwa kwa mujibu wa sheria. Aidha maelekezo ya Kamati za juu ya ada za vibali vya kazi yamefanyiwa kazi kwa mwaka huu wa fedha 2013/14 ada hizo zimeongezwa kwa asilimia 100, ili kutoa fursa pana zaidi kwa ajira kwa wazawa na vijana wetu hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Utumishi wa Umma naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:
Mhe. Naibu Spika, nataka nikushukuru kwa mara nyengine tena kunipa fursa hii kuwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala yaliyotolewa katika ripoti ya Kamati hiyo ya mwaka 2012/13.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwanza kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kuwa na afya njema na

kutuwezesha kukutana katika kikao hichi muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Vile vile, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa uongozi wenu wenye hekima, busara na uadilifu katika kuliongoza Baraza na kuliwezesha kusimamia vyema majukumu yake.

Mhe. Spika, pia natoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyekiti, na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mashirikiano makubwa wanayoipatia ofisi yetu na kwa ushauri na maelekezo yao kwetu yanayotusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/13 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ilipokea jumla ya maagizo 18 kutoka kwa Kamati ya Katiba , Sheria na Utawala, ambayo yaligusa idara na taasisi mbali mbali za ofisi hii. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ilifuatilia maagizo hayo na kuchukua hatua za utekelezaji kama ifuatavyo. Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo.

Agizo Namba Moja
Kamati ilituagiza kufungwa kwa mashine katika kisima kilichopo kwa Pweza na hali ya kisima hicho kudhibitiwa na ZAWA, kumepelekea bonde hilo kukauka. Suala la kilimo cha kutegemea mvua nalo limepitwa na wakati. Hivyo kuna haja ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kukutana ili kusaidia JKU kupata visima kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika mabonde hayo. Vyenginevyo uzalishaji katika maeneo hayo utaendelea kuwa mdogo na usioridhisha.

Utekelezaji
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na JKU tayari imewasiliana na mamlaka ya maji yaani Zawa kuhusiana na suala la kuchimba kisima chengine. Aidha wizara inaendelea na juhudi zake za kuwasiliana na taasisi nyengine husika ili kuweza kufanikisha suala hilo.

Agizo Namba Mbili
Kamati iliiagiza serikali kuhitaji kuiunga mkono wake kwa ajili ya kuiendeleza JKU, vyenginevyo lile lililokusudiwa katika uanzishwaji wa JKU litakuwa halifikiwi.

Utekelezaji
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na JKU imelisimamia suala hilo na tayari serikali imeongeza bajeti ya JKU kwa kuzingatia haja ya kukidhi dhamira ya uanzishwaji wake. JKU imerejesha mfumo uliowekwa kisheria wa kuchukua vijana na kuwalaza makambini kwa madhumuni ya kupewa mafunzo ya uaskari, uzalendo, uraia, mafunzo ya kilimo, mifugo na kazi za amali. Pia kwa kuendeleza dhamira hiyo Ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo inatarajia kuwaongezea JKU matrekta kwa ajili ya kukuza shughuli za kilimo na kukidhi azma ya uanzishwaji wake.

Agizo Namba Tatu
Kamati iliagiza Chuo cha Mafunzo kichukue jitihada ya kuwaajiri wataalamu wa Kilimo na Mifugo. Aidha Chuo hicho katika suala la mpito kinahitaji kuwapatia mafunzo ya aina hiyo askari wake ili waweze kutoa huduma kwa ufanisi.

Utekelezaji
Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Chuo cha Mafunzo kimeajiri wafanyakazi watano wenye taaluma ya Kilimo na Mifugo, ambapo wawili wapo katika ngazi ya Diploma na watatu wapo katika ngazi ya Cheti. Kuwepo kwa wataalamu hao kutasaidia kueneza taaluma hiyo na kujenga uwezo wa askari wengine.

Agizo Namba Nne
Kwa kuwa Chuo cha Mafunzo Pemba kimeahidiwa na Makao Makuu Unguja kupatiwa wanasheria wawili ni vyema mchakato huo ukaharakishwa kwa lengo la kuwasaidia watuhumiwa na wanachuo kupata huduma za kisheria.

Utekelezaji
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Chuo cha Mafunzo kimewateua wanasheria wawili ambao hivi karibuni tu wamemaliza mazoezi ya vitendo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenda Pemba. Hatua inayofuata sasa kwa wafanyakazi hao ni kuandaliwa safari ya kuelekea Pemba na kwenda kuendelea na majukumu ya kazi waliopangiwa.

Agizo Namba Tano
Kuna umuhimu mkubwa kwa serikali kutengenisha Chuo cha Mafunzo kwa watu wazima na lile la watoto kwa lengo la kuwawezesha watoto kuishi kwa amani katika vyuo hivyo.

Utekelezaji
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Chuo cha Mafunzo imeshaanza hatua za kulishughulikia suala hilo la kutenganisha watu wazima na watoto kwa upande wa Unguja na hatua kama hizo zitaendelezwa kwa upande wa Pemba haraka iwezekanavyo.

Agizo Namba Sita
Serikali ichukue jitihada za kujenga majengo ya kisasa kwa ajili ya Vyuo vya Mafunzo.

Utekelezaji
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Chuo cha Mafunzo, imechukua hatua ya ujenzi wa chuo kipya cha mafunzo cha kisasa cha Hanyegwa Mchana. Ujenzi huo umezingatia majengo ya kisasa na kitakuwa na jengo maalumu kwa ajili ya wanafunzi watoto. Aidha ukarabati wa majengo ya zamani unaendelea kwa baadhi ya vituo. Nyumba mbili za kisasa kwa ajili ya walimu katika kambi ya Hanyegwa Mchana zipo katika hatua ya mwisho ya kukamilika. Nyumba moja ya kisasa yenye uwezo wa kuchukua familia mbili imejengwa na tayari imeshahamiwa na nyumba mbili zinaendelea kukarabatiwa katika kambi ya Kangagani.

Agizo Namba Saba
Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, Kamati iliagiza kwamba kuna haja kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kukutana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (ZIPA) na Idara ya Mazingira kukisaidia kikosi hiki ili kiweze kushirikishwa katika ujenzi wa hoteli pamoja na kuwashajihisha wananchi kujenga kwa kufuata utaratibu wa Mipango miji.

Utekelezaji
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Kikosi cha Uokozi imekutana na taasisi husika kuhusiana na suala hilo. Kwa sasa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kinashirikishwa katika mipango ya ujenzi wa mahoteli ya kitalii kwa kupitia *ZIPA*. Aidha Mawasiliano yanaendelea kufanyika ili kikosi hiki kiweze kushirikishwa kikamilifu katika kamati ya *Joint Building Authority* ambayo inafanya kazi za idhini ya ujenzi.

Agizo namba Nane
Kikosi kinahitaji kupatiwa vifaa ili viweze kufanya kazi zake kwa ufanisi. Utekelezaji Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na kikosi cha Zimamoto na Uokozi, tayari imeanza jitihada za kupata magari na tayari vifaa mbali mbali vya kuzimia moto vimepatikana na kusambazwa katika vituo vyake mbali mbali vya Unguja na Pemba. Hata

hivyo juhudi mahsusi zinaendelea kufanyika ili kupata magari na vifaa katika bandari zetu za Unguja na Pemba.

Agizo namba Tisa
Mamlaka ya Uwanja wa Ndege inapaswa kulifanyia matengenezo jengo la Uwanja wa ndege ili kuondosha usumbufu kwa kikosi hiki kuvujiwa na mvua. Ofisi ya Rais na Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, tayari tumeshawasiliana na uongozi wa mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhusiana na matengenezo ya jengo la Zimamoto katika uwanja wa ndege wa Karume Pemba. Mamlaka imekubali kulifanyia matengenezo jengo hilo.

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo. Kikosi hiki kilipewa kuanzia Agizo namba 10, Kamati imeona kuna haja kwa Kikosi cha KMKM kuongezewa bajeti ya mafuta kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi zake.

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na KMKM imewasiliana na Wizara ya Fedha na tayari kikosi hicho kimeongezewa bajeti ya mafuta kwa ajili ya kazi za doria.

Agizo namba 11.
Kamati iliagiza ipo haja ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufanya jitihada za makusudi kukarabati majengo ya Vikosi vya Serikali. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa.

Utekelezaji:
Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana KMKM tayari imeanza kulitekeleza agizo hili na itaendelea kulifanyia kazi hatua kwa hatua kufuatana na uwezo wa kifedha hasa ukizingatia kwamba majengo hayo ni mengi na yapo karibu katika kila pembe ya nchi yetu.

Agizo namba 12
Kamati imeona kuwepo haja ya jitihada za makusudi kurekebishwa na kununuliwa mashine mpya za *radar* kule Sengenya iliyopo Mtambwe. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, imechukua hatua ya kuwasiliana na Wizara ya Fedha na washirika wengine wa maendeleo kwa ajili ya ununuzi wa *radar* mpya katika vituo vyote muhimu kwa Unguja na Pemba.

Agizo namba 13
Kuna haja kwa askari kupatiwa vitendea kazi ikiwemo *uniform* kwa ajili ya ufanisi wa kazi zao. Utekelezaji Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na kikosi cha KMKM na Vikosi vyengine

tayari kimepatiwa boti 5 za uokozi mpya, kwa hivyo vituo vyote vya Pemba vimeshapata boti kwa ajili ya kufanya kazi za doria. Aidha askari wote wa vikosi vya SMZ tayari hivi sasa wamepatiwa *uniform* za kufanyia kazi.

Agizo namba 14.
Kuhusu suala la hatimiliki, kamati imeshauri kupitia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kushughulikia kambi zote za Unguja na Pemba na kuweza kupatiwa hatimiliki ili kuepuka changamoto wanazozipata katika maeneo ya kambi.

Utekelezaji: Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na KMKM imeanza kulisimamia suala hilo na kwa upande wa Unguja maeneo yote ya KMKM yameshapatiwa hatimiliki isipokuwa eneo la Maisara na Tumbatu. Kwa upande wa Pemba kikosi kinaendelea na hatua ya kupima maeneo yake kwa ajili ya kupatiwa hatimiliki.

Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mamlaka hizi zilipewa agizo namba 15 kuzipatia halmashauri za Pemba watumishi wa kada ya sheria na ukusanyaji wa mapato ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuongeza mapato katika halmashauri.

Utekelezaji: Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Miji, tayari juhudi za kuzipatia watumishi wenye taaluma, halmashauri na mabaraza yote zimeanza, ambapo kwa upande wa Unguja, jumla ya wafanyakazi 15 wameajiri wakiwemo wanawake 7 na wanaume 8. Wafanyakazi hao wameajiriwa katika kada mbali mbali wakiwemo Maafisa Mapato, Afisa Utawala, Wahandisi wa Majengo, Afisa Teknohama na Maafisa Manunuzi na Maafisa Kumbukumbu.

Kwa upande wa Pemba jumla ya wafanyakazi 16 wameajiriwa wakiwemo wanawake 5 na wanaume 11, wafanyakazi hawa wameajiriwa katika kada zifuatazo. Afisa Mapato, Afisa Sheria, Afisa Mipango, wanasheria na wahandisi.

Agizo namba 16
Maafisa wa Mikoa wanahitaji kupatiwa usafiri na mafuta ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Mikoa tayari imeanzisha juhudi za kuipatia usafiri Mikoa ambapo kwa sasa mikoa minne kati ya mitano tuliyonayo imepatiwa fedha za ununuzi wa magari na tayari hatua za manunuzi zinaendelea kwa mujibu wa taratibu na sheria.

Agizo namba 17
Serikali bado izingatie kuwa na mradi wa kujenga majengo ya kisasa kwa Taasisi zake zikiwemo Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya na pia nyumba zao kwani nao wanaishi katika mazingira magumu. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Mikoa na Wilaya tayari inaendelea na juhudi za ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya.

Tayari Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja na Kusini Unguja zimejengwa upya. Kwa mkoa wa Mjini Magharibi, mipango ya ujenzi inaendelea kuratibiwa. Kaskazini Pemba jengo limekarabatiwa vizuri sambamba na la Kusini Pemba limekarabatiwa kwa kuongezwa ofisi za ziada. Taratibu zinaandaliwa za ujenzi wa nyumba za makaazi ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya.

Agizo namba 18
Kamati iliagiza suala la migogoro ya ardhi kutatuliwa katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Mikoa na Wilaya imeshughulikia migogoro ya ardhi na tayari ipo iliyopatiwa ufumbuzi na mengine inaendelea kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

Hitimisho:
Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kukushukuru wewe binafsi na Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano mnayotupatia katika Ofisi yetu. Ninamshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wa kamati ya kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala kwa ushauri na maelekezo yao yanayotusaidia sana katika kufanikisha majukumu yetu. Ni imani yangu kwamba Wajumbe wamefuatilia kwa makini maeneo niliyoyatoa ambayo yamefafanua utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika ripoti yao ya mwaka 2012/13.
Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, kwa kazi kubwa uliyoifanya, na kwa kuwa muda uliobakia hautoshi, Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala watawasilisha ripoti zao kesho baada ya maswali na majibu. Ninawashukuru kwa ushirikiano huo.

Baada ya maelezo hayo ninaakhirisha kikao hiki hadi kesho siku ya Jumanne tarehe 28/01/2014 saa 3.00 barabara za asubuhi.

(Saa 1.40 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 28/01/2014 saa 3.00 asubuhi)